

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Nane – Tarehe 22 Juni, 2007**

*(Kikao Kilianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 67

**Wimbi la Watumiaji Dawa za Kulevyta Nchini**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, dawa za kulevyta zimekuwa zikikamatwa mara kwa mara na vyombo husika; na kwa kuwa vyombo vya habari hutangaza habari hizo; na kwa kuwa wahanga wa dawa hizo hasa vijana wanazidi kuongezeka:

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kudunmu wa kuwaelimisha watumiaji na hasa jamii, ubaya wa dawa hizo ili wasiendelee kutumia?
- (b) Je, Serikali imewahi kukamata kiasi gani cha dawa za kulevyta na ni wapi zinahifadhiwa?
- (c) Je, Serikali hutumia njia gani kuziharibu dawa hizo hatari?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli dawa za kulevya zimekuwa zikikamatwa mara kwa mara hapa nchini na matukio hayo hutangazwa na vyombo vyahabari kama yalivyotokea katika sehemu mbali mbali. Tanzania kama nchi nyingine duniani, inakabiliwa na tatizo hili la dawa za kulevya linaloonekana kuongezeka na kukithiri siku hata siku. Hata hivyo, Vyombo vyahabari vinaendelea kufanya kazi kubwa kuwabaini watumiaji na wahalifu wanaojihusiha na biashara hii haramu na kuwakamata.

Wapo waathirika wengi ambao idadi yao inaelekea kuongezeka kutokana na kuongezeka kwa tatizo lenyewe.

Juhudi kubwa zimeelekezwa katika kushirikisha jamii kuelewa na kudhibiti ili kukabiliana na usambazaji (*Supply Reduction*) na pia utumiaji (*Demand Reduction*). Ili kufanikisha suala hili, Elimu inatolewa kwa wananchi kwa kutumia mbinu mbali mbali kama zilivyoainishwa katika Mpango Kabambe wa Taifa wa Udhibiti Dawa za Kulevya (*The National Drug Control Master Plan*). Mpango ambao unatekelezwa chini ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya, kupitia Vyombo vyahabari mbali mbali, miadhara wakati wa mbio za Mwenge na Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani, ambako watu wengi wanaupata ujumbe unaowahu na kuwagusa walengwa. Vile vile machapisho mbali mbali yamesambazwa na kutolewa kwa wananchi yakiwa yamebeba ujumbe wa athari za dawa za kulevya. Aidha, semina, warsha makongamano kwa walengwa yanafanyika na sasa suala la dawa za kulevya limeingizwa kwenye Mitaala ya Shule za Msingi.

(b) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2003 hadi sasa, kiasi kilichokamatwa ni *Heroin* kilo 117, *Cocaine* kilo 6.6. Bangi tani 2,045 na Mirungi tani 28. Dawa hizo zinahifadhiwa na Jeshi la Polisi na kutumiwa kama vielelezo wakati wa maamuzi ya mahakama.

(c) Mheshimiwa Spika, mara nyingi dawa za kulevya huteketezwa kwenye Kiwanda cha Saruji cha Wazo Jijini Dar es salaam na hufanyika mbele ya wadau mbali mbali ikiwemo Mahakama, Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Wanamazingira, Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za kulevya, Mamlaka ya Chakula na Dawa, Idara ya Ushuru na Forodha, Washitakiwa na Mawakili wao na vile vile Vyombo vyahabari. Kwa upande wa mashamba ya bangi yanayogundulika, Serikali imekuwa iyateketeza mara moja na wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini, kilichonisukuma kuuliza swali hili ni kwa sababu nimeshuhudia ndani ya vyombo vyahabari, walipokuwa wanatekeza vifaa kwa mfano kama bunduki, wanatangaza na hata kwenye hivyo vyombo watu wanaviona. Sasa, sijawahi kuona mimi dawa za kulevya zikitangazwa kwenye vyombo vyahabari zikionyeshwa kama kwamba zinateketeza. Sasa ninachopenda kujua, kama zinateketeza kwa siri, tutaamini vipi kama kiasi kikubwa hiki kinachokuwa kimekamatwa kweli kinakuwa kinateketeza na kitanaangamia chote na siyo kwamba kinarudi tena katika mzunguko na kuwa ndizo dawa zinazoendelea kuuzwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mbunge kwamba kutokana na uwingi wa wadau wanaohusishwa wakati wa kuteketeza dawa hizi za kulevyta, ni wazi hakuna usiri ndani ya hilo. Isipokuwa kutokana na athari za moshi ambaa hutokea wakati wa uteketezaji huo, si rahisi kuonyesha au kuachia moshi huu utokee hadharani na hivyo huteketezwa kwenye tanuru la *cement* kule *Wazo Hill*. (*Makofi*)

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Napenda pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa Majibu yake mazuri. Mheshimiwa Spika, katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri amesema dawa za kulevyta huwa zinateketezwa kule *Wazo Hill*; na kwa kuwa Kiwanda cha *Wazo Hill* sasa hivi kimezungukwa na watu wanaoishi kule ikiwemo familia ya Mzee Kawawa: Je, dawa zile zinapochomwa, moshi wake hautadhuru wananchi wanaoishi karibu na eneo lile?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa utengenezaji wa saruji, uteketezaji wa dawa za kulevyta unalengwa kuhakikisha kwamba hauwafikii wale watu wanaozunguka kama ilivyo kwa vumbi la saruji ambalo hupeperuka angani, na hivyo hivyo ule moshi wa dawa za kulevyta hupeperuka angani.

Na. 68

#### **Upandishaji wa Hadhi Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi**

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali. Lakini, kabla sijauliza swali langu, kwanza naomba nifafanue kidogo kwa ajili ya kuweka rekodi zetu tu sawa sawa. Siku za karibuni nimekuwa naripotiwa kuwa mimi ni Juma Hassan Killimbah, Mbunge wa Iramba Mshariki. Mimi ni Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba (CCM).

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Kwa kuwa, uchumi wa Mkoa wa Mtwara unategemea sana barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala hadi Masasi; na kwa kuwa barabara hiyo inaunganisha Wilaya zote za Mkoa na ilisaidia sana kuimarisha biashara kati ya Tanzania na Msumbiji; na kwa kuwa, itakuwa ni utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais wa nchi wakati wa Kampeni za Uchaguzi:

- (a) Je, Serikali haioni kuwa sasa wakati umefika wa kuipandisha hadhi barabara hiyo iwe barabara kuu?
- (b) Je, Serikali itaanza lini kuiwekea lami barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, napenda kwanza kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Mtwara kuanzia mwaka wa fedha 2005/2006, imeishatumia jumla ya shilingi bilioni 2.782 ili kuifanyia matengenezo mbali mbali barabara hiyo kama ifuatavyo:-

Katika mwaka wa fedha 2005/2006, matengenezo makubwa kwa kiwango cha changarawe jumla ya kilomita 13.3 yalifanyika kwa gharama ya shilingi milioni 200 kati ya ya Mbawala na Maranje na kilomita 10 kati ya Mahuta na Newala kwa gharama ya shilingi milioni 191. Ukarabati pia umefanyika kwa kiwango cha lami kati ya Masasi na Chiwisi kilomita 7 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.335.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 kilomita 50 za barabara hiyo kati ya Maranje na Tandahimba zinafanyiwa ukarabati kwa gaharama ya shilingi bilioni 1.056. Ukarabati huu unatarajiwa kuendelea mwaka 2007/2008 kati ya Tandahimba na Newala na kuweka changarawe kati ya Newala na Masasi. Pamoja na ukarabati huu, matengenezo ya kawaida yataendelea kufanyika kila mwaka ili barabara hiyo isiharibike kwa haraka na iweze kupitika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swal la Mheshimiwa Juma A. Njwayo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a) Kama itakavyokumbukwa, Sheria ya Barabara imepitishwa na Bunge katika Mkutano wa Mwezi Aprili, 2007. Miiononi mwa mambo mengine, Sheria hiyo inaweka vigezo vya kupanga na kupandisha hadhi kwa barabara nchini. Hivyo, upangaji wa upandishaji daraja wa barabara nchi nzima utafanyika kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa katika sheria hiyo. Barabara ya Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi ambayo sasa ni barabara ya Mkoa, pia itaangaliwa kwa vigezo hivyo.

(b)Kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali haina mpango wa kuiwekea lami barabara hiyo, isipokuwa imeweka lami sehemu korofi za Namaleche, Nanyamba na pia sehemu ya Masasi. Serikali itaendelea kuifanyia matengenezo kwa kiwango cha changarawe barabara hiyo ili iweze kupitika majira yote ya mwaka.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swal la nyongeza. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yenye maelezo ya kutosha. Lakini, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza: Kwa sababu barabara hii huko nyuma ilikuwa barabara kuu, lakini yakafanyika makosa kui-

*down grade* ikawa barabara ya Mkoa. Je, sasa tathmini za kutosha za kuifanya kuwa barabara kuu zitazingatiwa? Pili, kwa sababu katika kikao cha RCC kilichofanyika hivi karibuni, tulikubaliana kwa pamoja na kwa ushauri wa Meneja wa TANROADS aliyeleo pale kwamba barabara hiyo inakidhi vigezo vya kuwa barabara kuu sasa. Je, Wizara inaahidi wananchi wa maeneo haya kuafikiana na ushauri unaotoka kwa wananchi kule chini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, nimeeleza kwamba upandishaji wa barabara hadhi zake utafanyika kwa kuzingatia sheria tulioipitisha Bungeni hivi karibuni. Lakini, kwa sasa inavyojulikana barabara kuu ambayo inaunganisha Mkoa wa Mtwara, Makao Makuu ya Mkoa wa Mtwara na Makao Makuu ya Mkoa wa Ruvuma ambayo ni Songea ambayo ndiyo kigezo cha kuwa barabara kuu ni ile inayotoka Mtwara kupitia mpakani mwa kuingia Lindi pale Mpapula hadi Mnazi Mmoja au Mingoyo na kuja kuingia tena Mkoa wa Mtwara pale Nanganga hadi Masasi kuelekea Tunduru hadi Songea.

Sasa kama hiyo barabara ya kwanza ilikuwa imeshushwa, bila shaka kilichoangaliwa ni kwamba hizi barabara zinakwenda *parallel* na kwa kawaida barabara ambazo karibu zinakwenda *parallel* kuzifanya zote kuwa barabara kuu si rahisi. Lakini nasema kama wadau na vile vile sheria mpya itakuwa imeona kwamba na hii barabara nyingine ambayo imetajwa kupitia Newala na yenye we iwe *Trunk Road* ama kwa kushusha ile nyingine, kwa kupandisha hii au zote mbili, ingawaje ninavyodhani kwa kweli barabara ambazo ziko sambamba na zote zinaunganisha Makao Makuu ya Mikoa miwili, kwa kawaida itakuwa moja inakuwa ya Mkoa, moja inakuwa *Tarunk Road*. Lakini tusubiri vigezo hivyo vya sheria ili tuweze kuona hali itakuwaje.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, barabara inayoombeva ya Mtwara – Tandahimba – Masasi – Nanyumbu iko jirani sana na Nchi ya Msambiji; na kwa kuwa ni nia ya Serikali kwamba tufungue mawasiliano na biashara na nchi jirani ya Msambiji; na kwa kuwa barabara inayosemekana ya lami inafika Mtwara, eneo kubwa linatembea Mkoa wa jirani siyo Mtwara; na kwa kuwa Serikali nia yake ni kutuwezesha kupata usafiri wa urahisi. Je, Serikali inaweza ikaahidi kwamba hali ya fedha itakaporuhusu, itaijenga barabara hii kwa lami ili iweze kuungana na Songea na mpaka *Mbamba Bay* ili mizigo ya watu wa Ruvuma na Mtwara ipitie Bandari ya Mtwara? (*Makofi*)

**NAIBU WA ZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kama alivyosema mwenyewe, tatizo kubwa ni ufinyu wa Bajeti na si kwamba kama uwezo upo hatuwezi kujenga baadhi ya barabara za mikoa kwa lami. Kwa hiyo, kama uwezo utakuwepo na umuhimu utakaokuwepo wakati huo, kama ambavyo ameellezea vizuri, Serikali itafikiria hilo. Lakini, kwa sasa uwezo wa kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami hakuna.

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa waolikuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walilalamika sana katika kudai stahili zao kwa muda mrefu uliopita. Je, suala hilo limefikia wapi hadi swali hili linajibowi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi sasa Serikali imeweza kulipa jumla ya wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki wapatao 36,405 ikiwa ni Jumla ya madai ya miradhi pamoja na walio hai. Kati ya hao, wastaafu 31,612 ni wa madai ya uchambuzi wa mwanzo na wastaafu 4,793 ni madai mapya. Kati ya wastaafu hao 36,405, wastaafu 6,888 hawajajitokeza kuchukua mafao kwenye Benki za *NMB* na *CRDB* licha ya majina yao kutangazwa kwenye magazeti. Wastaafu hao ambao hawajajitokeza wanaombwa kujitokeza na kuchukua mafao yao.

Mheshimiwa Spika, upungufu/ukosekanaji wa nyaraka muhimu kutoka kwa waajiri ndiyo sababu kubwa ya ucheleweshaji wa malipo hayo. Nyaraka hizo zinatakiwa kuwasilishwa na Mwajiri kwa ajili ya uthibitisho wa malipo hata kama mtumishi mwenyewe atakuwa na nakala ya kumbukumbu za nyaraka hizo. Hii ni kutohana na kuhakikisha malipo hayo kweli ni ya walengwa kwani wapo watumishi/watu wasiokuwa waaminifu ambao wamediriki kugushi nyaraka hasa za marehemu ili kujipatia fedha kwa njia ya udaganyifu.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa wastaafu wataendelea kuwepo katika nchi yetu kwa kuwa kuna wafanyakazi; na kwa kuwa wastaafu hao wa Afrika Mashariki wamekumbana na misukosuko mingi mpaka kupata haki zao na wengine kufikia hatua ya kufariki. Je, Serikali sasa inajiandaa vipi kuhakikisha kwamba usumbufu kama huu hautokei tena kwa wastaafu watakaofuata siku za usoni? Swali la pili, kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge ni Viongozi wa Kitaifa na kumbukumbu zinatuonyesha kwamba asilimia kubwa ya Waheshimiwa Wabunge ambao baada ya kumaliza muda wao wanakabiliwa na hali ngumu ya maisha; na kwa kuwa aibu ya kiongozi wa kitaifa akishastaafu ni aibu ya Serikali. Je, hamuoni sasa kwamba ni wakati muafaka mkaleta sheria humu Bungeni ili Waheshimiwa Wabunge wanapostaaafu waweze kulipwa hata nusu mshahara ili kumudu angalau maisha yao kuweza kupata hela ya mafuta ya taa na dagaa? (*Makofî/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):**  
Mheshimiwa Spika, Wastaafu wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ndio hao niliotaja na waliosalia ni kama hao niliowataja. Serikali inasubiri tu wenywewe kama wako

hai au wale ambao wamefariki, warithi wao waje wachukue mafao yao. Kuhusu Wabunge, kama mnavyojua mambo yote ya pensheni ikiwa ya Wabunge, ikiwa ya Wafanyakazi, yote yana sheria zake. Kwa sasa Serikali haiwezi kusema kwamba tuwafikirie Wabunge tu wakati kuna wastaafu ambao Waheshimiwa Wabunge katika mjadala wa Bajeti hii wamesema imefika hadi ya wao vile vile kwa sababu nao wametoa mchango wao katika nchi hii wafikiriwe kupata chochote. Mara zote tunasema hali ikituhusu tutafanya hivyo. Kwa hiyo, tunafikiria wale tunaowatumikia kwanza, halafu baadaye kama itatokea haja, basi na Wabunge nao pengine watafikiriwa waletewe Bajeti hiyo.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wastaafu wengi hivi sasa ni wazee sana, wengine ni wagonjwa hawana uwezo; Utaratibu wa sasa wa Hazina ni kuwataka wazee hawa waende Dar es salaam ndio wakalipwe mafao yao; Naiarifu Serikali, wazee hao hawawezi kusafiri, hawana fedha, wagonjwa. Serikali inaonaje kama itaweka utaratibu wa kuwalipa wastaafu hawa huko huko waliko hususan kwenye Makao Makuu ya Mikoa yao kama vile Tabora, Mwanza, Kigoma na kadhalika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Spika, hili pamoja na barua yake ambayo ameuliza hayo hayo, nimemwambia katika barua yake na hapa namjibu tena kwamba wastaafu walioko Mikoani kwamba wajaribu wafanye kila njia, kuna *Sub-Treasury* zetu. Baada ya kupata hati zile za waajiri walipokuwepo, Mashirika walipokuwepo maana ndio ushahidi kamili kwamba walajiriwa huko, wazipeleke *Sub-Treasury*, na hizo Hazina Ndogo ndizo zitachukua hatua za kupeleka madai yao Treasury. Mlolongo mrefu niliokuelekeza na nitakuomba utusaidie kama Serikali, ningependa uchukue japo kuwa mlolongo ni mrefu. Kwa sababu ni mrefu, wale ambao vile vile wana shida, tunaweza kuwatolea nakala ni yepi yafanyike ili mstaafu aliyefariki au aliye hai hatua gani achukue ili apate fedha zake kule kule mkoani aliko. (*Makofî*)

Na. 70

#### **Hitaji la Huduma ya Benki – Nanyumbu**

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA** aliuliza:-

Kwa kuwa Nanyumbu ni moja ya Wilaya katika Mkoa wa Mtwara zinazozalisha sna Korosho na mazao mengine ya biashara kama ufuta na karanga; na kwa kuwa hakuna huduma yoyote ya kibenki katika Wilaya hiyo hali inayosababisha wananchi Wilayani humo kutunza fedha zao sehemu zisizo na usalama:

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha Benki zilizopo hapa nchini kujenga matawi yao Wilayani humo?

- (b) Je, kwa wakati huu ambao hakuna huduma hiyo Wilayani humo, Serikali itawasaidiaje wananchi ili waweze kutunza fedha zao sehemu zenye usalama?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kufuatia mabadiliko ya mfumo wa kifedha *nchini* (*Financial Sector Reforms*) unaotekelezwa na Serikali kuanzia mwaka 1991, ni azma ya Serikali kujitoa katika kuhusika moja kwa moja na biashara ikiwemo ya Benki na kuwezesha wananchi kuanzisha na kusimamia shughuli hizo wao wenyewe. Pia, katika mfumo wa soko huria, wawekezaji hupendelea kuwekeza katika maeneo yanayoonekana kuwa na faida kwao. Si busara kwa Serikali kuwalazimisha wawekezaji kuwekeza katika maeneo ambayo hawako tayari kuingia.

Hata hivyo, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu Wilayani Nanyumbu ili iwe kivutio kwa Benki nchini kufungua matawi yake Wilayani humo. Pia tutahamasisha Benki kufanya hivyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kuwasaidia wananchi kutunza fedha zao sehemu yenye usalama, Serikali inapenda kuwahamasisha wananchi wa Nanyumbu kutumia fursa hii ya mazingira mazuri ya uchumi endelevu yanayoendelea kuwekwa na Serikali, pamoja na sheria zinazosimamia uanzishwaji na uendeshaji wa Benki na Taasisi za fedha, kuungana pamoja na kuanzisha Benki yao kama vile *Community Bank*. Benki Kuu iko tayari kuwapa ushauri.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kuendelea kuboresha miundombinu katika kuweka mazingira ya kiuchumi, sheria na miongozo imara itakayowawezesha wananchi kuungana na kuanzisha Benki au Taasisi za Fedha katika maeneo yao. Hatua hii itasaidia kutatua tatizo linalowakabili wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu na maeneo mengine yenye matatizo kama hayo nchini. (*Makofsi*)

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo kidogo hayakuniridhisha. Wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu hasa walimu, wanapata tabu sana kusafiri mwendo mrefu kwenda Masasi, wanaacha shughuli zao, wanafunzi wanakaa bure siku nyingi bila kusoma, wanunuzi wako hivyo hivyo, wanapata taabu.

Sasa kupitia Bunge hili, kwana nayaomba Mashirika ya Benki kama wapo humu watafute sasa uwezekano wa kufungua mabenki pale Nanyumbu, lakini je, Mheshimiwa Naibu Waziri kupitia Wizara yako tunakuomba uhamasishe mabenki haya haraka ili waweze kufungua mabenki hayo pale Nanyumbu hasa pale Mangaka. Je utatusaidia kufanya hivyo haraka iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwanza Serikali inaandaa mazingira mazuri katika Wilaya ya Nanyumbu ili kuyahamasisha mabenki yaweze kuja Nanyumbu kufungua mabenki kule. Lakini pia tungependa kushauri Wilaya ya Nanyumbu kama wananchi wenyewe mngeweza mkaungana mkaanzisha Benki ya Wananchi. Mifano mizuri ni kama Wilaya ya Mbinga, Wilaya ya Mwanga, Wilaya ya Mufundi na Dar es Salaam ambako mabenki haya ya wananchi yamekuwa na mafanikio makubwa sana. Kwa hiyo, pamoja na Serikali kuandaa mazingira mazuri, pamoja na Serikali kushawishi mabenki yaje Nanyumbu, nakushauri Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri yenu jaribuni kuona kama kuna uwezekano wa kuweza kuanzisha Benki ya Wananchi pale Nanyumbu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na karibu hujakuwepo humu ndani kwa muda. Swalii la nyongeza.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, naomba na mimi niulize swalii la nyongeza kwa sababu hali ya Nanyumbu haina tofauti sana na hali ya Kilindi na kwa kuwa kilio cha muda mrefu ndani ya Wilaya ya Kilindi ni benki tukiwa na rasilimali mbalimbali na fedha nyingi ndani ya majumba yetu na kwa vile Wizara ya Fedha na kwa msukumo wako wewe mwenyewe Naibu Waziri Mkulo, tumeweza kongea na *NMB* na wakakubali kufanya hilo. Lakini hadi leo pamoja na kuandaa jengo hakuna kilichofanyika. Je, utawaambiaje wananchi wa Kilindi ili waweze kuwa na matumaini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, hilo tunalifahamu, *NMB* iko tayari. Hapo nje kuna *Public Relations Manager* wa *NMB*, nashauri baada ya kumaliza kikao hiki wewe, mimi na yeye tuzungumze ili tuone jinsi gani tutaweza kukusaidia. (*Makofsi*)

**SPIKA:** Kwa nini amekaa nje, si angeingia tu akasikiliza. (*Kicheko/Makofsi*)

Na. 71

### **Kuondolewa kwa Kidato cha I – IV Nganza**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2004 kulitokea mabadiliko yaliyotokana na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (*MMES*) ya kupunguza nafasi za wanafunzi wa kike kuingia Kidato cha Kwanza hadi cha Nne katika shule ya wasichana Nganza, hali iliyosababisha mlundikano wa wanafunzi wa kike katika shule ya Bwiru na kwa kuwa sababu zilitolewa kuwa, lengo ni kufikia mwaka 2009 kuwezesha asilimia hamsini (50%) ya wanaomaliza Kidato cha Nne kupata nafasi ya Kidato cha Tano.

Hali iliyohitaji upanuzi wa nafasi za Kidato cha Tano na Sita na kwa mpango huo umeathiri mambo mengi ikiwa ni pamoja na wanafunzi kukosa nafasi ya kwenda Bweni na kusababisha mlundikano Bwiru, kwa kuwa, Mwanza ina shule mbili tu za bweni kwa wanafunzi wa kike:-

(a) Je, kwa hitilafu hizo zilizojitokeza Serikali haioni kuna haja ya kufuta mabadiliko hayo ili shule hiyo iendelee kupokea wanafunzi wa Kidato cha I-IV?

(b) Kwa kuwa Kidato cha I – IV kiliondolewa bila ya maandalizi ya kutosha kwa walimu waliokuwa wanafundisha madarasa hayo, hali iliyosababisha kuyumba kwa ajira zao mpaka sasa. Je, Serikali ina mpango gani kwa hilo?

**NAIBU WAZIRI ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mabadiliko yaliyotokana na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (*MMES*) ya kupunguza nafasi za wanafunzi wa kike kuingia Kidato cha Kwanza hadi cha Nne Shule ya Sekondari ya Nganza yelitekelezwa kwa mtindo wa *phasing out* kuanzia mwaka 2005 kwa kutochukua wanafunzi wa Kidato cha Kwanza. Hakuna wanafunzi waliohamia katika shule ya sekondari ya Bwiru kutoka Nganza Sekondari, hivyo hakuna hitilafu zozote zilizotokea katika Shule ya Sekondari ya Bwiru Wasichana kutokana na mabadiliko hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mabadiliko haya yalifanyika kwa mtindo wa *phasing out* walimu nao walikuwa wanahamishiwa katika shule nyininge kwa utaratibu huo huo. Kwa hivyo hakuna mwalimu ambaye ajira yake iliyumba. Utaratibu huu umesaidia pia kuzipatia walimu shule mpya zinazokuwa katika mkoa wa Mwanza.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Mkoa wa Mwanza una shule za sekondari za Serikali 222 na kuna shule za watu binafsi 29. Kwa hiyo Mkoa wa Mwanza una shule za sekondari 251. Tukizingatia kwamba nimezungumzia suala la wasichana, Mkoa wa Mwanza kuna shule za sekondari za bweni mbili tu ningeanza na Bwiru.

Mheshimiwa Spika, Waziri haoni sasa hawatendei haki wasichana wa mkoa wa Mwanza kutokupata nafasi nyangi za kuingia katika shule za sekondari hizi alizopunguza shule ya Nganza kwa kuwa shule ile ni ya bweni, wanapunguziwa nafasi ya kuingia kuendelea na shule hizo? (*Makofi*)

La pili, Mheshimiwa Spika, kwa sababu hali hii ipo Bwiru na mimi natoka Mkoa huo wa Mwanza, je Mheshimiwa Waziri yuko tayari tukaongoza na yeze twende moja

kwa moja mpaka Bwiru tukaone hali ya mlundikano wa wasichana walivvolundikana pale? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba shule za sekondari za bweni za kitaifa ni Bwiru na Nganza na wanafunzi wanaosoma pale ni wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania sio Mwanza peke yake.

Kumbe hizi ni shule za kitaifa na wala siyo sababu ya kulundikana wanafunzi wasichana katika shule hizo. Ndio maana Serikali ya Awamu ya Nne inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete, imesisitiza ujenzi wa shule za Kata na kuwahimiza wazazi wajitahidi kadri ya uwezo wao waweze kujenga mabweni ili wanafunzi na wao wasichana waweze kupata mahali pa kukaa ili waweze kwenda kusoma kama wanafunzi wengine.

Kumbe tunahimiza Halmashauri na wananchi kwa ujumla tushirikiane na Serikali ili kujenga mabweni katika shule hizi zilizojengwa kwa wingi ili tuweze kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wa kike na wa kiume wanasona katika shule hizi.

Kuhusu ombi la Mheshimiwa Mbunge, tuweze kuongozana ili kuweza kwenda kuangalia mlundikano wa wanafunzi katika shule hizi. Suala hili tunalifahamu. Tatizo linalojitokeza wazazi wengi wanapoona watoto wao wamepangwa katika shule hizi za Kata au shule hizi ambazo ni *Day Schools* wanaendelea kuomba watoto wao wapelekwe katika shule za bweni, ndiyo maana tunapata matatizo ya mlundikano.

Lakini wapo wanafunzi wengine ambao wanakwenda pale kwa sababu ya matatizo mbalimbali. Tunaendelea kushauri wananchi waendelee kuwa na mpango wa kushirikiana kujenga mabweni katika shule zao na Serikali itashirikiana nao kwa sababu fedha zinazopatikana zitakuwa ni kushirikiana na wananchi ili tuweze kujenga mabweni au tuseme *hostel* katika shule mbalimbali ili tuweze kupunguza mlundikano huo unaopatikana katika shule hizi.

Pamoja na hayo, nipo tayari kuweza kuongozana tuende tukathibitishe hilo suala. Ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 72

### **Tatizo la Uvujaji wa Mitihani**

**MHE. LUCY T. MAYENGA (K.n.y. MHE. AMINA C. MPAKANJIA)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa suala zima la uvujaji wa mitihani ya kitaifa limekuwa kero kubwa kwa wanafunzi, maana wengi wao wanafaulu mitihani kwa kutotumia akili zao ikiwa ni baada ya kufanyiwa na walimu au watu wengine:-

- (a) Je, kuna urasimu gani katika kulitatua tatizo hilo?
- (b) Je, Serikali ya Awamu ya Nne ina mipango au mbinu gani za kulimaliza tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hakuna urasimu wowote katika kutatua tatizo la uvujaji wa mitihani ya kitaifa. Uvujaji wa mitihani maana yake ni karatasi za maswali au baadhi ya maswali ya mitihani kuonekana kabla ya muda uliopangwa kufanyika. Kwa hivi sasa tatizo hilo limedhibitiwa kwa kiwango kikubwa. Kilichopo sasa ni matukio machache ya udanganyifu ambayo hufanyika ndani ya vyumba vyta mitihani. Serikali imekuwa ikichukua hatua dhidi ya udanganyifu katika mitihani ikiwa ni pamoja na kuwafutia matokeo ya mitihani wale waliobainika kuhusika na udanganyifu huo. Aidha, hatua za kinidhamu zimekuwa zikichukuliwa kwa wote wanaobainika kuwasaidia wanafunzi kudanganya katika mitihani ikiwa ni pamoja na kuwavua madaraka waliohusika na udanganyifu huo.

(b) Mheshimiwa Spika, mipango au mbinu mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali za kupambana na kudhibiti udanganyifu katika mitihani ni pamoja na:-

- v Kubadili mfumo wa usimamizi wa mitihani ambapo msimamizi haruhusiwi kusimamia shule anayofundisha;
- v Kutoa semina na maelekezo kwa wasimamizi siku chache kabla ya mitihani kuanza;
- v Kuendelea kuwahimiza wamiliki wa shule na vyuo kujenga kumbi za kufanya mitihani ili kurahisisha kazi ya usimamizi;
- v Kuongeza Bajeti ya Baraza la Mitihani ili kuboresha usimamizi wa mitihani;
- v Kuendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ili kuwawezesha wanafunzi kujiamini zaidi wanapofanya mitihani;
- v Kuelimisha wadau na wananchi wote kwa ujumla kuhusu madhara ya udanganyifu katika mitihani kwa lengo la kuwashawishi

wajihusishe kikamilifu kupiga vita vitendo vyta udanganyifu katika mitihani na mwisho; na

- v Kuchukua hatua kali zaidi kwa mujibu wa sheria kwa wanaobainika kuhusika na udanganyifu wa mitihani, ikiwa ni pamoja na kuwapeleka katika vyombo vyta dola.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mitihani ya Baraza la Mitihani pamoja na ile ya Darasa la Saba na kwa kuwa wanafunzi wanaomaliza darasa la saba ndiyo wanaojiunga na kidato cha kwanza wale wanaochaguliwa na kwa kuwa matokeo ya kidato cha pili yameonyesha kwamba watoto wengi wanafeli na hulazimika kurudia badala ya kupanda darasa.

Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba wale watoto wanaochaguliwa kwenda kidato cha kwanza kunakuwa na mitihani tu wa kuwachuwa mara wanapoingia ili wale ambao kulifanyika na vitendo vyta kuwafanya mitihani kwenye vyumba vyta mitihani na ikaonekana wamechaguliwa waweze kurudishwa na hizo nafasi kupewa wale ambao wangestahili kuzipata?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru kwa namna ya kipekee ambavyo ameguswa zaidi na maswala haya ya mitihani. Nampongeza sana. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tayari Wizara yangu imeshafanya kazi marekebisho na mwaka kesho kutakuwepo na mitihani mara baada ya wanafunzi waliochaguliwa kidato cha kwanza itakapofika mwezi wa tatu, kutakuwa tena na mitihani na mitihani huo utakapobaini kwamba waliofanya vibaya watarudishwa kwa sababu hicho kitakuwa ni kigezo kizuri cha kuweza kudhibiti badala ya kugonja mpaka watakapofika kidato cha pili na wengi wao kukariri. (*Makofi*)

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameleeza kwamba kuvuja kwa mitihani kwa kweli wameweza kukabiliana kwa kiwango kikubwa, hii inaonyesha kwamba hata kwamba kiwango kidogo mitihani hiyo inavuja, na kwa kuwa wanaoshughulikia mitihani wanaishi kwa muda mrefu katika sehemu hiyo ya mitihani haoni kwamba itazuia zaidi kwa kuweka kiwango maalum watu wale wanaoshughulikia mitihani na kuondoka na kuweza kukaa wengine ili wasijenge usoefu katika sehemu hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, naomba kumthibitishia kwamba mitihani hivi sasa haivuji na nimeshueleza katika swali langu la msingi maana ya kuvuja kwa mitihani. Matokeo yaliyobainishwa ni udanganyifu.

Mheshimiwa Spika, naomba niliarifu tena Bunge lako Tukufu kwamba utaratibu umefanyika wa kuwabdalisha vituo vyta kazi ikiwa ni pamoja na watumishi

waliokuwepo Baraza la Mitihani muda mrefu na bado tunaendelea kufanya uchunguzi kuona wale wote ambao si waaminifu na si waadilifu kuwaondoa ili kulijengea taifa hili heshima kubwa. (*Makofi*)

Na. 73

### **Miradi ya Umwagiliaji**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

- (a) Je, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika inasema nini juu ya miradi ya umwagiliaji ya Mwangeza na Msingi ambayo imeharibiwa na mafuriko makubwa yaliyosababishwa na mvua za mwaka huu?
- (b) Je, Serikali haioni kwamba, ni muhimu kuifanyia ukarabati kwa faida ya wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, naomba kutoa maelezo mafupi sana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kati ya mwezi Novemba, 2006 na Februari, 2007, mvua nyingi zilinyesha katika maeneo mengi ya nchi na mafuriko yaliharibu miundombinu nyingi ikiwemo ya umwagiliaji maji mashambani.

Baada ya mvua kwisha, Wizara yangu imefanya tathmini ya uharibifu uliotokana na mafuriko ili kubaini miradi inayoweza kufanyiwa ukarabati wa muda mfupi kuwawezesha wakulima kuendelea na kilimo katika msimu unaofuata. Tathmini ya Wizara yangu imeonyesha kwamba miundombinu ya skimu za umwagiliaji 50 katika nchi nzima zikiwemo skimu za Mwangeza na Msingi iliharibiwa. Gharama ya kukarabati miundombinu hiyo imekadiriwa kuwa shilingi bilioni 5.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Msindai, lenye sehemu (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekwishakagua miradi ya umwagiliaji ya Mwangeza na Msingi na kubaini kwamba ili kukarabati miundombinu ya skimu hizo, skimu ya Mwangeza inahitaji shilingi 143,831,125 kwa ajili ya kukarabati bwawa lililobomoka na mifereji ya maji. Aidha, skimu ya msingi ambayo tuta lake la kuzuia mafuriko (*flood dyke*) liblomoka linahijitaji shilingi milioni 30. Tayari, maombi ya fedha yamekwishafanywa kupitia Mpango wa Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya ya Iramba (*DADPs*), 2007/2008.

Aidha, napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara yangu imefanya uchunguzi zaidi katika skimu ya Msingi na kubaini kuwa kwa kutumia Mto Ndurumo pamoa na kuvuna maji ya mvua kwa kujenga bwawa, skimu ya Msingi inaweza kupanuliwa na kumwagilia hekta 400 badala ya hekta 200 za sasa.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaangalia uwezekano wa kutekeleza kwa awamu mradi huu unaokadiria kugharimu shilingi bilioni moja kupitia katika *basket fund* ya Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo – *ASDP*.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa majibu ya Waziri yameonyesha kwamba maeneo hayo ya Mwangeza na Ndurumo kuna uwezekano wa kupanua skimu za umwagiliaji. Swali la kwanza. Kwa kuwa karibu na skimu ya Mwangeza kuna Mto Msu ambao nao unaweza kumwagilia hekta zaidi ya 500. Je, Waziri atakuwa tayari kuwatuma wataalam wakachunguze ili tutumie maji hayo yasipotee bure?

Swali la pili, swali la pili kwa kuwa kwenye Mto Ndurumo Wajapan waliokuwa wanatengeneza Mradi wa *Lower Moshi* walikwenda wakafanya uchunguzi na wakabaini kwamba kunaweza kuwa na hekta 2,400 ambazo zinaweza kumwagiliwa, haya maji yakikingwa sehemu ya Kinyangiri kwenye mto huo huo Ndurumo. Je, Serikali itakuwa tayari pia kwenda kufanya utafiti juu ya skimu hizo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara yangu itawatuma Wahandisi kwenda kukagua Mto Msu na huo mto mwininge ambao ameutaja kwa maana ya skimu yenye hekta 4,200 iliyokwishafanyiwa upembuzi yakinifu zamanii na Wajapan. Tutatuma wataalam wetu wa Kanda ya Manyara na watakwenda kama walivyofanya kwenye miradi hiyo mingine niliyoisoma kwenye majibu yangu ya msingi watakagua na tutaendelea kuiweka katika taratibu za kuendeleza miradi. (*Makofi*)

Na. 74

#### **Ugonjwa wa Kahawa – Mashambani**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa kahawa ndilo zao kuu la biashara kwa wakulima wa Wilaya ya Mbozi; na kwa kuwa hivi karibuni kumezuka ugonjwa unaoshambulia mibuni na kuikausha kabisa na kwa kuwa wataalam wa kilimo Wilayani wanasema ugonjwa huo hauna dawa na ukiingia shambani dawa ni kung’oa Mibuni iliyoshambuliwa:-

- (a) Je, huo ni ugonjwa gani, na ni kweli kuwa, hauna dawa?

(b) Kama kweli hauna dawa na haujulikani. Je, Serikali itakuwa tayari kuwatuma wataalam wake wakafanye utafiti wa kina ili kujua aina ya ugonjwa huo kwa lengo la kukabiliana nao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Jimbo la Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, visumbufu na magonjwa ya kahawa yenye uwezo wa kukausha mibuni ni pamoja na ugonjwa wa mnyauko fuzari, kutu ya majani (*coffee leaf rust*), wadudu aina ya bungua mweupe wa kahawa (*white coffee stem borer*), vidung'ata (*mealy bugs*), vidugamba (*green scales*) na kidomozi (*leaf miner*). Sababu zingine ni upungufu wa rutuba katika udongo. Aidha, ukame wa muda mrefu na mibuni yenye wekuzaa sana (*over bearing*) ni sababu zingine ambazo zinaweza kufanya mibuni kukauka. Kati ya magonjwa hayo niliyoyataja hapo juu mnyauko fuzari ndio ambaa hauna dawa. Lakini hadi sasa ugonjwa huu uko katika Mkoa wa Kagera tu na kwa kahawa aina *robuster* tu.

(b) Mheshimiwa Spika, ilipoanzishwa programu ya kuendeleza zao la kahawa Wilayani Mbozi katika miaka ya tisini, wataalam wa utafiti wa kituo cha utafiti wa zao la kahawa (*TACRI-Lyamungu*) wamekuwa wakitembelea Wilaya ya Mbozi ili kutafiti na kuyapatia ufumbuzi matatizo mbalimbali ya kahawa katika Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Spika, ili kusaidia wakulima wa kahawa kwa karibu zaidi *TACRI* imeweka Wilayani Mbozi mtaalam aliyebolea katika kilimo cha kahawa. Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kuwa kwa tukio hilo lililozuka hivi karibuni kama swalii lake linavyojieleza, wataalam wa utafiti wa kahawa wataendelea kufanya utafiti wa kina ili kujua aina ya ugonjwa huo kwa lengo la kukabiliana nao.

Aidha, Wizara yangu ingependa kuwashauri wakulima wa kahawa nchini wakiwemo wakulima wa Wilaya ya Mbozi, kuanza kupanda miche mipyaa ya kahawa, inayozalishwa na kituo cha utafiti cha *TACRI-Lyamungu*, ambayo ina sifa ya kutoa mazao zaidi na pia kuhimili magonjwa kama hayo niliyotaja. Kwa kuanza kupanda miche hiyo baada ya muda, zao la kahawa litaongezeka kwa vile gharama za kutunza aina hii ya miche ni nafuu zaidi kuliko ile ya zamani.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba niulize maswali mawili kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, kwa kuwa uzalishaji wa miche mipyaa ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameitaja wakati akijibu swalii langu, inazalishwa hata kule Mbozi kwenye kituo cha *TACRI* pale Mbimba lakini kwa uzalishaji wake ni kidogo sana hauwezi kukidhi mahitaji ya wakulima wa Wilaya ya Mbozi. Je, Wizara ina mkakati gani wa

kuhakikisha kwamba hii miche inazalishwa kwa wingi zaidi ili iweze kukidhi mahitaji ya wakulima wa Wilaya ya Mbozi?

Swali la pili, kwa kuwa miche hii inauzwa kwa wakulima. Je, Serikali kama njia ya kuhamasisha wakulima waweze kuzalisha zaidi, itakuwa tayari badala ya kuiiza miche hii ikatolewa bure kwa wakulima hawa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa miche ya mibuni ambao hivi sasa unafanyika kule katika kituo kidogo cha Mbimba, kwanza nafikiri ingekuwa ni vizuri nimpongeze Mheshimiwa kwamba yeye ni mmojawapo tu katika vituo vichache ambavyo tayari vimeshaanzishwa katika mikoa ukiacha kile cha *TACRI*. Kituo kingine kidogo kimeanzishwa kule Kigoma. Sasa mimi ningemshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba awahamasishe, tushirikiane kuhamasisha wakulima katika Wilaya ile ya Mbozi. Kwanza kabisa kuunda vikundi vyta uzalishaji. Vikundi hivi vitafanya mambo mawili:-

Moja, vikundi vitaweza kupatiwa elimu ya kuzalisha miche hii ili wenyewe waweze kuvizalisha katika mashamba yao kule kule kwa ajili ya kupunguza gharama. Lakini pia vikundi hivi vinao uwezo kuweza kupata mikopo kama vitakuwa vimesajiliwa vizuri itakayowawezesha kumudu gharama hizi za kuzalisha miche hii. Naomba pia nimshauri Mheshimiwa kwamba tutaendelea kuweka mipango yetu katika mipango ya maendeleo ya kilimo ya wilaya, kwa ajili ya kueneza mbegu hizi.

Kuhusu kuitoa bure Mheshimiwa Spika, mimi nasita kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali sasa itaanza kugawa miche bure. Kwa sababu kwa kufanya hivi hatutakuwa tunajenga uwezo ambao ni endelevu. Mimi naomba tukubaliane tu kwamba vikundi vyetu hivi vipate utaalamu hata *TACRI* wanakubali kabisa kufanya mafunzo na hatimaye vikishapata uwezo kupitia kwenye *SACCOS* na kupitia kwenye taratibu zingine basi vikundi hivi vitaweza kujidesha vyenyewe bila kutegemea Serikali kila wakati.

Na 75

### **Askari Polisi kwenda Vituo vya Mijini na Vijijini.**

**MHE. ANNE K. MALECEL**A aliuliza.

Kwa kuwa vituo vya Polisi viro Mijini na Vijijini; na kwa kuwa baadhi ya Polisi Mijini wanaishi kwenye nyumba za Polisi tofauti na wale wa vijijini ambao wanaoishi kwenye nyumba za kupanga:-

- (a) Je, mishahara na marupurupu ya wale askari wa mijini na wale wa vijiji inatofautiana?
- (b) Kama inatofautiana. Je, inatofautiana kwa kiasi gani?

## **NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia napenda kumjibu Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mishahara na posho mbalimbali za askari wanaofanya kazi mijini na wale wa vijijini haitofautiani. Kila Askari Polisi hulipwa mishahara kulingana na cheo chake na kwa mujibu wa viwango vinavyotokana na muundo wa mishahara wa Jeshi la Polisi bila kujali askari huyo anafanya kazi eneo gani la nchi.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa jibu fupi sana la Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini limenipa elimu. Naomba ruhusa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Same ina Tarafa nne ambazo zote ziko milimani na ninashukuru wewe mwenyewe umekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro unajua hilo, Mheshimiwa Sarungi, Mheshimiwa Kimiti wanalifahamu hilo. Tarafa zote hizo nne zina Kata za Serikali 16 na zaidi ya asilimia 65 ya wananchi wa Wilaya ya Same wanaishi milimani, lakini hakuna kituo cha Polisi hata kimoja. Je, Serikali haioni kwamba wananchi hawa maisha yao yanakuwa kidogo katika hali isiyo ya usalama wao pamoja na mali zao kwa hiyo wakaona umuhimu japo wa kuanza kujenga kituo kimoja cha Polisi?

Swali la pili, Mheshimiwa Spika, huku milimani kunatokea matukio mengi sana kama kawaida, na mara kwa mara matukio haya yako tokea unakuta askari wa kutoka tambarare kama vile Kihurio au Ndungu ndiyo wanaopanda milimani kwenda kutatua matatizo hayo. Lakini askari hao wanapanda kwa miguu na kazi ile ni ngumu sana kupanda milimani kwa miguu.

Kulingana na jibu la Mheshimiwa Waziri inaonyesha mijini wanalipwa mishahara na marupurupu sawa na vijijini. Je, Serikali haioni kwamba hawa askari ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu ni bora ikawaangalia kuliko ambavyo inawalinganisha na wale wanaofanya kazi mijini? (*Makofifi*)

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, naomba nimjibu Mheshimiwa Anne Kilango Malecela swali lake la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa Anne Kilango kwa jitihada zake anazofanya kushirikiana na Askari wetu wa Polisi kule Same pamoja na kushirikiana na Wizara ya Usalama wa Raia.

(a) Ni nia ya Serikali yetu kujenga Vituo vya Polisi katika maeneo mbalimbali nchini kama nilivyojibu katika majibu yangu ya nyuma, nasema hivi, sasa Serikali kupitia Jeshi la Polisi inafanya tathmini ya kina ili kujua maeneo mbalimbali yanayopaswa kujengwa Vituo vya Polisi kufuatana na vigezo vya Kipolisi.

Namwomba Mheshimiwa Anne Kilango Malecela aendelee kuvuta subira wakati tunaendelea kushughulikia suala hili ili tutatue suala hili ambalo amelionyesha.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kweli kuwa na vituo katika maeneo yaliyo nje ya miji yetu lakini naomba atusubirie tufanye kazi hiyo.

Kwa upande wa magari, nia yetu ni kuhakikisha kwamba kila kitu kinapata magari na katika tathmini hiyo tunafanya pia kuweza kujua magari yaliyopo katika kila kituo ili tuwe na uwiano mzuri wa kugawa magari katika vituo vyetu mbalimbali hapa nchini. Namwomba pia Mheshimiwa Mbunge nalo hili avute subira.

Kuhusu suala la marupurupu, kama alivyosema, kwa kawaida Askari hawa wote wa mijini na vijiji wanafaya kazi katika mazingira magumu sana na hivi sasa Tume ya Rais inayoshughulikia maboresho ya Askari wa Polisi tayari imeshafanya kazi kwa upande wetu na tayari taarifa hizi ziko Serikalini. Naomba Mheshimiwa Mbunge asubiri yale ambayo Serikali itaamua kwa ajili ya maslahi ya Askari wetu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na lilibaki swalii moja ambalo ningeweza kuruhusu lijibiwe, lakini nahisi linazo nyongeza nyongeza hivi, kwa hiyo, nitalisogezza siku nyingine. Matangazo ni kama ifuatavyo:-

Wageni tulionao ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa John Paul Lwanji ameniomba niwatambushe wageni wake ambao ni Obeid Lwanji na Wilson Lwanji, Walimu wa Shule za Msingi kutoka Jimboni kwake kwenye maeneo ya Itigi.

Naomba wageni wetu wasimame ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuwasalimu. Ah! walikwishatambulishwa jana? Basi nimepewa leo hii.

Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi Prof. Juma Athuman Kapuya ameniomba nitangaze kuwepo kwa mgeni wake aitwaye Hatuna Shamsheli, Diwani wa Kata ya Ushokola Kaliwa Wilaya ya Urambo. Karibu sana Maalim. Habari za Kaliwa? (*Kicheko/Makofi*)

Pia, tunao wageni Hamas Issa Sariko na Imondi Suleiman Imondi, wageni wa Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki - Mbunge wa Viti Maalum, Dodoma.

Karibuni sana na ahsante sana. Matangazo mengine ni kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala leo saa 7:00 mchana katika Ukumbi 219 ghorofa ya pili, jengo la Utawala.

Waheshimiwa Wabunge, kesho asubuhi saa 3:30 kutakuwepo na semina ambayo inahusu mafanikio ya Benki ya NBC katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameomba Wabunge tujitahidi ili tuweze kusikia mafanikio ya Benki hii ambayo na sisi Tanzania ni wana hisa. Hayo ndiyo matangazo sasa kwa shughuli inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hoja ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango Kuhusu hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2007/2008

(*Majadiliano yanaendelea*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa mipango yake mizuri na inayotekelzeza, ambapo Pato la Taifa limekua na pato la wastani la Mtanzania limeongezeka. Ili ukuaji wa pato uweze kwenda kwa kasi zaidi suala la kilimo cha umwagiliaji lipewe kipaumbele, mradi wa uvunaji wa maji ya mvua uandalawe kwani nchi yetu imebarikiwa kuwa na mvua nyingi na rasilimali maji hupotea bure.

Viwanda vidogo vidogo vya usindikaji kwa wananchi navyo vipewe kipaumbele. Serikali kwa makusudi kabisa iiandae Benki mahususi kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wakulima na miradi ya kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali ni vyema isipandishe bei ya mafuta ya taa, kwani wananchi walio wengi mijini na vijijini wenyewe kipato hafifu wanatumia mafuta ya taa na hii itasadia kupunguza uharibifu wa mazingira na nchi yetu kuinusuru na jangwa.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, napenda kukupongeza kwa Bajeti yako nzuri licha ya kuwa na malumbano makubwa ya ushuru wa mafuta. Naanza kwa kusema naomba kuunga hoja mkono ili Bajeti ipite.

Kwa kuwa ongezeko la mafuta ya taa ni shilingi 4/= tu kwa lita, ukilinganisha na kelele zinazotoka kila mahali kwa maoni yangu kama itawezekana uondoe ushuru huo wa mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa zaidi la tofauti ya ushuru kati ya dizeli na mafuta ya taa, nashauri Serikali itafakari na iweke mikakati madhubuti ya namna ya kudhibiti mafuta ya taa yasichanganywe na dizeli vinginevyo makusanyo yatashuka kwa kuagiza mafuta ya taa ambayo yanachanganywa na dizeli. Naomba kuwasilisha.

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na hali ya uchumi wa nchi ni lazima wananchi waelimishwe kuwa na utamaduni wa kuweza kulipa kodi. Hatuwezi kuendelea kama wananchi hawawezi kulipa kodi hizo. Nchi zilizoendelea lazima wamewawezesha wananchi wao, wanalipa kodi kutokana na hali yetu ya nchi ya kuweza kuendelea na ushuru wetu ukue.

Mheshimiwa Spika, *TISCAN* iliyopo haina haja kuendelea na kazi, ushauri ni kuwa kazi hii waachiwe wenyewe *TRA* kwa sababu mkataba wanaopata *TISCAN* ni fedha nyingi, makusanyo wanayopata 1.2% ni kubwa na ni bora fedha hizo wapatiwe mafunzo wafanyakazi wa *TRA*.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa utoaji wa magari na makontena bandarini unafanywa makusudi kucheleweshwa bandarini kwa ajili ya kampuni iliyopewa dhamana, ilifanya makusudi kuchelewesha mizigo ili mfanyakibashara atoe au apate *storage charge* kubwa.

Mheshimiwa Spika, wazalendo wawezeshwe kupata muda kwa mizigo yao wakati wageni wanapewa siku 60 ndio mizigo uwe na *storage charge*. Kwa Mtanzania mizigo wake apewe baada ya siku 7 tu, Wizara husika iliangular hili ili tuwawezeshe Watanzania wapate kuwa na uwezo kufanya biashara nchini kwao. Naunga hoja hii.

**MHE. TEDDY L. KASELLA - BANTU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote natoa salaam za rambirambi kwa ndugu na jamaa wa marehemu wote waliofariki kwa ajili ya basi la *Mohamed Trans* hivi karibuni kule Singida, naomba roho za marehemu wote wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa amani, *Amin*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza *Taifa Stars* kwa ushindi waliotuletea Tanzania kama Taifa, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, naona nitakuwa si mwangi wa fadhila nisipompongeza mwanamke mwenzangu Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Fedha kwa uhodari, ujasiri na umakini wake kwa kusoma Bajeti hii nzuri kwa muda wa saa 1.30 mfululizo bila kutetereka wala kukwama au kunywa maji. Kweli ana *stamina* na anastahili sifa na pongezi ya hali ya juu. Hongera sana, naam amedhihirisha sisi wanawake tunawaeza *I am proud of her*.

Mheshimiwa Spika, bila kusahau naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, wananchi yaani wapigakura wangu wameniomba nifikishe kilio chao kwamba wanaomba sana Serikali iondoe au isipandishe bei ya mafuta hasa mafuta ya taa, hasa ukizingatia sisi Bukene, hatuna umeme hivyo tunahitaji mafuta ya taa hasa kwa mwananchi wa kawaida kwa vibatari au chemli yaani taa na watoto wanosomea taa hizi zinazotumia mafuta ya taa naomba sana bei ya mafuta ya taa chonde chonde ibaki pale pale.

Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana na maneno na mawazo ya Mheshimiwa Wilson Masilingi, kwa kuomba Serikali iangular nini hasa kinachopandisha bei ya mafuta ya petroli, dizeli. Serikali ione ni shilingi ngapi yanakotoka hadi kufika Dar es Salaam Bandarini na baadaye iongeze kodi zake.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini ikifuatiliwa vizuri bei ya mafuta haya haiwezi kufikia shilingi 1,600/= tu kwa lita Bukene, sijui itakuwa shilingi ngapi yawezekana ikawa shilingi 2,000/= kwa lita ili kuwapunguzia mizigo huu, naomba Serikali isijitoe

kabisa kwenye shughuli hizi kwa manufaa ya Taifa. Mimi naamini kabisa ikitazama ipasavyo itapunguza mzigo huu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mengine nitachangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Naomba kuwasilisha.

**MHE. OMAR SHEHA MUSSA:** Mheshimiwa Spika, na mimi sina budi kupata nafasi hii ya kuchangia Bajeti ya Serikali kwa maandishi kwa ajili ya kujadili Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, nataka nichangie jambo moja tu la kuondoa kero kubwa ya Muungano iliyodumu sasa kwa kipindi kirefu sana ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kero hii kubwa si nyingine bali ni ile ya mchango na mgawanyo wa Mapato na Matumizi ya Muungano kama ilivyoainishwa kwenye Sura ya Saba Ibara ya 133 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Toleo la mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, Ibara hiyo ya Katiba niliyoitaja hapo juu kinaleza kazi kuu ya Tume ya Fedha ya Pamoja (*Joint Finance Commission*) kufungua *account* ya pamoja ya fedha ili kuweka fedha zote zitakazochangwa na Serikali zetu mbili kwa kugharamia shughuli zote za Muungano baada ya kugawanywa.

Mheshimiwa Spika, sheria namba 15 ya mwaka 1984, Kifungu cha 42 kimeainisha kuundwa kwa Tume hiyo ili ifanye kazi zilizotajwa kwenye Ibara ya 134 (2)(a) hadi (c).

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyopo ni kwamba Tume hiyo kwanza imechelewa sana kuundwa na ilichukua miaka kumi na mbili tangu mwaka 1984 hadi 1996 kuundwa kwa Tume hiyo. Isitoshe baada ya kuchelewa huko, imechukua miaka mingine ni nane tangu mwaka 1996 hadi 2003 ndio Tume hiyo imeanza kazi zake zilizotajwa ndani ya Katiba na bado SMT haijakamilisha kuweka *formula* ya kudumu ya kugawa Mapato na Matumizi ya shughuli za Muungano hadi sasa (Juni, 2007) baina ya SMT na SMZ.

Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji huo sio wa kawaida kwani ulisababishwa na Wizara ya Fedha ya SMT tangu Katiba ya mwaka 1984 ilipobadilishwa na kutungwa sheria hiyo mwaka huo na bahati mbaya Mawaziri wote wa Fedha waliokaa ofisi za Waziri wa Fedha wameachwa bila kuchukuliwa hatua zozote kwa kutotekeleza Ibara ya 133 ya Katiba ya nchi yetu ambapo hadi leo, bado Wabunge tunaelezwa kuwa mazungumzo ya suala hilo yanaendelea na haijulikani lini yamatilizika ili Bunge hili la Tanzania liarifiwe ugawaji wa Mapato na Matumizi ya Muungano wetu tangu tulipoungana.

Mheshimiwa Spika, hali hii ni ya aibu sana kwa Taifa la Tanzania na ni vyema mwaka huu Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi wakalimaliza suala hili kabla ya kwisha mwaka wa fedha wa 2007/2008. Hivyo vikao vyao vya kuondoa kero

viongezwe ili kuyafanya maamuzi ya mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha (*JFC*) ya kugawana Mapato na Matumizi ya Muungano wetu pamoja na kufungua *account* hiyo ya pamoja kama ilivyoelekzwa kwenye Ibara ya 133 ya Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Waziri wa Fedha wa hivi sasa Mheshimiwa Zakia Meghji asimamie suala hili kwa kuleta waraka Bungeni kabla ya Juni, 2008 ili kumaliza kero hili kubwa la Muungano kwani yakifanyika hayo faida zifuatazo zitapatikana.:-

- (a) Pande zote mbili hazitalalamika mbele ya wananchi wao juu ya nani anafaidika au kupunjika na Muungano wetu wa Tanzania.
- (b) Maadui wa Muungano wetu watakosa la kusema juu ya kasoro hii ya muda mrefu.
- (c) Tanzania Bara na Zanzibar kila upande utapata kinachostahili na kuchangia kinachostahiki vile vile.
- (d) Zanzibar kama ni sehemu ndogo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itawenza kuchangia għarama zake za Muungano kutokana na mapato ya Muungano wenyewe.
- (e) Zanzibar, itafaidika zaidi kwa mgao wake wa mapato, hata kwa fomula yoyote ile itakayokbalika baina ya SMT na SMZ.
- (f) Hisa za taasisi zote za pamoja kama vile Benki Kuu ya Tanzania na kadhalika, zitawenza kujulikana wazi kwa asilimia ya mchango wa kila nchi kutokana na *formula* hiyo ya kudumu itakayowekwa.
- (g) Muungano wetu utakuwa imara zaidi kuliko ulivyo sasa kwa kutuwezesha kila upande kupata haki yake na kulipia għarama zake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba mchango wangu huu uingizwe kwenye *Hansard* za mchango ya Wabunge kwa mwaka 2007/2008 kwa mada hii nyeti ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, nimeamua kuchangia mada hii kwa maandishi ili kuepu ka jazba isiyo na maana na hii ni (*constructive criticism*) yenye lengo la kusaidia pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na kukubali mapendekezo ya Bajeti ya mwaka 2007/2008, ahsante sana.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Zakia Meghji na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa pamoja na Manaibu wahusika wote.

Bajeti hii ni Bajeti mpya kwa kuwa tu imegusa mafuta ambayo karibu kila shughuli ya kiuchumi inaendeshwa na nishati hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kwa upande mwingine ni fursa nzuri ya jamii kuchangia ghamama za maendeleo lakini sambamba na matumaini tunayotoa leo kwa wananchi ni vema yakatekelezwa, langu kuu ni moja.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nitasema kweli daima fitina kwangu ni mwiko. Naomba niseme nionavyo mimi, ni wajibu wangu kushauri. Tunawapongeza *TRA*, naungana nanyi kutoa kipaumbele kwa wafanyabiashara wakubwa wanaotulipia kodi wapewe *classic services* ndio uungwana, wapewe geti maalumu, wapewe huduma ya haraka (*fast track*), lakini siridhiki na neno kupitisha mizigo bila ukaguzi kwa asilimia fulani. Hayo ni majaribu na hatari.

Mheshimiwa Spika, kampuni ina watendaji wazuri na wabadhirifu, yawezekana kinyume na wenyе kampuni mara nyingine hao ndio wanaotuvuruga. Hata *VIP Lounge* bado kuna mashine za ukaguzi. Mnaonaje tukienda awamu kwa awamu? Nadhani hii haitaathiri Bajeti yetu.

Mwisho, maneno ya wenzetu wa Kambi ya Upinzani ukweli wana uhuru wa kutoa mawazo yao ili kuongeza ufanisi kwa Watanzania kama hizo *formula* walikuwa nazo nao ni Wabunge kwa nini wasiziseme kabla na badala yake wanalaumu? Hii ni tabia ya *ineffective leaders*. Naunga mkono hoja zote.

**MHE. USSI AMME PANDU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka kuchukua nafasi hii kuzipongeza Wizara zote mbili ya Mipango, Uchumi na Uwezesaji na ile ya Wizara ya Fedha kwa kuwasilisha Bajeti zao kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na kwa sababu Bajeti hii inatekeleza ile sera ya Chama Tawala, Chama cha Mapinduzi ni dhahiri kwamba maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha, ukurusa wa 23 wa kitabu hicho unazungumzia Tume ya Pamoja ya Fedha ambayo mazungumzo bado yanaendelea lakini kiwango cha fedha cha 4.5% ambacho SMZ inapata kwa kweli ni kidogo na kimeshapitwa na wakati, kiwango hicho mwanzo kilipotolewa makubaliano ya kiwango hicho ni cha muda tu na sasa huu ni mwaka wa 13 toka mwaka 1994 yalipofanyika makubaliano hayo.

Hivyo ili kuendelea kudumisha Muungano wetu naomba Tume hii ya Pamoja iweze kukamilisha mazungumzo hayo na SMZ iweze kufanya maendeleo ikiwa kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushuru wa bidhaa, vile vile ukurasa wa 81 wa kitabu hiki unazungumzia ushuru wa bidhaa. Nataka kuchukua nafasi hii pia kuipongeza Serikali kwa makusudi kuweza kuwasaidia ndugu zao wa Zanzibar kwa sheria ya ushuru wa bidhaa wa kuirejeshea Serikali ya Mapinduzi Zanzibar makusanyo ya ushuru wa

bidhaa zinazozalishwa Bara na kuuzwa Zanzibar. Kwa kufanya hivyo Serikali itakuwa imesaidia sana katika kuongeza mapato ya SMZ.

Mheshimiwa Spika, mwisho naipongeza Serikali kwa Bajeti hii kuimarisha miundombinu muhimu ya Kitaifa, kuimarisha sekta ya kilimo ikiwemo mipango ya maendeleo ya kilimo ya Wilaya na miradi ya umwagiliaji maji, pamoja na kuimarisha sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, tukiweza kukamilisha mambo hayo ni kuimarisha sekta ya elimu ni wazi kwamba maisha bora kwa kila Mtanzania yatapatikana.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kukushukuru na naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote ahsante.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza Mawaziri, Mheshimiwa Zakia Meghji na Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa pamoja na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu na Mheshimiwa Gaudence Kayombo, kwa kazi kubwa waliyofanya katika maandalizi na uwasilishaji wa hotuba za Hali ya Uchumi na Bajeti kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali kuboresha maisha ya Watanzania kupitia Bajeti, nashauri mambo kadhaa yafuatayo ya uboreshaji kwenye Bajeti. Serikali ipanue wigo wa kodi kwa kuangalia maeneo yafuatayo:-

(a) Pato toka sekta ya madini; uwekezaji unaofanywa katika sekta hii hauogezi mapato, tuwashirikishe wazawa kwa kutekeleza Ibara ya 39(g) ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Pia tupunguze misamaha ya kodi kwa wawekezaji hawa.

(b) Pato toka sekta ya sanaa haitozwi kodi, sekta hii inayokua kwa kasi inaingiza mabilioni ya fedha lakini haitozwi kodi. Niko tayari kushirikiana na Serikali kujadili zaidi juu ya eneo hili.

(c) Watanzania wengi wanaofanya biashara ndogo bila elimu ya biashara hawatambuliwi na mfumo wa kodi. Kwa kuwa sekta hii sasa imekua kwa kasi, yaani wamachinga ni wengi sana lakini hawatambuliki, . Serikali iharakishe MKURABITA na pia iwasaidie kimafunzo kisha *TRA* ishiriki katika kuwabadilisha kuwa wafanyabiashara wanaotambulika na kulipa kodi. *TRA* iandae *special tax regime* kwa ajili yao, nikoo tayari kushirikiana na *TRA* katika kufanikisha hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihusishe mfumo wa kodi nchini, mfumo wa sasa unamuumiza sana mwananchi wa kipato cha chini. Kwa mfumo wa sasa mfanyakazi analipa kodi *on the basis of gross income* wakati mfanyakazi anatozwa kodi *on the basis of taxable profit (net profit after operating expenses)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali idhibiti misamaha ya kodi hasa kwa wafanyabiashara wawekezaji kwenye madini.

Mheshimiwa Spika, baada ya mapendekezo hayo basi nimalize kwa kuiunga mkono hoja hii.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, tayari nimeunga mkono Bajeti ya Mipango ya mwaka huu wa fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo yafuatayo ambayo ingefaa Serikali iyashughulikie kwa makini sana. Kwanza, suala la ombi la Wabunge kuhusu uwezekano wa kuondoa ongezeko la bei katika mafuta ya taa. Lakini nashauri ongezeko la mafuta (petroli) libaki kama liliyyo. Maelezo ya kina yawepo.

Pili, suala la kutafakari ada ya liseni ya magari kulingana na ukubwa wa injini za magari kwa kuzigawa toka *cc 0 – 500*. (*ii*) *cc 500 – 1000* (*iii*) *cc 1000 – 2000* (*iv*) *2000 – 3500* (*v*) *cc 3500 – 4800*. Bado tozo za magari makubwa zibaki zilivyo. Maelezo ya ziada yatolewe ili wananchi waelewe umuhimu wa kila mtu kuchangia mfuko wa barabara kwa madhumuni ya kujenga barabara zetu na vivuko vyake vyote muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwa sera ya idadi ya watu ambayo ni sera mama kwa sera nyingine zote, nashauri kuwa katika kipindi hiki cha Bajeti, tumwombe Waziri mhusika aandae semina kwa Wabunge wote kuhusu sera hii. Lakini hata kama Wizara itaona gharama kwa Wabunge wote, basi angalau kwa Wabunge wanachama wa *Tanzania Parliament Association Development (TPAPD)*. Hili lipewe *priority*, unaona wajumbe wakielewa, watazitangaza vizuri sera hizi vijijini na mijini kwa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, bado nitaendelea kuipongeza *TRA* kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa nchi yetu. Naelewa pia kwa kuwapa nguvu za kisheria kufanya kazi yao vizuri, wataendelea kuchapa kazi kwa kufuatialia wale wakwepaji kodi, mafunzo ya walipa kodi yaendelee kupewa kipaumbele. Naelewa Mikoa mingine yenye wafanyabiashara wachache wanapopangiwa viwango vikubwa, vinawafanya baadhi ya wafanyabiashara kuhama na kukimbilia Dar es Salaam mafichoni.

Mheshimiwa Spika, MKURABITA sasa uanze kutekelezwa kwa vitendo na Serikali ianze maandalizi kwa kuwafundisha watalaamu wa jinsi ya kurasimisha mali na hasa nyumba zao na ardhi yao. Hii ndiyo changamoto yetu ya kuanza kuwapa uwezo wananchi vijijini na hata mijini kwa kuwawezesha kuwa wajasiriamali. Tuanze na wao wenyewe ili tuwapunguzie umaskini. Sijui kwa nini hatujatumia uzoefu wa wenzetu wa *Grameen Bank* na ushauri wa mtaalamu kutoka Peru juu ya MKURABITA.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji akubali kuanzishwa kwa Tume ya Mipango au Baraza la ushauri kuhusu mipango yetu. Baraza hili lijumuise viongozi na watalaamu mbalimbali wenye uzoefu wa Mipango na Ustawi wa Jamii nchini. Viongozi wa *NGOs*, madhehebu ya dini, wanasiasa, watalaamu wa fani mbalimbali na makundi maalumu ya wananchi wetu wakiwemo walemavu.

Mheshimiwa Spika, nashauri suala la kuanzisha vyanzo vyetu wenyewe kwa ajili ya barabara zetu lifafanuliwe vizuri sana. Hili ni muhimu kwa sababu lawama nyingi

zitaendelea kutolewa kwa Wizara hiyo ya miundombinu. Tutumie nafasi hii kuanza kufafanua malalamiko ya Wabunge juu ya suala hili ili hoja za Wizara husika isije ikaachiwa mzigo wa kujibu, miundombinu ndiyo itasumbua kwenye mipango yote hii, ningeshauri Bajeti ijayo itoe kipaumbele namba moja mwakani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MARGARET A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa hotuba nzuri zilizotanabaisha umma Mipango, Mapato na Matumizi ya fedha za nchi kwa mwaka 2007/2008. Pamoja na Bajeti kufafanuliwa kwa lugha inayoeleweka na nyepesi kueleweka na wananchi walio wengi, nimeguswa kuchangia katika maeneo machache ya hotuba hasa ya Waziri wa Fedha kuhusu Bajeti.

Nimefurahishwa na Serikali kuweza kupanga vipaumbele vitakavyoshughulikiwa mwaka 2007/2008 kwa makini zaidi hasa ikizingatiwa kuwa Tanzania kama nchi inayoendelea na kuwa bado katika hali ya uchumi duni, hatuwezi kuendelea kwa kutawanya rasilimali zetu kwa kila sekta na kuweza kupata matokeo (*impact*) kwa haraka na thabit. Hivyo naamini tukiendelea kwa mtindo huu wa kupanga vipaumbele kwa makini tutapata maendeleo ya haraka. Si hivyo tu, napongeza pia kwa Bajeti hii kuweza kuzingatia kikamilifu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ambayo wananchi watahukumu utendaji wa Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuanza kuboresha maslahi ya watumishi wa umma kwa kupunguza asilimia ya kiwango cha kukatwa kwenye mishahara yao ikiwa ni kodi ya mapato. Lakini tahadhari ni kwamba ahueni hiyo isije ikamezw na mfumuko wa bei na mahitaji mbalimbali la sivyo haitakuwa jambo la faida kwao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema machache na kutoa maoni juu ya ya maeneo yaliyonipa faraja, nitazungumzia maeneo mengine ambayo nadhani yanahitaji kuangalia kama si katika Bajeti hii basi katika siku zijazo. Katika ukurasa wa 42 upelekaji wa madaraka kwa wananchi yaani *D by D*, nakubaliana kabisa na mfumo lakini Serikali itatumia mikakati gani kati ya sasa na wakati ambapo nchi itakuwa na wahasibu na wakagazi wa fedha wa kutosha katika Halmashauri zetu ili kudhibiti rasilimali nyingi ambazo zitaelekezwa huko kwenye miradi ya maendeleo mbalimbali au kwa mwaka huu Serikali imeandaa watalamu wa fani ya uhasibu wangapi ambao watakwendwa kupokea majukumu haya kwa matarajio ya kupata tija?

Katika ukurasa wa 55, kuhusu leseni za magari kutozwa kutohana na ujazo wa injini hasa sehemu (ii) ada naona imezidi kuwa kubwa hasa ikizingatiwa kuwa hayo yatagusa magari madogo (*saloon cars*) na pikipiki vinavyotumika kama sehemu ya ajira kwa wengi mijini na vijijini, nyenzo za kufikishia wafanyakazi maofisini hasa mijini, *pick ups* kwa kubeba watu na mazao hasa vijijini na kadhalika, kwa msingi huo wahusika watakwepa kodi kwa kuacha kujajiri, hivyo wananchi vijijini kuendelea

kuhangaika na suala la usafiri na usafirishaji mazao hasa katika maeneo ambayo barabara ni mbovu sana, milimani na kadhalika.

Naiomba Serikali ione uwezekano wa kupunguza kiwango hiki na kuongeza kwenye maeneo ya vitalu vya uwindaji, uuzaji wa magogo ambapo naamini ukwepaji wa kodi hautakuwepo endapo udhibiti utaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, zaidi naishauri Serikali kupunguza bei ya mafuta ya taa ambayo ndiyo nishati muhimu kwa wananchi walio wengi ambao hawana umeme wa maji, wa mafuta wala wa juu. Kwa msingi huu uhifadhi wa mazingira utawezekana kwa sababu ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa unaweza kupungua ikizingatiwa kuwa kuna kampeni ya kutumia nishati mbadala inayoendelea nchini.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 59, nakubaliana na jitihada za Serikali za kujaribu kupunguza ucheleweshwaji wa kutoa mizigo katika bandari ya Dar es Salaam. Lakini nashauri ifuatavyo:-

(a) Uwekwe mkakati wa kupunguza taasisi nyingi zilizopo zinazosimamia uingizaji wa bidhaa. Wingi wa taasisi hizo unaongeza urasimu na uwezekano wa rushwa endapo mtu unataka mizigo yako iondoke haraka bandarini.

(b) Paongezwe milango ya kuitishia mizigo kwa kuongeza teknolojia ya kukagua mizigo yote bandarini na kuondoka haraka. Vinginevyo haina maana kuwa na taasisi nyingi zisizofanya kazi kwa ufanisi. Cha msingi ni kuwa na nyenzo na vifaa vya kisasa katika bandari ya Dar es Salaam vitakavyowezesha kukabiliana na ushindani wa kiutendaji katika bandari za Mombasa, Durban na kadhalika. Tukijizatiti kiteknolojia nchi itaweza kuingiza mapato ya kutosha kutokana na nchi za Maziwa Makuu kuitishia mizigo Tanzania.

Naomba kutahadharisha utaratibu wa kuitisha mizigo bila ukaguzi (*fast tracking*) ni hatari kwa nchi kwa sababu binadamu hasa mfanyakishara ana hulka ya udanganyifu kwa minajili ya kupata faida kubwa. Sasa kiasi, aina ya mizigo kitathibitishwaje? Huu ni mwanya mkubwa wa kusababisha nchi iwe ni njia ya kuitishia bidhaa hatari na haramu. Naiomba Serikali imalizie ujenzi wa barabara ya Kibiti-Lindi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maoni haya, naunga mkono Bajeti hii na kutoa angalizo juu ya umuhimu wa kudhibibiti matumizi ya rasilimali fedha kwa maendeleo yaliyokusudiwa.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri wake wote wawili pamoja na watendaji wao wote kwa kuwasilisha Bajeti hii mbele yetu kwa ufasaha na kuleta matumaini katika maeneleo na ufanisi wa shughuli za kawaida za kibinadamu.

Mheshimiwa Spika, hakuna Taifa hata moja ambalo halitegemei kodi katika nchi yake, lakini pia ni lazima kuangalia kodi hiyo inapandishwa kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutaka kujikwamua ni vizuri kuangalia athari ambayo inaweza kupandisha gharama ya ukaguzi wa vyombo vyta moto chombo chenye cc mpaka 1500 kitatozwa shilingi 80,000/= badala ya shilingi 20,000/=. Huu ni mfano wa kwanza tu.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri kuwa kupanda kwa gharama hizo kwa ghafla na kwa kiasi kikubwa kama hicho ni hatari sana hasa ukizingatia uwezo wenyewe wa vyombo hivyo, ni vyema kuondoka katika shilingi 20,000/= basi twende angalau kwenye shilingi 50,000/= lakini pia tutoze kodi hiyo kutokana na uwezo wa tani wa chombo husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upandaji wa mafuta ningeshauri ubakie hapo hapo isipokuwa mafuta ya taa ningeshauri yapungue ili wananchi wetu waweze kuwa watumizi wazuri na kuachana na uchafuzi wa mazingira kwa kukata miti ovyo.

Mheshimiwa Spika, kuna kero nyingi zinazohusu masuala ya Muungano, napenda nimpongeze Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa kutoa wazo la kuunda Kamati ya viongozi ambao watendaji wakuu wa Serikali hizi mbili kwa kukutana kila miezi mitatu ili kuzungumzia kero zote za Muungano.

Mheshimiwa Spika, suala la mgao wa 4.5% kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar sasa umepitwa na wakati, kama kweli tunataka Zanzibar ijikomboe kimaendeleo na kuweza kujiendesha katika shughuli zake za kawaida, nawaombea kila la kheri viongozi hao wafanikiwe katika kutatua kero hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wafanyabiashara wakubwa kupewa kipaumbele kwa TRA katika kuingiza mizigo yao bandarini na wakaitoa bila ya kuangaliwa kwa kigezo kuwa ni waaminifu na ni walipakodi wazuri, sishauri kuwaachia kiasi hicho kwani hakuna mfanyabiashara hata mmoja asiyetaka faida ya haraka katika biashara zake, kwa hiyo wanaweza kutumia mwanya huo kwa kujinufaisha haraka na kuwaacha wafanyabiashara wadogo kubakia hapo hapo bila kupata mabadiliko yoyote katika biashara zao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ushauri na kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu suala la magari yanayotoka Zanzibar bado ni usumbu na zinaonekana kama ni gari zinazotoka nchi za nje hilo ni kosa kubwa kwani gari ya Zanzibar ni gari iliyomo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Waziri Kivuli

wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji Mheshimiwa Kabwe Zitto, kwa maoni mazuri yenye kuleta dira halisi ya kumkomboa Mtanzania katika umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Spika, kupanda kwa mafuta ya taa kutaathiri Watanzania walio wengi maskini ambao wengi wao wanaishi vijijini, wanategemea mafuta kwa matumizi mbalimbali. Wanafunzi wa shule za sekondari vijijini wanatumia mafuta ya taa, hivyo kwa jinsi ya umuhimu wa hali ya maisha ya Watanzania wengi ambao ni maskini ninashauri, Serikali kupunguza bei ya mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, suala ya kuchanganya petroli na mafuta ya taa limekuwa likilalamikiwa na madereva mbalimbali wakionyesha huruma ya injini zao za gari kuingia dosari na hasa *injector pump*.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kutumia mbinu za ziada kuwakabili wahalifu hao wanaodidimiza maendeleo katika kupambana na umaskini. Bajeti hii pia imegusia UKIMWI, ambapo janga hili linaendelea kuua maelfu na kutesa vijana na watoto. Naishauri Serikali kuwalinda wataalamu wa Wizara mbalimbali wasiathirike na UKIMWI kwa kuwaruhusu na kuwawezesha kuondokana na wanandoa wao pale wanapopata fursa ya kufanya kazi nje ya Wilaya zao kuanzia siku tano na zaidi.

Mheshimiwa Spika, semina na makongomano yametosha, fedha za wahisani zipelekwe kwa walengwa vijijini. Kuhusu ajali za baharini ni vyema vikatafutiwa mbinu za kukabili tatizo la vifo kwa kuwawezesha kupatiwa makoti ya kuokolea maisha. Hata majahazi ya mizigo, boti ndogo ndogo ni vyema wakapatiwa makoti ya kuokolea maisha angalau tupunguze vifo vinavyotokana na bahari.

Suala la upungufu wa maji safi na salama vijijini linaonekana mbali na jitihada zinazofanywa, nashauri Serikali kuangalia kwa makini sana upungufu wa maji Kondo Kaskazini. Kata nyingi bado hazijapata huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo barabara ya Mkoa kwenda Kondo bado haijakidhi kiwango ni vyema ikawekwa lami ili kurahisisha wakulima wa alizeti, maharage na mazao mengine kuweza kufika Dodoma Mjini kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, fedha za msamaha wa madeni toka nchi wanachama wa *Paris Club* zitumike ipasavyo, ili ione kane msamaha huu umewasa idia eneo fulani la nchi kupata maendeleo. Vitambulisho vya Taifa ni jambo zuri sana lakini naishauri Serikali kufanya uhakiki wa wageni haramu waliopo mpakani ili uraia huu usije ukaenda kwa wasiohusika. Ahsante. Naomba kuwasilisha.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni juu ya hotuba hizi mbili za Bajeti kutoka Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

Kwanza kabisa naishauri Serikali ifute kodi zote za mafuta kwani mafuta ndio mahitaji yanayochangia katika uzalishaji, ni nishati itumikayo katika usafirishaji. Kwa

mantiki hiyo mlipuko wa bei unaendelea kwa kasi kwani bei ya mafuta ina athari kubwa katika maisha ya kila siku.

Kuhusu mafuta ya taa, Waziri atakubaliana nami kuwa asilimia 90 ya wananchi maskini wanaishi vijijini na mafuta ya taa ndio pekee yanayowasaidia kupata mwanga kwani vibatari ndio taa yao. Kwa upande wa wale waishio mijini mafuta ya taa husaidia katika kupika kwa kuwa mkaa umepanda bei mno, gunia sasa ni shilingi 18,000 mpaka 25,000. Kwa Mtanzania wa kawaida kiasi hicho ni kikubwa na tukipunguza kodi ya mafuta ya taa matumizi ya mkaa yatapungua hivyo mazingira yataendelea kuwa bora kwani miti haitaendelea kukatwa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina vyanzo vingi sana vya mapato, tukianzia kwenye rasilimali tulizonazo, mfano maliasili, madini, maziwa, hifadhi za wanyama, vyote ni vyanzo vizuri kama vitatumiwa vizuri na kama mipango itakuwa mizuri na endelevu.

Nchi yetu imekithiri kwa rushwa na ubadhirifu wa fedha za umma. Mimi nina maswali machache kwani nahitaji Serikali itueleze juu ya ukiukwaji na utaratibu wa kumpata mzabuni wa kuchunguza mauzo ya dhahabu unaofanywa na kampuni ya *Alex Stuart Asseyers*. Ni kiasi gani kimepatikana kutokana na taarifa ya *Alex Stuart Asseyers* baada ya Serikali kulipa shillingi bilioni 85 au *USD 65,00.000?* Pesa hizo zingeweza kusomesha zaidi ya Watanzania vyuo vikuu zaidi ya watu 20,000.

Suala la pili, naomba ufanuzi juu ya udhamini wa dola 100 milioni kutoka *BoT* kwa kampuni ya *Meremeta Gold Mine Company* ambayo ilikuwa chini ya uongozi wa *Time Mining* ya *South Africa* baada ya kuichukua kutoka kwa *JWTZ*. *BoT* imetoa taarifa gani ya kina juu ya tathmini ya mradi huo?

Mheshimiwa Spika, hayo ni mambo machache, lakini hata taarifa ya *CAG* inaonyesha upotevu au ubadhirifu mkubwa wa pesa, natarajia kusikia wahusika wanachukuliwa hatua kwani pesa zilizopotea karibu trilioni 1.2 katika Halmashauri zetu. Pesa hizo nyingi sana zingeweza kuingizwa katika mipango yetu ya maendeleo kwani nchi ina mahitaji mengi. Shule zimejengwa hazina mabweni, maabara za sayansi na wala walimu hawatoshi, maktaba hakuna wala nyumba za walimu. Hayo ni mambo ya kuzingatia.

Mheshimiwa Spika, tujiulize juu ya Bajeti hii itainua maisha ya Mtanzania? Vile vile mipango ni endelevu au itaendelea kuwa duni na mlo mmoja kwa siku utaendelea kuwa shida?

Mheshimiwa Spika, mengi yamejadiliwa sioni haja ya kurudia nasisitiza matumizi mazuri ya rasilimali pesa iliyopo na ubunifu uongezeka kwa kutafuta vyanzo vingine.

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu ya kuniwezesha kuchangia Bajeti hii iliyopo mbele yetu. Pia niwashukuru kina mama wa CCM, Mkoa wa Kusini Pemba kwa kuniwezesha kuingia katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kuchangia Bajeti hii kwa kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa kuwasilisha Bajeti vizuri kabisa bila ya kuwasahau watendaji wao waliowasaidia kutayarisha Bajeti hii. Mimi naipongeza Bajeti na kuiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Bajeti hii kwa kuipa kipaumbele elimu kwani elimu ndio ufunguo wa maisha na ndio kiini cha maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa kuendeleza elimu, naiomba Serikali iangalie nyanja zote yaani nyumba za walimu, maslahi ya walimu ili kuwapa moyo walimu wetu pia kuondoa tabia ya kuhama kwa walimu katika maeneo waliyopangiwa.

Mheshimiwa Spika, pia niungane na Wabunge wenzangu waliochangia kuhusu ukaguzi wa mizigo bandarini. Mizigo yote ambayo inapita katika bandari zetu ni lazima ikaguliwe kwa sababu wafanyabiashara wengine si waaminifu na wanatafuta njia kama hizo ili walete vitu vya ajabu ajabu ambavyo wataiangamiza nchi na wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, dawa za kulevyia zinaingia nchini kwa kupitia wafanyabiashara wakubwa wasio waaminifu, nazo zinapita humo humo kwenye vyombo vyetu; sasa tukiruhusu mizigo isikaguliwe, watu hawa wataiangamiza nchi, hawa ni watu hatari sana! Tusiwaamini.

Mheshimiwa Spika, Bajeti yetu imepandisha bei ya mafuta ya aina zote. Hilo sina pingamizi nalo kwa sababu naamini hakuna Serikali ambayo inawataka wananchi wake wapate shida na hasa Serikali yetu ya Awamu ya Nne inayoongozwa na CCM inawapenda wananchi wake. Hata Ilani yetu inaeleza hivyo lakini naiomba Serikali yetu tukufu kuangalia uwezekano wa kupunguza ongezeko katika mafuta ya taa. Mafuta ya taa ni nishati ambayo inatumika na wananchi wengi wa kipato cha chini kabisa kwa hiyo, naomba ongezeko hilo liondoshwe na litafutiwe mbadala ili Bajeti yetu isiathirike.

Mheshimiwa Spika, mafuta ya taa yanatumika katika vijiji na miji ambapo umeme haujafika na ukizingatia umeme tulionao na ni 10% ndio umesambazwa katika nchi yetu. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa jimbo la Njombe Magharibi, wanapongeza sana Bajeti hii nzuri iliyo mbele yetu na kwa niaba yao nawasilisha pongezi hizo.

Aidha, tunampongeza sana Waziri wetu wa Fedha, Mheshimiwa Mama Zakia Meghji kwa Bajeti nzuri pamoja na timu yake ya Mawaziri wadogo pamoja na watendaji wake, hongera sana. Kwa vile Bajeti inalenga miundombinu: Barabara, elimu na afya, kilio cha wananchi wangu ni barabara kutoka Njombe kwenda Wilaya Makete kupitia Igosi/Kipengere. Kule vijijini wanaomba kodi ya mafuta ya taa. Ipunguzwe siyo kufutwa, ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii ni nzuri sana kwani mategemeo makubwa ya barabara za vijini na kata zitafufuliwa. Mfano mkubwa kwenye kata ya Saja katika Wilaya ya Njombe, barabara hazipitiki kabisa na kwa muda mrefu barabara zile zimesahaulika na Halmashauri ya Njombe. Pamoja na juhudzi nyingi za kuzielezea bado hakuna kilichofanyika na kuna Shule ya Sekondari ya Saja, walimu na wanafunzi wanateseka sana kwa usafiri. Pia kuna Zahanati ya Saja, tatizo ni barabara, watumishi wanakwepa kwenda huko kwa sababu ya tatizo la barabara. Kwa vile mengi wamechangia wenzangu naomba Serikali iliangular Jimbo la Njombe Magharibi yaani Tarafa ya Wanging'ombe, Mdandu na Imalinyi kwani tuko pembezoni mwa Wilaya na Mkoa wa Iringa. Napongeza Serikali kwa kujenga barabara ya Illembula-Usuka, Njombe, Soliwanya-Lyambuki-Njombe.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia suala la ukaguzi wa mizigo bandarini. Mpango huu wa kupitisha makontena kwa kigezo cha aina ya wafanyabiashara hautaleta ufanisi wowote, bali utaleta matatizo makubwa na hatutawatendea haki Watanzania. Pia, ni kukaribisha mianya ya rushwa ambayo tumekuwa tukiipigia kelele muda mrefu humu Bungeni na lingine ni kuwa makontena hayo yanaweza kuingizwa na vitu vingine kama vile dawa za kulevyia jambo ambalo litaendelea kuiathiri jamii ya Tanzania. Je, tunatoka wapi tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, kupandisha bei ya mafuta si kumsaidia mwananchi wa kipato cha chini bali ni kumkomoa na hilo lengo la maisha bora kwa kila Mtanzania hatutalifikia. Tukiongeza bei ya mafuta tumeongeza bei ya vitu vyote. Mfano, hatujamsaidia mkubwa ambaye anataka asafirishe bidhaa zake na kwa hiyo, hatujamsaidia mtu wa kawaida ambaye ni mlaji kutokana na gharama za usafirishaji.

Pili, hatujamsaidia mwanamke ambaye anahitaji kwenda kliniki ama akiwa mjamzito ama kumpeleka mtoto wake kutokana na nauli kupanda. Pia tumemuongezea mizigo hata mwanafunzi ambaye anahitaji nauli ya daladala ili afike shulenii, je, tumsaidiae mwananchi?

Mheshimiwa Spika, kupanda kwa bei ya mafuta ya taa kutachangia zaidi uharibifu wa mazingira kwani badala ya kutumia mafuta ya taa kwa kupikia ama kuwashaa taa, watu wetu wataendelea na mtindo wa kutumia kuni, kwa hiyo, misitu itaendelea kutoweka na ukame utashamiri zaidi kwa maana hiyo.

Hivyo naishauri Serikali itumie vyanzo vingine mbadala vy a mapato ili tuweze kupata fedha za kukidhi mahitaji yetu kwa nia ile ile ya kumkomboa Mtanzania aondokane na umaskini.

Mheshimiwa Spika, kuongeza bei ya dizeli ama petroli ni kumpunguzia Mtanzania uhuru wa mawasiliano na mawasiliano ni njia mojawapo ya kujikwamua na umaskini. Gharama za usafiri zikipanda haitakuwa rahisi mtu wa kipato cha chini au wa kijijini kuweza kufika eneo lingine ama kufanya biashara ndogo ndogo ama kuwasiliana na wengine.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali imfikirie zaidi Mtanzaznia ambaye ndiye aliyetuleta hapa Bungeni ili tumwakilishe na siyo tumuangamize. Tuachenii siasa, tupo hapa kwa ajli ya watu, hivyo basi tutumie vyanzo mbadala vilivyoainishwa na wasemaji wengi kutoka Kambi ya Upinzani ili tupate maisha bora kwa kila Mtanzania. Ahsante nakushukuru.

**MHE. OMAR YUSSUF MZEE:** Mheshimiwa Spika, malori na mabasi yanafanya faida kubwa ulikinganisha na yale ambayo ni zaidi ya *cc 1,500* na chini ya *cc 5000* ambayo yenewe hawayatumii kwa biashara kama ilivyo kwa mabasi na malori. Biashara inayofanywa kwa mabasi na malori ina faida ya zaidi ya shilingi *3,500,000/-* kwa mwezi. Naishauri Serikali gari zote zaidi ya *cc 1500* zitoze shilingi *250,000/=* kwa mwaka. Hii ni pamoja na mabasi na malori.

Mheshimiwa Spika, Serikali iharakishe sera ya madini ili iweze kuchangia katika kodi za Serikali. Hii itasaidia pia gesi ambayo imeanza kuzalishwa kwani madini yote yana muda (*Life Span*). Serikali iangalie zaidi kodi katika sekta ya maliasili, kwani sekta hii haionyeshi kuchangia hasa ikilinganishwa na uvunjaji wake.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie Katiba kuhusu Mfuko wa Fedha wa Pamoja (*JFC*). Katiba haijaruhusu upande mmoja kukukusanya na kutumia. Katiba inasema mapato yote yataingia katika Mfuko wa Pamoja na baadae utaratibu wa matumizi utafuata. Naomba Serikali iangalie utaratibu mzima na iharakishe, kwani inaonekana kuwa hii ni kero.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia nikiwa mzima na salama; na vile vle napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Micheweni kwa kuendelea kuniwezesha kuwa Mbunge wao.

Mheshimiwa Spika, nikianza kuchangia katika Bajeti hii ya Serikali kwanza kabisa napenda nianzie kwenye mgao wa fedha kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mheshimiwa Waziri wa Fedha anasema kuwa Tume ya Fedha ya Pamoja imewasilisha mapendekezo yale Serikalini na mchakato wa kufikia maamuzi kuhusu mapendekezo hayo unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Tume hii siku zote inasema maneno hayo hayo tayari yamekamilika na kila siku tunaambiwa kuwa tume hii inaendelea tu haifiki mwisho na Serikali ya Zanzibar inaendelea kupunjwa mgao huu na inaendelea kupewa kiasi kidogo cha asilimia 4.5.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kuwa Serikali ya Muungano hajataku tu na ndio ikawa inapiga danadana. Sio kweli kuwa jambo hili ni gumu la kuchukua muda wote huu. Hakuna ukweli.

Mwisho, Mheshimiwa Waziri naomba ndani yake kuelewa ni lini Tume hii itakamilisha kazi hii. Mimi napata tatizo la kuelewa kila siku Bajeti ya nchi yetu inaposomwa na Mawaziri wetu wa Fedha huwa wanaongeza kodi. Kwenye sigara, vinywaji vikali, mvinyo na bia hivi sisi hatuna vitu vingine vya kuongeza bei au Serikali inaongeza sana kodi kwenye mambo hayo kwa kuwa ni mambo ya anasa.

Mheshimiwa Spika, vile vile nizungumzie kuhusu ushuru wa magari. Ushuru wa magari uliomo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha utawaumiza sana wananchi wa nchi hii kwa sababu watu wengi hawana uwezo wa kulipa ushuru huu na utasababisha watu kukwepa ushuru na wengine watawaumiza wananchi kwa kuwaongezea bei hasa wale matajiri wa daladala na madereva wa teksi. Kwa hali hii mimi napendekeza kodi hizi zipunguzwe pale palipowekwa Sh. 80,000/= ziwekwe Sh. 40,000/= na pale kwenye shilingi 230,000/= ziwe Sh. 100,000/= na pale kwenye Sh. 100,000/= ziwe Sh. 50,000/= tu.

Mheshimiwa Spika, kodi za mafuta huko ndiko kwenye kizaazaa zaidi kwani unapoongeza mafuta unaongeza kila kitu, hivyo basi kodi hii imewaumiza sana wananchi kwani unapoongeza kodi ya mafuta unawapa watu wenye uwezo kuongeza fedha kila kitu chao kwa kisingizio cha mafuta. Hapa mwenye gari, kiwanda, meli, boti, mashine za kusaga nafaka na kadhalika. Wote hawa wataongeza bei na ni haki yao kufanya hivyo, Serikali itafute vyanzo vingine iachane na kodi hii.

**MHE. FELIX N. KIJKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Fedha kama ifuatavyo:-

Kuhusu sekta ya maliasili na utalii ni vema kwa makusudi mazima kuwepo kwa usimamizi wa mapato yatokanayo na rasilimali ya wanyamapori. Ukweli ni kwamba wapo wajanja ambao wamegeuza mapori kama mali zao na kwa kujijua hivyo Serikali inajikuta inapoteza mapato bila kujua mali inayochukuliwa.

Napenda kufafanua hili nikitoa mfano kwamba mgao wa fedha unatolewa kwenye Halmashauri za Wilaya kwa kulipwa asilimia 25 inayopatikana katika pori ni uongo.

Katika pori la Mayowosi lililopo katika Mkoa wa Kigoma na Wilaya ya Kibondo na Kasulu zikimiliki pori hilo kuna uwanja wa ndege. Ndege za watalii zinafika hapo hapo na kuchukua maliasili yetu pasipo Serikali kujua. Ipo lugha kwamba watalii wanapokwenda huko husindikizwa na watumishi wa maliasili ama wenye *plots*, hao hawawezi kusimamia ushuru kwa sababu wao siyo watalaamu wa ushuru.

Hali hii pia inayakumba maeneo yenyе machimbo ya madini mahali ambapo mchanga wenye dhahabu huchukuliwa kwa kupakiwa kwenye *containers* na kupelekwa nje ya nchi. Hivi karibuni vyombo vya habari vimelaani kwa ukali kitendo hiki ambacho ushauri wangu kwa Wizara ya Fedha ni kutumia chombo ch *TRA* chenye ujuzi na uzoefu katika kupambana na hali hii. Ni kichekesho na aibu kwa Serikali kupokea asilimia 25 kwa madai kwamba ndicho kipato kilichopatikana eneo linalohusika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Serikali ya Awamu ya Nne iliahidi kupitia upya mikataba ya madini. Bajeti haijazungumzia hili. Tunawaeleza nini wananchi na hasa hawa wachimbaji wadogo wadogo?

Onyo kabla ya malalamiko ni kwamba utaratibu wa wafanyabiashara wanaodaiwa wawajibikaji kuwa wapitishiwe mizigo yao haraka huko Bandarini kutatoa mwanya kwa wafanyabiashara hao kukwepa ushuru na kuliibia Taifa. Wengi wa watu wa aina hii watakuwa ni wenye asili ya Kiasia ambao uzoefu umeonyesha kutokuwa na uaminifu katika biashara zao. Baada ya ushauru huu mdogo naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kuwa naunga mkono Bajeti hii. Sababu ya kuunga mkono Bajeti ni pamoja na:-

Bajeti ya mwaka 2007/2008 imeweka vipaumbele ambavyo katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2005 tulijiwekea wenyewe na ndiyo iliyotuwezesha kupata kura za wananchi. Hivyo Bajeti hii inajibu matakwa na matarajio ya wananchi. Bajeti hii kwa ujumla wake ni Bajeti ya mwananchi. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kuandaa Bajeti nzuri yenye matumaini, wajibu wetu kama wawakilishi wa wananchi ni kusimamia kwa karibu utekelezaji wake kwa kushirikiana na wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi zangu napenda kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha juu ya eneo ambalo kama lingesimamiwa vizuri na kuwa na mpango mzuri linaweza kuiongezea Serikali pato maradufu.

Mheshimiwa Spika, uvuvi unachangia asilimia 8.0. Katika thamani ya mauzo yote bidhaa za nje mwaka 2006 ukuaji wa uvuvi ulikuwa asilimia 5.0 ikilinganishwa na asilimia 7.4 mwaka 2005. Hii ilitokana na meli nyingi za uvuvi kuchelewa kuingia baharini. Tatizo hili halina uhusiano wa maziwa. Uvunaji wa samaki nchini mwaka 2006, ilikuwa tani 350,000. Uvunaji katika maji baridi ilikuwa 300,000 sawa na asilimia 86.

Ziwa Victoria linachangia zaidi ya asilimia 86 ya mazao ya uvuvi nje ya nchi na ilikuwa shilingi 170.2 bilioni zaidi ya asilimia 80 ya samaki kutoka maji baridi. Katika Jimbo la Ranya kuna vikundi 36 vya uvuvi. Vikundi hivi vinachangia mauzo ya samaki ndani na nje ya nchi. Kwa miaka mingi samaki wanaovunwa katika Jimbo la Ranya wanaishia nchi ya jirani na Serikali hukosa mapato ya kuimarisha Mfuko wa Taifa.

Serikali kupitia Wizara ya Maliasili, uvuvi na Wizara ya Fedha ziwe na mipango mkakati ya kusimamia mavuno ya samaki katika Ziwa Victoria hususan sehemu ya Jimbo la Ranya ambayo samaki wengi wanavunwa na mapato yanapotea.

Wizara ya Fedha ianzishe Ofisi ndogo ya TRA katika Jimbo la Ranya ili wataalamu wa TRA waweze kukusanya mapato yatokanayo na samaki.

Nchi jirani ya Kenya wanamiliki asilimia ndogo ya Ziwa Victoria lakini katika mji wa Kisumu, Kenya kuna viwanda takribani 10, wanapata samaki kutoka wapi? Kutosheleza viwanda vyao jibu kutoka kwa vikundi 36 vya wavuvi Jimbo la Ranya.

Mheshimiwa Spika, ifanywe tathmini kuhusu kiwango cha tani za samaki zinazopatikana kutoka Jimbo la Rarya na thamani ya fedha zitokanazo na uvunaji wa samaki kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Wizara ishirikiane na vikundi 36 vya wavuvi ili kudhibiti magendo ya samaki yanayofanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu. Wananchi wapewe motisha kwa kusimamia zoezi hili na wavuvi wapate motisha kama kusamehewa ushuru katika zana za uvuvi.

Wizara inayohusika na maliasili ivihamasish vikundi vya uvuvi kupata asilimia tano ya fedha zitokanazo na mauzo ya ndani na nje ya nchi ili kuchochea maendeleo vijijini. Naomba Mheshimiwa Waziri azingatie na kufuutilia ushauri niliofa, nitashirikiana naye ili Serikali iweze kuongeza mapato yake maradufu kama sio zaidi badala ya shilingi 6.2 bilioni mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Waziri wa Fedha na timu yake kwa kutekeleza sera na Ilani ya uchaguzi ya CCM kuhusu ushirikishwaji wa wananchi katika mipango yao ya maendeleo na kusimamia miradi yao.

Nampongeza sana kwa hatua ya Wizara ya Fedha iliyochukua kupeleka madaraka kwa wananchi (*D by D*) kuitia Serikali za Mitaa. Kwani maamuzi mengi yanahuusu mipango na utekelezaji wa wananchi yaliyokuwa yanashughulikiwa na Serikali Kuu kuitia Wizara husika. Rasilimali ilikuwa inasimamiwa na kudhibiti na Wizara. Urasimu ulikuwa kero na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa mipango vijijini. Nampongeza sana Waziri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uamuzi huu wa kimapinduzi napenda kutoa ushauri kwa Wizara ili zoezi hili lisije likakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, Halmashauri nyingi zina matatizo kuhusu uchache wa wahasibu, maafisa mipango, wakaguzi wa ndani na kadhalika. Pamoja na nia njema ya Serikali ya kuajiri wataalamu hao, ni vema mpango huu ufanyike haraka na kwa uangalifu mkubwa ili wataalamu watakaosajiliwa, wawe wale waliochujwa, wenye sifa na maadili. Ubadhirifu ulioko katika Halmashauri zetu zinatokana na watendaji wasio na maadili.

Uhamishwaji wa rasilimali fedha katika Halmashauri zetu utaongeza wingi wa fedha katika mfuko wa Halmashauri. Ili usimamizi wa fedha zitakazohamishwa katika Halmashauri uweze kudhibitiwa, napendekeza utaratibu wa Hazina ndogo zilizopo Mikoani, mpango ufanywe ili Hazina ndogo zifunguliwe Wilayani na wataalamu wa kutosha waajiriwe katika Hazina hizo. Naunga mkono hoja.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezesaji na Waziri wa Fedha kwa hotuba zao kuhusu hali ya uchumi na Bajeti ya mwaka 2007/2008. Hoja yangu kubwa mimi ni kuhusu misaada ya mikopo tunayopata kutoka kwa wahisani. Naomba sana

misaada na mikopo hii ilengwe kwenye sekta ambazo zitatuwekea uwezo wa kujitegemea hapo siku za baadaye kwa mfano:-

Mheshimiwa Spika, uchumi wa jiografia, tutumie misaada na mikopo hii kupanua Bandari ya Dar es Salaam na Bandari ya Kigoma. Bandari ya Dar es Salaam inaweza kupanuliwa na upande wa Mashariki ambayo iko wazi. Bandari hizi zikipanuliwa na reli ya kat iimarishwe na kuwa na uzito wa paundi 120. Pamoja na hilo barabara zote zinazoenda nchi jirani za Uganda, Rwanda, Burundi, DRC na Zambia ziimarishwe kwa kiwango cha lami. Jambo hili pekee la Bandari za Dar es Salaam na Kigoma, reli na barabara linaweza kuijengea nchi uwezo wa kujitegemea baadaye.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukusanyaji wa kodi na maduhuli, Serikali ifikie uamuzi wa kuimarisha ukusanyaji wa kodi na maduhuli mengine. Mfano leseni za uwindaji hapa nchini ziko chini sana ukilinganisha na nchi nyingine hapa Afrika. Pale ambapo kuwinda simba au chui ni dola 7,000, nchi zingine inafikia dola 40,000. Pia uvunaji wa mazao ya misitu na mazao ya baharini unawanufaisha watu wachache, Serikali isimamie kwa makini sana eneo hili na kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, kama inawezekena basi kodi iliyopo kwenye mafuta ya taa ihamasishwe kwenye simu za mikononi. Mwisho napenda kuipongeza sana Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na TAMISEMI kuimarisha Halmashauri zote nchini kiutawala na kiuhasibu hasa kukamilisha kanuni za ununuzi kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, hali ya Bajeti ni ngumu mno na ina tatizo kubwa kwa wananchi. Ni kweli si vyema kuwa na Bajeti tegemezi lakini hali halisi ni mbaya. Unapopandisha bei ya petroli na dizeli unapopandisha bei ya kila kitu, gari ni sehemu ya vitu muhimu katika maisha ya mtu, sasa unapopandisha ada ya kutunza hata gari la mtu, ni mateso. Kuruhusu baadhi ya bidhaa zipite bila ya kazi ya upukuzi ni kuleta fursa ya kuingiza nchini vitu vya hatari. Bajeti yenye kazi ya upukuzi ni kuleta fursa ya kuingiza nchini vitu vya hatari. Bajeti yenye haioneshi namna ya kuondoa umaskini bali kuongeza umaskini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ajira, hata katika Ilani ya uchaguzi ya CCM haileti maana kuiachia sekta binafsi bali ni kazi ya Serikali. Bajeti ya kilimo ni ndogo ukilinganisha na mahitaji. Bajeti haioneshi namna itakavyokusanya kodi katika sekta muhimu sana ya uvuvi, imeeleza juu juu tu. Bajeti imeeleza kwa juu juu namna itakavyochangia Zanzibar kwa *formula* ya 4.5%, lakini je, ni kiasi gani kinategemewa kupatikana ili wananchi waelewe?

Mheshimiwa Spika, mchango wa sekta muhimu ya mifugo haupo wazi pamoja na kuwa nchi yetu ina mifugo mingi sana. Suala la elimu ya juu lilipaswa kuelezwu vyema hasa baada ya kudhihirika kuwepo kwa uwezo mdogo wa kuchangia kwa wananchi.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia hotuba hizi, ninawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Fuoni kwa kunichagua na nikaweza kuwa Mbunge wa Jimbo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze *TRA* kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kukusanya mapato mengi na kuiwezesha Serikali kupanga Mapato na Matumizi na kuiwezesha Mipango na Uchumi wa nchi yetu kukua.

Mheshimiwa Spika, ninachokiomba kwa Serikali ni kuhakikisha mipango tulioileta katika Bajeti hii tuhakikishe tunaitekeleza na kuifuatilia na isiishie kwenye vitabu. Tukiifuatilia mipango hii Bajeti hii itakuwa haina ugumu wowote kama inavyozungumzwa na wengi huko Mitaani.

Mheshimiwa Spika, Bajeti yetu imepandisha kodi ya mafuta ya aina zote na hili ndilo linaloleta minong'ong'o kwa wananchi kwa kuhofia upandaji wa bei za bidhaa. Suala hili la kupanda kwa bei kwa bidhaa ni kweli lipo na lakini si sababu ya mafuta, kila siku bidhaa zinapanda bei bila ya kupanda bei ya mafuta.

Ninachokiomba Serikalini kuwe na mikakati ya kuzuia mfumuko wa bei, pia naomba ifikirie sana suala la mafuta ya taa hasa kwa vile ni nishati inayotumiwa na kila mtu hasa mwananchi wa chini kabisa na kodi hii itafutiwe mbadala ihamishwe kwenye maeneo mengine ili Bajeti yetu isipungue kama ilivyokaridiriwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wastaa fuwa ili yokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuna wazee wetu ambao wamefanya kazi na kustaafu baada ya kuvunjika Jumuiya hiyo hadi leo hawajapata mafao yao, wengine hata majina yao hayajatoka kwenye magazeti na wengine majina yametoka magazeti na kukamilisha taratibu zinazotakiwa. Hadi leo hakuna utaratibu wowote unaoendelea wala hakuna taarifa zozote zinazotolewa kwa wahusika na kusababisha usumbufu wa ufuatiliaji na kupoteza fedha nyingi za nauli na mambo mengine ya kujikimu.

Naiomba Serikali ituambie imefikia wapi na inalishughulikiaje suala hili ili wale wote wanaohusika wapate mafao yao hasa ukizingatia wengine wamekuwa wazee sana na hawawezi kufuatilia na wengine wamefariki na wameacha watoto yatima.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo yatolewe ili wahusika wajue wafaye nini ili wapate haki zao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hizi kwa asilimia zote mia moja.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Iramba Mashariki ni wakulima wazuri sana wa alizeti, wanaendelea kuiomba Serikali izidishe kodi ya mafuta yanayotoka nje ili wao wapate bei nzuri ya alizeti yao ambayo itawasaidia kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Iramba Mashariki wanaomba msaada toka Serikalini ili waanze kulima zao la Mbongo (*Jatropha*) ambalo linastawi vizuri sana Mkoani Singida hasa Iramba Mashariki.

Kuhusu mafuta ya taa tunaomba sana Serikali itafute njia nyingine ya kupata fedha toka vyanzo vingine ili iwaokoe wananchi kwa kutoongeza bei ya mafuta ya taa. Hii itasaidia sana kulinda misitu yetu isimalizike kwa kuchoma mkaa na kukata kuni.

Kuhusu mizigo kupita bandarini bila kukaguliwa, mpango huu usitishwe kwanza kwani utaleta matatizo makubwa kwa watu kuingiza mizigo kiholela na kweli kuna uwezekano mkubwa wa kuangiza bidhaa zisizo na viwango na hata kuleta bidhaa nyinginezzo ambazo ni hatari.

Mheshimiwa Waziri wakati umefika sasa wa Wilaya ya Iramba kugawanywa, wananchi wa Iramba Mashariki wapewe Wilaya yao ili waachane na mateso wanayopata ya kwenda kupata huduma za matibatu Mkoa wa Manyara tena kwa kulipia, kila mwezi walimu wanapoteza siku tano za kazi kufuata mishahara yao Wilayani ambako ndiko iliko Benki. Wastaafu wa Iramba Mashariki walishasamehe kufuata fedha zao za pensheni kwa sababu pensheni ni ndogo kuliko gharama za usafiri wanazotumia.

Mheshimiwa Spika, vigezo vyote vya kupata Wilaya viro na tarehe 23 Septemba, 2005 Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alishaahidi wananchi wakati alipokuwa anajinadi kwa wananchi wa Iramba Mashariki alipofanya mkutano wa hadhara kwenye miji midogo na Iguguno.

**MHE. MWAKA ABRAHAMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuzipongeza hotuba zote mbili, ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kwa maandalizi yao mazuri ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gawio la 4.5%, linahusu *formula* ya muda, iliyokubaliwa tangu mwaka 1994 baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kuipatia Zanzibar:

- (i) Faida ya kila mwaka ya Benki Kuu ya Tanzania.
- (ii) Misaada ya fedha za nje kutoka kwa wafadhili wanayoisaadia Tanzania kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, gawio hilo limeanza kutolewa tangu Julai, 1995, lakini ieleweke kuwa gawio hilo ni la muda tu hadi pale Tume ya Fedha ya Pamoja itakapopendekeza kwa Serikali zote mbili gawio la kudumu kwa ajili ya mapato na matumizi ya muungano baina ya pande hizi mbili za Jamhuri yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ingawa mazungumzo ya SMT na SMZ yanaendelea hadi sasa lakini imechukua muda mrefu sana (tangu Tume hiyo ya Fedha ilipoanza kazi zake mwaka 2005.)

Mheshimiwa Spika, wakati sasa umefika kwa Bunge hili kuelezwu ni lini gawio la kudumu litaamuliwa ili kuondoa kero hii ya Muungano ambayo ndiyo kero muhimu

kuliko kero zote za Muungano zilizopo kwani bila ya kuweka *formula* ya kudumu ya kugawana Mapato na Matumizi ya Muungano, Zanzibar itaendelea kuumia zaidi kiuchumi kuliko Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu mafuta. Kwa upande wa mafuta ya taa haya yanatumika sana hapa nchini kwa matumizi mbalimbali ukizingatia zaidi huko vijijini ambako hakuna umeme. Hivyo, ongezeko la bei ya mafuta litawaumiza sana wananchi hasa wale wa kima cha chini. Naishauri Serikali ipunguze bei ya mafuta ya taa ili watu wa hali ya chini waweze kumudu kununua mafuta ya taa kwa matumizi ya lazima.

Pia nzungumzie kuhusu upandaji wa mafuta ya petroli na dizeli. Kupanda huku kwa mafuta kutamuathiri mkulima kijijini, mwananchi wa kawaida na hata wanafunzi wanaopanda daladala. Naishauri Serikali itafute mbinu nyingine ya kuingiza mapato ya Serikali na kupunguza bei ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, sasa nichangie Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kuhusu wawekezaji. Nchi yetu Mwenyezi Mungu ameipa baraka kubwa kwani ina bahari na mapori makubwa ambayo hawaishi watu. Nashauri Serikali iletu wawekezaji ambao wataweza kujenga viwanda vya kusindika samaki kupelekwa nje kwa kuuuzwa. Pia kujengwe viwanda vya kutengeneza *juice* za chupa na maboksi ziweze kuuzwa nje ili kuipatia kipato Serikali na kuwapatia ajira wananchi, kwani nchi yetu ina matunda mengi sana na kufikia kuharibika.

Mheshimiwa Spika, pia wawekezaji wapewe mapori kwa ajili ya kilimo tofauti kwa kutumia nyenzo za kisasa kuliko kuachwa mapori matupu bila ya kulimwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja zote mbili mia kwa mia.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Spika, ni vyema nitoe shukrani zangu kwako wewe binafsi pamoja na wale wote waliota michango yao kwa kuweza kufanikisha Bajeti yetu ambayo ina mtazamo wa azma ya Serikali ya kuwawezesa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na azma hiyo tukumbuke kwamba hakuna kizuri kisicho na kasoro. Kwa hiyo, mimi nitoe mtazamo wangu kwa yale ambayo yanaonekana na kasoro.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara zilizopewa vipaumbele tuitupie macho Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Serikali inajisahau sana kuwa na kumbukumbu za maafa ya njaa yaliyotukumba ambayo yaliitikisa Serikali na kusababisha viongozi wetu kuhangaika ili kuwanusuru Watanzania. Mlipuko wa njaa nchini kutokana na ukosefu wa vyakula hili husababishwa na ama kukosekana kwa mvua au kuwepo kwa mvua nyingi. Mambo haya ni siri ya Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, vitu kama gesi ya kuzimia moto na *pempas* (Nepi) ni Watanzania wangapi wanaotumia vifaa hivi? Serikali imeondoa kodi vitu visivyotumika na wengi kwani watu wengi wanaoishi vijijini hawajui hata matumizi ya vifaa hivyo!

Mheshimiwa Spika, nepi (*pempas*) ni wachache wanaotumia na hasa wale wa mijini na wenye uwezo. Kivazi hiki mara nyingi huviswa watoto ama wagonjwa tena kwa mara moja hivyo ni vyema kumpa msaada mwenye uwezo au ni ile lugha isemayo nyongeza huenda juu ya fungu?

Kuhusu gesi ya kuzima moto, ni kweli silaha hii ni nzuri lakini Serikali ifikirie, dereva kuua mmoja ni bora kuliko kuua wengi, kama hii ni kweli ni kwa nini kuwapatia nafuu wachache ikaacha kuwanusuru wengi? Au tuseme ni kutaka viwanda viweze kuwa na zana hiyo? Ni imani yangu hili limeeleweka. Ahsante.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukupongeza wewe pamoja na Naibu Spika kwa kutekeleza majukumu yenu kwa *Standard and Speed*. Ulipoahidi mbele ya Bunge hili kwamba utatekeleza majukumu yako na maslahi ya Wabunge na umefanya hivyo, hongera sana.

Naomba sasa niwapongeze Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Waziri wa Fedha Mheshimiwa Zakia Meghji, kwa hotuba zao nzuri walizoziwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Hii ikiwa ni Bajeti ya pili ya Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, japokuwa kipindi kilichopita uchumi wetu ulikabiliwa na matatizo makubwa ya ukame, upungufu wa umeme na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia, lakini waliweza kuendeleza uchumi wetu bila kuyumba na sasa hivi kuleta mapandekezo mazuri ya kuendeleza uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba nielezee kwa kifupi mambo makuu mawili yanayotakiwa kuzingatiwa kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kama ifuatavyo:-

(a) Kujenga uchumi wa kisasa unaoendelea kukua kwa kasi na endelevu ambao utawatoa wananchi wetu katika umaskini na kulifanya Taifa letu liwe katika hali ya kati.

(b) Kuwawezesha wananchi kiuchumi ili waweze kumiliki na kuendeleza uchumi wao wenyewe, hotuba zote za Mawaziri zinajieleza.

Mheshimiwa Spika, bado kuna maeneo ambayo pia tunatakiwa kuyatazama kwa uangalifu zaidi. Moja ya maeneo haya ni kushuka kwa ukuaji wa Pato la Taifa. Pato la Taifa lilikuwa kwa asilimia 6.2 na asilimia 5.9 kwa kipindi hicho na ukuaji wa asilimia 6.7 mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, naomba tutambue wazi kwamba ili maendeleo yapatikane katika uchumi wa nchi yoyote huduma za taasisi za vyombo vyta fedha ni muhimu sana. Wananchi wengi wanazo nyenzo za uzalishaji kwa maana kwamba wanayo ardhi na

nguvu kazi. Tatizo kubwa ni mitaji pamoja na ujuzi wa ujasiriamali. Bado kwa Watanzania wengi suala la mikopo linaonyesha kuwa asilimia 4 tu ya wananchi vijijini wanakopa mabenki wakati asilimia 38 ya wananchi wanakopa kutoka kwa marafiki au familia.

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali ya Awamu ya Nne kwa uamuzi waliofanya ili kuwawezesha wananchi kupata mikopo ya masharti nafuu kuititia benki za *CRDB* na *NMB* katika utaratibu huu kila mkoa umetengewa shilingi bilioni moja, mtazamo wangu ni kwamba fedha hizi zilizotolewa bila kuwepo mafunzo juu ya utaratibu wa kuwawezesha wananchi kupata mikopo. Ni matumaini yangu kuwa katika awamu hii ya pili na mpango huu ili kuondokana na matatizo yaliyojitokeza wananchi sasa wapatiwe elimu ya ujasiriamali, kanuni na taratibu za kupata mikopo.

Aidha, kukabiliana na changamoto zilizopo katika sekta ya fedha ambazo ni pamoja na kiwango kikubwa kikubwa cha riba za amana na za mikopo, eneo hilo lifanyiwe kazi mapema ili hatua za uwezeshaji zilizopangwa na Serikali ziweze kufanikiwa. Mathalani *SACCOS* zilizoanzishwa na Serikali ziweze kufanikiwa kama riba itakuwa kubwa lengo na mkakati mzima wa uwezeshaji wananchi halitaza matunda yaliyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, wastani wa kasi ya upandaji wa mfumuko wa bei (*inflation*) katika mwaka 2006 ulikuwa kwa asilimia 7.3 ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, huu ni wakati mzuri sasa kwa Serikali yetu kujihami na upatikanaji wa umeme ili kuzuia hasara isitokee katika uchumi wetu. Mikakati ilioandalialiwa wakati wa uhaba wa umeme iendelezwe hasa ikizingatiwa kuwa hadi kufikia mwisho wa Juni, 2007 shilingi bilioni 204.5 zitakuwa zimetumika kununua na kukodi mitambo ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2006/2007 wananchi wamekuwa wakilalamikia makali ya uchumi yaliyotokana na għarama kubwa za mahitaji yao ya kila siku hasa mahitaji ya msingi (*basic needs*). Chanzo cha hali ni mfumuko wa bei ulioongezeka kutokana na bidhaa zinazohusiana na chakula na ule uliohusiana na chakula. Mafuta yamechangia kwa mfumuko wa bei kwa asilimia 9 kwa kuwa Tanzania hatuzalishi mafuta inabidi tuendelee kuagiza mafuta ambayo hakuna dalili yoyote ya bei ya dunia kupungua. Hivyo basi mafuta yataendelea kuchangia mfumuko wa bei nchini.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ni kuwa ughali wa mafuta unagusa maeneo mengi ya kiuchumi katika Bajeti ya mwaka huu, ushuru wa mafuta aina zote umepanda yakiwemo mafuta ya taa, petroli, dizeli na mafuta ya viwandani. Kuongezeka kwa ushuru wa mafuta ya dizeli na petroli kutaongeza għarama za usafirishaji ambazo zitawagusa wananchi. Pia għarama za usafirishaji, ada ya leseni za magari zimeongezeka na hili litawagusa wananchi moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, kupanda kwa kodi na ushuru wa mafuta kutaleta athari za kuongezeka kwa gharama zinazowagusa wananchi wa kawaida moja kwa moja. Hali hii haiwezi kuleta afueni kwa wananchi wengi, hivyo nashauri Serikali kuangalia upya uamuzi wake wa kuongeza ushuru wa mafuta. Aidha, ushuru wa mafuta ya taa ni vema ukapunguzwa hasa ukizingatia kuwa hii ni moja ya nishati inayotumiwa na wananchi wengi wa kipato cha chini kama kule Simanjiro, Kiteto na maeneo mengine ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika suala la madini naishauri Serikali kuendelea na hatua zake kuhakikisha kuwa Taifa linapata manufaa zaidi kutokana na uwekezaji katika sekta ya madini ili kuongeza mchango wake katika sekta ya madini na katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mimi ninatoka Manyara na kati ya wananchi ninawawakilisha katika Bunge hili ni pamoja na wananchi wa eneo la Mererani, eneo maarufu kwa uchimbaji *Tanzanite*.

Mheshimiwa Spika, kinachonisikitisha ni kwamba madini haya hayapatikani mahali pengine popote duniani isipokuwa ni Mererani peke yake. Madini haya tunayadharau wenye kana kwamba hayana maana. Leo hii tunasikia mauzo ya dhahabu nje ni asilimia 46 wakati kwa habari ya *Tanzanite* hakuna kitu kinachoeleweka. Serikali inazungumzia *Nickel*, dhahabu na chuma tu, naomba sana Mawaziri hawa watakopokuwa wanahitimisha hoja zao nataka nielezwe kuwa Tanzania imechangia kwa kiasi gani mauzo ya nje? *Tanzanite* inayochimbwa na wawekezaji asilimia 30 tu ndiyo wanayopeleka kwenye Soko la Dunia wakati *local miners* wanaanza asilimia 70, huoni kuwa Serikali yetu inaacchia madini yanauzwa kiholela tu? Ikiwa Bunge lilikaa na kuitisha Sheria ya Madini ya Vito kwamba yasipelekwe katika Soko la Dunia kabla ya kukatwa na kusafirishwa, itakuwa rahisi kuyadhibiti madini haya.

Je, Serikali haioni kuwa kutokufanya hivyo madini mengi yanasafirishwa kiholela yakiwa bado hayajakatwa?

Mheshimiwa Spika, napongeza mpango huu wa Seriakli kuanzisha *EPZ* ili kuwavutia wawekezaji. Naomba *EPZ* ianzishwe Mererani ili kudhibiti *Tanzanite* na kurudisha heshima ya madini haya. *EPZ* ianzishe Mererani itawasaidia wananchi zaidi ya 500,000 kupata ajira Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanzania nzima kunufaika na mpango huo. *EPZ* Mererani itaua soko la *Jaipur* lililoko India na Thailand ambapo ndipo kilipo kiwanda kikubwa cha kukatia madini ya vito. Hivyo madini yote ya Tanzania yanapelekwa *Jaipur* kwa ajili ya kukata ndipo yapelekwe kwenye soko la dunia. *EPZ* ikiletwa Mererani tutayadhibiti madini yetu na Pato la Taifa katika sekta hii litaongezeka. Wafanyakazi wa *Jaipur* walioko India na Thailand watakosa kazi na watakuja kutafuta kazi hapa.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyokuwa zamani Kenya waliitangazia dunia kuwa *Tanzanite* inachimbwa Kenya mpaka wakapatiwa tuzo, vivyo hivyo *South Africa* sasa inatangaza kuwa *Tanzanite* inatoka kwao kila mara na kila mwaka *TAMIDA* walikuwa wakiandaa *Auction*. Wageni kutoka pande za dunia walifika Arusha kuja kununua madini ya *Tanzanite*. Wakati huo huo madini mengine kama *Green Ginet*, *Suphirre*,

*Amethyst, Rodolite, Red Gynet, Blue Surphire, Almandite* na kadhalika, yalikuwa yakipata bei na wachimbaji wengine wananaufaika na hiyo *Auction*. Sasa hivi wageni wote wanaishia *South Africa* ndiko madini yote ya Tanzania yamehamia.

Mheshimiwa Spika, suala la *Auction* lipatiwe ufumbuzi wachimbaji wadogo wadogo wanalamika, hawana pa kuuzia madini yao, kwa sababu ya kukosa wageni wanunuzi wa madini katika Mji wa Arusha. Hali hii inatukosisha mapato makubwa sana katika sekta ya madini. Naomba *EPZ* ianzishwe Mererani haraka.

Mheshimiwa Spika, suala la Barabara inayotoka *KIA* kwenda Mererani, ni kivutio cha wawekezaji, inaunganisha Mikoa mitatu ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Rais wa Awamu ya Tatu na Nne wote wametoa ahadi kwamba zijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara hii sasa ijengwe kwa sababu kauli ya Rais ni kauli ya Mungu, kwa hiyo, iheshimiwe na itekelezwe mara moja. Ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na afya njema na kuweza kunipa wasaa wa kutoa mchango wangu katika hoja ya Mawaziri wa Fedha yaani kuhusu Bajeti ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya 2007/2008 ni ngumu sana ikilinganishwa na Bajeti za miaka mingi ya nyuma. Maana kwa ujumla Bajeti hii haikumlenga mwananchi wa kawaida yaani yule wa kipato cha chini au Serikali katika kuandaa Bajeti hii labda ilisahau ule mkakati wake wa kuondoa umaskini nchini (MKUKUTA).

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu unapopandisha ushuru wa mafuta kama ya petroli, dizeli na yale ya taa basi ni kwamba utakuwa umemgusa kila mwananchi hasa katika maeneo ya vijijini ambako hakuna huduma za umeme.

Mheshimiwa Spika, kupanda kwa ushuru wa bidhaa ya mafuta kutaifanya hali ya maisha nchini kupanda yaani gharama ya maisha itaongezeka maradufu. Gharama za usafiri na usafirishaji zitapanda, hivyo kuzifanya bidhaa zote kupanda bei.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali ingetafuta vyanzo vingine ambavyo vipo vingi nchini badala ya kuongeza ushuru wa bidhaa ya mafuta na hivyo kumnusuru mwananchi na hali ngumu ya kupanda kwa maisha.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna vyanzo vingi tu ambavyo viliainishwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni siku alipowasilisha maoni ya Kambi kuhusiana na Makadirio na Matumizi ya mwaka 2007/2008 (angalia kiambatisho 1 ukurasa wa 47 wa hotuba ya Kiongozi wa Upinzani na Msemaji wa Wizara ya Fedha).

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa utaratibu wa kupitisha moja kwa moja (*fast tracking*) bila ukaguzi bidhaa zote zinazoagizwa na wafanyabiashara ambao tayari

wameshaainishwa kama wawajibaki wazuri na hapa pia Serikali imeenda mchomo. Utaratibu huu ni mbaya sana na unaweza kuingiza Serikali katika matatizo ya aina yake.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara hawana uaminifu wa kuendelea atajiaminisha leo, lakini kesho ataanza visa. Serikali inataka kuanzisha mwanya wa kumruhusu kuingizwa nchini bidhaa za ajabu ajabu kama vile dawa za kulevya na hata bidhaa ambazo kwa kawaida ni haramu kuziingiza nchini.

Mimi napenda kuuliza swal moja tu, hivi Serikali itakuwa na mikakati gani ya kuhakikisha kuwa bidhaa ambazo zitaingizwa nchini na hao wafanyabiashara wanaoitwa wawajibaki ni zile tu bidhaa ambazo ni halali kuingizwa nchini?

Mheshimiwa Spika, pamoja na vyanzo vingi vya kuliingizia Taifa mapato ambayo viliainishwa katika maoni ya Kambi ya Upinzani, sasa ni jukumu la Serikali kubadili *mind set* ili kuliokoa Taifa hili dhidi ya kutumbukia katika umaskini wa kutupwa. Serikali iongeze kima cha chini cha mishahara kwa wafanyakazi angalau kufikia shilingi 215,000/= hivyo kuongeza wigo wa kodi kama ilivyopendekezwa katika maoni ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, suala la kwamba wananchi wajikaze mikanda kukabiliana na hali hii halina maana yoyote wala hayo ya kujikaza mikanda sijui kama imeelezwa kwenye Ilani ya CCM! Vipi wananchi wajikaze mikanda na uchumi upo nchini? Suala hapa ni Serikali ibadilishe, ifuate ushauri unaotolewa bila kujali itikadi kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa nchi ukiimarishwa na wananchi wakapata unafuu wa maisha, sifa zitaenda kwa nani? Sote ni Watanzania na sote tunaitakia mema nchi yetu, sote tutajihisi wenye furaha kama tutaona siku moja mwananchi wa nchi hii anapata mikoa mitatu kwa siku bila usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kufikia hatua hiyo kunahitaji viongozi wanaojali sana nchi yao na maendeleo ya wananchi wao. Tujitumeni tuchukue na tufanyie kazi ushauri wa wengine kwa kutambua kwamba kila mwenye ujuzi basi yuko mwenye ujuzi zaidi kuliko yeeye na ujuzi wote unakubalika kwa Mwenyezi Mungu (*Quran Tukufu*).

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na siungi mkono Bajeti hii. Ahsante sana.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja hizi kwa asilimia zote. Suala linalopigiwa kelele sana kwenye Bajeti hii inaonekana ni ongezeko la ushuru wa bidhaa za mafuta. Mimi nataka nitofautiane na hao wanaopinga hatua hizi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ushuru wa bidhaa za petroli ulioongezwa ni shilingi 22 na ushuru wa mafuta kwa ajili ya mfuko wa barabara ni shilingi 100, jumla ni shilingi 122 kwa lita. Kwa hiyo, utaona kwamba ushuru mkubwa wa mafuta ulioongezwa ni kwa ajili

ya mfuko wa barabara kwa ajili ya kutengeneza barabara zetu ili ziweze kuwa nzuri na kupidika vizuri na kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa barabara nzuri kwa uchumi wa nchi kuondoa umaskini wa wananchi hauna sababu ya kusisitizwa zaidi hasa kwenye kusafirisha mazao ya wakulima kwenda kwenye masoko ya kuleta pembejeo, mbolea na mahitaji mengine ya wakulima.

Kwa upande mwininge utafiti uliofanywa kwenye nchi kadhaa za Kiafrika unaonyesha kwamba kila shilingi 100 ambayo haiwekwi na Serikali kwenye matengenezo ya barabara mbaya, wasafirishaji wanaotumia barabara hizo wanapata hasara ya shilingi 346 kwenye gharama za matengenezo ya magari, magurudumu na mafuta mengi wanapotumia barabara hizo zikiwa mbovu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli bei ya mafuta ya magari iliyoongezwa na ongezeko hilo likaenda kwenye mfuko wa mafuta ya magari iliyoongezza na ongezeko hili likaenda kwenye mfuko wa barabara na barabara mbovu zikatengenezwa vizuri, gharama za uendeshaji wa magari ya wasafirishaji zinaokolewa kwa kiwango kikubwa kuliko ongezeko la bei ya mafuta linalopelekwa kwenye matengenezo ya barabara. Kwa hali hii wasafirishaji kwa kweli wasingestahili hata kuongeza nauli kutokana na ongezeko hii linalowaokolea gharama za uendeshaji wa magari yao.

Kwa maana hiyo, ongezeko la bei ya mafuta (kwa shilingi 120 hadi 150 kwa lita) linalokwenda kwenye matengenzo ya barabara ni kwa faida ya wananchi, haiwezi au haitakiwi kuwa kero au kumuumiza sana mwananchi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali lazima iwe macho na wauzaji wa mafuta na wasafirishaji wa abiria na mizigo wasije wakatumia mwanya huu kuwaumiza wananchi. Kwa mfano, kwa sasa bei ya petroli ni kwenye shilingi 1,275 kwa lita. Ongezeko la ushuru wa shilingi 122 litaongeza bei ya mafuta hadi kwenye shilingi 1400 kwa lita na si zaidi. Ili hatua hii ya Serikali isitumi vibaya na wauzaji wa mafuta (pamoja na ukweli kuhusu soko huria) lazima *EWURA* watusaidie kuadhibiti wauzaji wa mafuta na kuhakikisha bei ya petroli na dizeli haipandishwi kiholela na kupita sana kiwango cha ushuru ulioongezwa na Serikali. *EWURA* wawe macho na wawe wakali sana kwenye hili.

Lakini ukiacha wauzaji wa mafuta, wasafirishaji nao wanaweza kutumia huu mwanya wa Serikali kupandisha kidogo ushuru wa mafuta, kupandisha mno nauli za mabasi na magari ya mizigo/bidhaa. Kwa mfano, kama basi litokalo Dar es Salaam hadi Dodoma linatumia mafuta lita 200, ongezeko la bei ya mafuta ya (*say*) shilingi 150 kwa lita ina maana ongezeko la shilingi 30,000/= kwa safari ya Dar – Dodoma au shilingi 600 kwa abiria mmoja (30,000/= abiria 50). Lakini kama nauli ya sasa ni ni shilingi 12,000/=, badala ya kuongeza hizo shilingi 600/= ili nauli iwe 12,600/= au tuseme 13,000/=, anaweza kuongeza shilingi 3,000/= nzima na kufanya nauli kuwa shilingi 15,000/= au zaidi. Hapa napo *SUMATRA* lazima wabebe majukumu yao kudhibiti wasafirishaji ili wasiwanyonge wasafiri na wananchi kwa sababu tu Serikali imeongeza kidogo ushuru wa mafuta.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafuta ya taa ambayo kwa sasa bei yake ni karibu shilingi 1,000 kwa lita, Serikali imeongeza kiasi kidogo tu cha ushuru wa shilingi 4 kwa lita. Hiki ni kiasi kidogo sana ambacho hakitakiwi kiongeze bei ya bidhaa hii muhimu kwa zaidi ya Sh. 5/= hadi Sh. 10/=. Lakini udhibiti wa *EWURA* usipokuwepo, wauzaji wanaweza kuongeza bei ya mafuta ya taa hata kwa shilingi 100 na hivyo kuwaumiza wananchi.

Mheshimiwa Spika, kama udhibiti wa Serikali kupitia vyombo vyake kama *EWURA* na *SUMATRA* ukiwa makini, nyongeza hizi za ushuru kwenye bidhaa za mafuta zilizopendekezwa na Serikali ni ndogo na haziwezi kuleta athari kubwa kwa maisha ya wananchi kama Wapinzani wa hatua hizi wanavyojaribu kupotosha wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote za Waziri wa Mipango, Uchumi na Uvezeshaji na Waziri wa Fedha.

**MHE. MWADINI ABAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hotuba hii nitauelekeza katika mambo mawili makubwa ambayo yamekuwa ni kero kwa wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa Mamlaka ya Mapato Tanzania imekuwa inaendelea kuimarisha usimamizi wa kodi na mapato mengineyo yanayokusanywa na mamlaka hiyo.

Aidha, mfumo wa utozaji kodi baina ya Zanzibar na Tanzania Bara umefanywa kuwa ni wa aina moja, tofauti na ilivyokuwa siku za nyuma, hali ambayo ilikuwa inapigiwa kelele sana na wafanyakishara wanaoleta bidhaa zao kutokea Zanzibar wanapotakiwa kulipa tofauti ya kodi kutokana na mifumo miwili tofauti ya utozaji kodi baina ya sehemu mbili hizi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili linaonekana kuwa ni mionganoni mwa kero zinazoathiri mustakabali wa Mungano wetu. Baada ya urekebishaji wa mifumo ya kodi kuwa sawa baina ya Tanzania Bara na Zanzibar wananchi wa Zanzibar na wafanyakishara wengine walitarajia ule usumbufu wa kutozwa kodi, ushuru wa ziada kwa bidhaa zinazotoka Zanzibar (*Double taxation*) ungeondoka.

Mheshimiwa Spika, la kusikitisha ni kwamba hali leo hii ipo vile vile. Wazanzibari pamoja na wafanyakishara wengine wanaendelea kusumbuliwa na wafanyakazi wa *TRA* Tanzania Bara kwa kutakiwa kulipa kodi/ushuru wa ziada kwa bidhaa zinazotoka Zanzibar.

Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu ni kwa nini usumbufu huu mpaka leo haujandolewa licha ya kuwa mfumo wa utozaji kodi/ushuru baina ya pande mbili hizi za Muungano hauna tofauti yoyote. Ni lini basi usumbufu huu wa *double taxation* utafutwa ili kuondoa hii kero inayodhoofisha Muungano wetu?

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la pili linalowakumba wananchi ni pale wanaposafirisha magari yao yaliyosajiliwa Zanzibar kuja Tanzania Bara. Adha ya kwanza wanayoipata ni ile wanayotakiwa na *TRA* kulipa tofauti ya kodi/ushuru wa gari hiyo zaidi ya ushuru aliolipa Zanzibar. Lakini baya zaidi ni pale *TRA* wanapopiga marufuku kwa gari zilizosajiliwa Zanzibar kutembea katika barabara za Tanzania Bara bila ya kununua kibali maalumu, kana kwamba Zanzibar na Tanzania Bara ni nchi mbili tofauti.

Mheshimiwa Spika, hii nayo ni kero kubwa na ambayo inawadhalilisha wananchi ndani ya nchi yao. Mara kadhaa tumekuwa tukiarifiwa Bungeni kwamba hapana hoja kwa gari zilizosajiliwa Zanzibar kununua kibali ndio ziweze kutembea katika barabara za Tanzania Bara. Agizo linalotolewa ni kwamba gari hizo zibadilishwe namba ili ziingie katika mfumo wa namba mpya zinazotumika Tanzania Bara. Ni vyema basi utaratibu ukaandaliwa kwa gari kama hizo kuwekewa muda maalumu ili ziwe zimebadilishwa namba na kwa hivyo pasiwe na pingamizi ya kutembea barabarani ikiwa muda uliowekwa haujamalizika.

Mheshimiwa Spika, vingenevyo utaratibu uandaliwe ofisi za *TRA* zilizoko Zanzibar zipewe jukumu la kutoa namba zinazotumika Tanzania Bara pale ambapo mwananchi anapotaka kusafirisha gari lake lililosajiliwa Zanzibar kulileta Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba kero hizi zitakapopatiwa ufumbuzi wa kudumu wafanyabiashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara pamoja na wananchi wengine kwa ujumla watafanya shughuli zao bila usumbufu wowote. Bila ya kutatua matatizo haya haraka iwezekanavyo tutabaki kuwa na kero nyingi ambazo zinaukwaza na kuathiri Muungano wetu.

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono kwa asilimia mia moja. Bajeti ya mwaka 2007/2008 inaonesha dhahiri ni ya Serikali ya kuendelea kujenga Taifa imara na kuongeza uwezo wa kujitegemea.

Bajeti ya mwaka 2007/2008 inalenga kukusanya mapato ya ndani hadi wastani wa asilimia 18 ya Pato la Taifa kwa mwenendo wa Mapato ya mwaka 2006/2007, tuna uhakika wa kuweza kukusanya asilimia 18 ya Pato la Taifa.

Aidha, ushuru wa bidhaa umeongezwa kwa kuzingatia sheria ya ushuru wa bidhaa na mwenendo wa mfumuko wa bei, jambo ambalo ni sahihi na linaendana na hali halisi ya uthumi.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wetu wa kuongeza ushuru wa barabara kwenye mafuta uko sahihi na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika zina mwelekeo huo kwa lengo la kujenga na kukarabati barabara. Kwa mfano, Uganda, katika Bajeti ya mwaka 2007/2008 ushuru wa mafuta ya petroli kwa lita umepandishwa kutoka shilingi za Kitanzania 470/= hadi 555/= ambayo sehemu yake itaenda kwenye matengenezo ya barabara wakati sisi mapendelekezo yetu ya ushuru wa petroli na ushuru wa barabara jumla yake ni shilingi 537/=. Ukizingatia ukubwa wa nchi yetu bado kiwango kinachopendekezwa kiko chini.

Mheshimiwa Spika, unapotengeneza barabara unasaidia kupunguza gharama za usafirishaji, unapunguza gharama za utunzaji na uendeshaji wa magari kwa maana ya vipuri, matairi, muda na wingi wa mafuta. Nyongeza ya mafuta kwa ajili ya kutengeneza barabara kwa upande mwingine ni faida kwa wenyewe mabasi ya abiria, magari ya mizigo hivyo hawastahili kuongeza nauli na gharama za usafirishaji. Changamoto tuliyonayo ni kuongeza kasi ya kuwadhibiti wasafirishaji na wauza mafuta ili wasiumize wananchi kwa kisingizio cha Serikali kuongeza ushuru kidogo kwa nia ya kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote mbili.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kongwa wanalamikia sana sarafu zisizofaa hasa za Sh. 100/= nyingi ni mbaya na hazifai. Tuchapishe za *Silver*, hizo ni bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wamelalamikia sana mambo mawili. Moja, bei ndogo kwa mazao yote ya kilimo pia mifugo yao yaani kipato kidogo. Pili, bei kubwa mno ya vifaa vyta viwandani kama sementi, mabati, sukari, mafuta na kadhalika. Ni kilio kikubwa kuhusiana na hali ya maisha kuwa ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. (*Makofî*)

**MHE. ALI AMEIR MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Waziri wa Fedha kwa hotuba yake na kazi nzuri anayofanya katika kuongoza Wizara ya Fedha. Mchango wangu unahuusu mambo yafuatayo:-

Moja, naipongeza Bajeti kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Mwaka huu ukizingatiwa katika Bajeti zote zijazo kweli maisha bora yatapatikana kwa Watanzania walio wengi kama sio wote. Jambo muhimu ni kuwasimamia watendaji katika Serikali ili wasikwamishe utekelezaji wa malengo ya Bajeti.

Pili, nami naungana na Waheshimiwa Wabunge walioonyesha wasiwasi kuhusu kupanda kwa kodi ya mafuta hasa ya taa. Kodi hii itawaathiri wananchi kila mahali Tanzania na watakaoathirika zaidi ni watu wa kipato cha chini. Kupanda kwa kodi ya mafuta ya taa pia kutaleta athari kwa mazingira kwa sababu wananchi watalazimika kutafuta nishati ya kuni kukwepa bei kubwa ya mafuta.

Tatu, mgao wa fedha kwa Serikali ya Mapinduzi, hili ni suala lingine ambalo naomba nitoe mawazo yangu, nayo ni kutilia mkazo haja ya kuharakisha kupata ufumbuzi wa suala hili kwa vile Tume ya Pamoja ilikwishawasilisha ripoti yake. Je, ni kitu gani kinachochelewesha maamuzi? Kwa nini mambo ambayo ni kero za Muungano hayashughulikiwi kwa *speed* mpya?

Mheshimiwa Spika, mimi namwomba Waziri atakapokuwa anatoa majumuisho aleze zaidi kuhusu suala hili. Yale maelezo yaliyomo katika hotuba yake ukurasa wa 47

hayatoshi. Tunataka kuelewa Tume ya Pamoja imependekeza nini na ni lini mgao mpya utanza. Mgao wa asilimia 4.5 ni wazi umepitwa na wakati kwa kigezo chochote.

Hoja yangu ya nne ni kuipongeza Wizara kwa nia yake ya kurasimisha ndani ya sheria ya ushuru wa bidhaa, utaratibu wa kurejeshwa SMZ makusanyo ya ushuru kwa bidhaa zilizozalishwa Bara na kuuzwa au kutumika Zanzibar. Nia hii inatekeleza moyo wa ushirikiano ambapo uchumi mkubwa lazima usaidie uchumi mdogo.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kumpongeza sana Waziri wa Fedha na naunga mkono hoja hii.

**MHE. ALI JUMA HAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwa pamoja na watendaji wao kwa kazi kubwa na nzuri walioifanya katika kuandaa hotuba hizi kwa ufanisi na umahiri ulio mkubwa.

Pili, nami naungana na wenzangu waliotangulia kwa kuwapongeza wachezaji wetu wa Timu ya Taifa pamoja na makocha wao kwa ushindi waliotuletea Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naungana na wenzangu kwa kutoa mkono wa pole kwa watu wote waliofiwa na ndugu na jamaa zao kwa ajali ya basi huko Singida na nawaombea marehemu wote Mungu awalaze mahali pema Peponi, *Amin!*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa niende kwenye mchango wangu. Kwanza, niipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kujiondoa katika ukopaji kwenye mabenki yetu (*Treasury bill*).

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo zuri sana kwani litasababisha Benki zetu kubakiwa na fedha nyingi jambo ambalo litapelekea wananchi wapate nafasi nzuri ya kuweza kukopa na kuweza kujidesha kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa jambo la msingi ni kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kusimamia na kuhakikisha mabenki yetu yanapunguza kiwango cha riba ili wananchi wetu waweze kukopa na kujidesha kimiradi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotoka kuzungumzia katika hotuba hii ni kuhusu gawio la asilimia 4.5 ambalo hupatiwa Serikali ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, invyoeweka *formula* hii ya asilimia 4.5 ni ya muda ambayo ilikubaliwa toka mwaka 1994 kati ya Serikali ya Muungano na ile ya Zanzibar katika mambo yafuatayo: Moja, faida ya kila mwaka inayotokana na *BoT* na pili, fedha za misaada ya wafadhili kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, ingawa utekelezaji wa *formula* hii ulianza toka mwaka 1995, lakini Mheshimiwa Waziri aelewé kwamba *formula* hii ni ya muda. Sasa jambo

la kushangaza na la kuumiza kwa upande wa Zanzibar ni kuona kwamba mwaka huo wa 1995 hadi leo hii bado tunatumia *formula* hiyo ya muda tu! Sijui mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, kama tunavyoolewa mwaka 1996 ilipitishwa sheria ya kuunda Tume ya Pamoja ya Fedha (*JFC*) na kuanza kazi mwaka 2003 na mwaka 2006 Tume hiyo ilipeleka mapendekezo yake kwa Serikali zote mbili (SMT na SMZ), lakini la kushangaza hadi leo hii Serikali zetu zimekuwa na kigugumizi cha kutoa maamuzi kama wamekubaliana na mapendekezo ya Tume au hapana. Hivyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha wa Serikali ya Muungano na wa Zanzibar wakae na kuharakisha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, sasa nigosie suala la wafanyabiashara ambao wameonekana kuaminika kwa kulipa kodi kwamba mizigo/makontena yao yasikaguliwe badala yake yapitishwe moja kwa moja. Hili ni jambo moja baya sana na la hatari kwani kufanya hivyo ni kutoa mwanya kwa wafanyabiashara hao kuweza kutumia vibaya mwanya huo ama hata kutumiwa na wafanyabiashara wengine kuperisha biashara zao na pengine zisiwe biashara halali.

Mheshimiwa Spika, mfanyakibashara anayeaminika anaweza kufanya biashara ndani kwa ndani kwa kupewa kitu kidogo na wengine ili awapitishie mizigo yao na huku akiachia Serikali kukosa mapato.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Spika, la kwanza, natoa pongezi kwa Mawaziri wote wawili kwa hotuba nzuri ambazo zimezingatia mambo mengi ambayo ni pamoja na hali halisi ya uchumi wetu.

Pili, mfumuko wa bei, pamoja na tatizo la ukame, udhibiti dhaifu wa Benki Kuu kwenye masuala ya riba, *exchange rate* na urari kati ya manunuzi toka nchi za nje na uuza (exports) nchi za nje, vimeeachangia sana kwenye mfumuko wa bei, biashara huria imegeuka kuwa holela pale watu wanaporuhusiwa kuingiza bidhaa ambazo mbadala wake unaweza kupatikana hapa hapa nchini. Aidha, Benki Kuu haijachukua hatua za kuhakikisha kwamba fedha ya ndani yaani shilingi inatumika kama *legal tender* kwa mujibu wa sheria badala ya dola ya Marekani. Pia siyo dhambi kwa Benki Kuu kutumia *Interest rates* katika kurekebisha *exchange rates* na hali ya fedha kiujumla pamoja na majukumu yetu katika dhana hizi za utandawazi.

Tatu, kuongeza kasi ya ujenzi wa Makao Makuu ya Serikali Dodoma. Moja, jukumu hili muhimu na ambalo limo katika Ilani ya Uchaguzi limepuuzwa kabisa!

Pili, matarajio yetu ni kwamba angalau Serikali ingetoa ratiba ya muda mfupi na ya muda mrefu inayoweka bayana ni lini Wizara na Idara mbalimbali zingehamia Dodoma. Badala yake Serikali imetenga fedha nyingi za kuimarisha ujenzi wa Wizara mbalimbali Dar es Salaam.

Tatu, wakati wa Kikao cha Bajeti cha mwaka jana, Waziri wa Fedha alitoa ahadi kwa maandishi kwamba alikuwa anafanya juhudini ya kupata fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa barabara za Dodoma Mjini kutoka Benki ya *BADEA*.

Mheshimiwa Spika, barabara za Dodoma zinatia aibu na ni fedheha kwa viongozi wote na maendeleo yake yamedumazwa kwa muda mrefu kutokana na *CDA* kutotimiza majukumu iliyoyachukua kutoka Manispaa. Ninaomba tamko kutoka kwa Waziri kuhusu hatma ya juhudini zake hizo.

Nne, fidia kwa wananchi wanaopisha ujenzi wa viwanja vya ndege. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha athibitishe tamko la Waziri Mkuu la tarehe 7 Juni, 2007 alipokutana na Kamati ya Miundombinu kwamba fedha za kuwafidia wananchi wa Msalato watakaopisha ujenzi wa kiwanja cha ndege zimetengwa katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza Mawaziri na Manaibu wao kwa maandalizi mazuri ya Bajeti na uwasilishaji mzuri.

Pili, leseni za magari hatua ni sahihi. Lazima mwenye gari achangie matengenezo ya barabara. Tuchangie ili misaada iwe ni nyongeza tu ila kiwango cha magari makubwa kiongezwe.

Tatu, mafuta, hatua hii ni muafaka, lazima tuchangie. Tusipofanya hivyo hizi barabara azijenge nani? Shilingi 100 siyo nyingi. Nne, tunaomba makusanyo haya yadhibitiwe na yaonekane yatakachofanya. Hilo litakuwa jibu. Naunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wa Wizara hizi mbili kwa hotuba zao nzuri zenye kuleta matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji katika ukurasa wa 41 na 57, Wizara imeainisha mpango wa mwaka 2007/2008 unaolenga kuweka mkazo kwenye mambo yafuatayo:-

Moja, kuimarisha maendeleo ya viwanda vidogo na vya kati (*SMEs*) na kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa kwa kusindika bidhaa za kilimo. Kuvutia uwekezaji katika sekta za uzalishaji, kuongeza upatikanaji wa soko na kuboresha teknolojia za *biogas* na mionzi ya jua, kuimarisha taasisi za maendeleo zinazojihusisha na utafiti, kutoa mafunzo ya ujasiriamali, kutekeleza programu ya MKUKUTA na sheria ya ushindani.

Mheshimiwa Spika, kwa haya mambo matano nianze na namba moja. Serikali iamue kwa dhati kuipatia uwezo *SIDO* ili kuipatia uwezo pia wadau wanaojihusisha na viwanda vidogo na vya kati kwa                       kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa kwa kusindika bidhaa za kilimo kama:-

(a) Mazao ya zabibu ambayo yana soko kubwa sana na zabibu zetu za Dodoma zinazopendwa sana katika soko la Marekani na Afrika Kusini.

(b) Matunda kama maembe, machungwa, mananasi, matikiti maji, mapera na kadhalika, yanaharibika sana kwa kukosa soko na pia *packaging* ni tatizo kubwa sana. Uamuzi huu uende kwa kasi kubwa.

(c) Mazao kama korosho, chai, kahawa, karanga, *chips* za mihogo, viazi, tambi za ngano na kadhalika zitangazwe dunia nzima hasa katika hoteli kubwa duniani, mashirika ya ndege na *supermarket* za nchi za Afrika na Ulaya.

(d) Watalaan wajenge uzalendo katika mioyo kwa kufanya kazi kwa kujituma na kutoa mchango kwa wananchi ili waondokane na umaskini na kuwaelimisha ili waweze kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, kuibua vyanzo vipyta vya mapato, watendaji wawe wabunifu wa kuanzisha vyanzo vya mapato, hatuwezi kila mwaka kuwa na vyanzo ni vile vile. Watu wa Mipango waangalie maeneo ya utalii, mifugo, madini na mazao ya kilimo.

Kuhusu uwekezaji katika sekta ya uzalishaji, kuongeza upatikanaji wa soko na kuboresha teknolojia za *biogas* na mionzi ya jua, suala hili limekuwa likiongelewa mara nyingi lakini ni jambo la msingi na busara sana iwapo utekelezaji wa kupatikana kwa *biogas* na mionzi ya jua utakwenda kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, katika nchi ya China asilimia kubwa ya wananchi wanatumia mionzi ya jua kwa ajili ya nishati za majumbani na taa za barabarani. Nashauri wanamipango wawe wepesi kwa kuiga mazuri yanayofanyika katika nchi za wenzetu.

Kuhusu suala la kuimarisha taasisi za maendeleo ya utafiti, hili ni jambo la msingi na litiliwe mkazo mahsus. Mafunzo ya ujasiriamali naomba Shirika la Viwanda Vidogo lenye dhamana ya kuwasimamia na kuwafunza wajasiriamali wetu iwasimamie ili mazao yao yauzwe ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Wizara idhibiti matumizi ya dola za Kimarekani kutumika nchini badala yake shilingi ndiyo itumike na iwekwe kisheria.

Mheshimiwa Spika, mahoteli yote ya kitalii hupokea *USD* na pia *bill* huletwia kwa gharama za dola za Kimarekani. Lakini ukienda Kenya tu huwezi kutumia *USD* ukapata huduma yoyote. Kwenye maduka ya kuuzia fedha za kigeni bila hata ya kuulizwa *passport*. Hali hii sio nzuri kwa uchumi wa nchi yetu. Tujaribu kurekebisha mapungufu hayo.

Mheshimiwa Spika, narudia kuwapongeza tena Mawaziri hawa pia naomba kuunga mkono hotuba zote mbili kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ikaondoa kabisa ushuru kwa mafuta ya taa kwa kuwa unagusa moja kwa moja wananchi wa kipato cha chini.

Pili, mishahara na posho kwa walimu iangaliwe upya kwa kuwa ni watu amba wana kazi kubwa sana ya kuwaandaa watoto ambaa ndio wazee na viongozi wa kesho.

Tatu, Serikali iangalie upya riba ya asilimia 10 kwa mkopo wa JK kwani kima hicho ni kikubwa kwa wajasiriamali wa kipato cha chini.

Nne, Serikali izidishe mikakati ya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI na homa ya Malaria kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na kutuwezesha kufika hapa leo hii. Pia nampongeza Waziri wa Fedha kwa hotuba yake nzuri na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii lakini nina mapendekezo yafuatayo: kwanza, elimu ipewe kipaumbele hasa hasa elimu ya juu. Tukiangalia katika sekta ya elimu kwa sababu ndiko wanakotoka Marais, Madaktari, Majaji na viongozi wote pamoja na nyie mliomo humu ndani, hivyo basi elimu ipewe kipaumbele tena asilimia 100 na walimu waboreshewe mishahara yao kwani wanapewa posho si mshahara.

Pili, ni kuhusu utalii. Kulingana na Bajeti ya mwaka 2006/2007 uliongozwa zaidi katika Sekta ya Utalii iliongoza zaidi. Hivyo basi ipo haja ya kupewa kipaumbele sekta hii kwa kuboresha sehemu mbalimbali za utalii mfano, misitu ihifadhiwe zaidi wala isikatwe ovyo ovyo kwani ni kivutio kwa wageni, vile vile wanyama wa asili walindwe kwa kuepusha uwindaji haramu. Pia itolewe elimu zaidi kwa wale wanaopokea wageni na kuwatemeza (*tour guide*) ili kupunguza uporaji wa mali holela.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kilimo, napenda kuchangia kidogo katika sekta ya kilimo. Kilimo kipewe kipaumbele kwani vijana wengi siku hizi wanawenza kujajiri wenyewe kuptitia sekta hii. Vile vile tunaweza kupata bidhaa mbalimbali mfano, dawa, viungo mbalimbali na vyakula kwani kilimo au jembe halimtupi mtu. Hivyo basi kilimo kipewe kipaumbele na kiweze kufikiriwa kwa undani. Kwa kutoa elimu kwa wakulima na vifaa mbalimbali vya kilimo kwani kuna msemo usemao: “*A country without a farmer is like a bus without passengers.*”

Kuhusu ushuru, kulingana na Bajeti ya fedha kusamehe ushuru wa forodha kwenye vifaa vya hospitali zilizosajiliwa ningependa kushauri kwamba tusiwasemehe bali watozwe angalau kidogo ili kuchangia mfuko huo kwani wananchi wanapokwenda hospitali hutozwa fedha, mfano, kufungua faili la mzazi tu ni shilingi mia tano hivyo basi nao ni vizuri kuchangia ili kuboresha matibabu ya wagonjwa na wasiojiweza.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Magogoni naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani kwenu kwa kupanga makadirio ya fedha. Kwanza katika Mipango ya Bajeti hii ni mambo au miradi mingi ya mwaka 2006/2007 ambayo bado hajatekelezeka. Mfano, uwanja wa ndege wa Bukoba kuwekewa uzio. Kwa kuwa uzio huo haujawekwa je, pesa ya uzio huo iko wapi au zilifanya kazi gani? Pia katika mipango naona kuna pesa kama *TASAF* haziingii kwenye Bajeti na zinatumika katika maendeleo kwa mpango huu, Wizara haioni kama ni muhimu sasa pesa zote zipite katika Bajeti na ndipo zitumike?

Katika hotuba ya Wizara ya Fedha, mimi tatizo ninaloona ni pale mafuta yalipoongezwa kodi, hii ni hali ya utata, kwani asilimia kubwa ya Watanzania wanaishi vijijini, ambako hakuna umeme na hata wale wanaishi mijini umeme haukamatiki kwa gharama. Watu wengi wanashindwa kumudu gharama hizo, hivyo, haipendezi wala haileti mantiki nzuri kuongeza kodi za mafuta. Tunaiomba Serikali iliangalie hilo.

Pili, katika kupitisha makontena kwa milango ya kijani na milango miekundu. Hii ni hatari sana kwani wafanyabiashara wengi wa Tanzania si waadilifu. Katika bandari yetu kuna makampuni mengi yanayoshughulikia makontena, sasa basi ni kwa nini wanashindwa kufanya kazi zao kwa wakati?

Mimi sikubaliani na hilo la kutoa kontena kwa wafanyabiashara wakubwa bila kukaguliwa, kwani wao ndio wenzao, huwa wanafanya mambo yasiyoliingizia Taifa faida, kwa kuwa hutaka faidi kubwa. Pia mimi binafsi sioni pale bandarini *TISCAN* wana faida gani? Kama wao wakitoa hesabu ya ushuru, *TRA* wanatengua hesabu hiyo na wao kutoa hesabu nytingine. Sasa basi kwa nini *TRA* wasifanye kazi hiyo na huko bandarini. Naiomba Serikali iianglie kuwepo hapo kwa Kampuni hiyo ambayo tunailipa pesa nytingi, kwa nini kazi hiyo isifanywe na *TRA* ili pesa hizo zikaingia katika pato la Serikali? Ahsante.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kupata fursa ya kuchangia hoja zilizotajwa hapo juu. Kwanza, nawapongeza sana Waziri wa Mipango, Uchumi na Uvezeshaji Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa na Mheshimiwa Zakia Meghji.

Maelezo haya ni ya ziada kwa mchango nilioutoa kwa kuzungumza Bungeni tarehe 20 Juni, 2007.

Kuhusu udhibiti wa matumizi ya fedha za Serikali Kuu na za Halmashauri, naishauri Serikali iwe makini sana kuwateua maafisa wengi katika Idara ya *Expenditure Tracking Unit*, wenye uadilifu mkubwa na makini ili kuepusha kurubuniwa au kudanganywa na watendaji wasio makini kutumia fedha za Serikali kwa malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia Wabunge wajulishwe kipindi ambapo maafisa wa *Expenditure Tracking Unit*, ingawa si kwa lengo la kushirikishwa, lakini, ni muhimu Serikali ihakikishe ripoti zao katika Wilaya/Jimbo husika zinawafikia mapema Wabunge wa maeneo hayo. Hii itasaidia sana Wabunge kuhakiki taarifa zilizotolewa na kuwawezesha kutoa hali halisi ilivyo katika maeneo husika vijiji kwenye *site* ya miradi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali inapotoa taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya Kitaifa iliyoahidiwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, ingewekewa *chapter* maalumu mara mbili kwa mwaka na kutolewa taarifa Bungeni. Miradi hii ni kama vile idadi ya ajira zilizofikiwa hadi sasa, idadi ya asilimia ya upatikanaji maji vijiji na mijini, idadi ya kilomita za barabara za lami iliyofikiwa hadi kipindi husika na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lengo la ripoti *in summary* ya aina hii kwa kifupi itasaidia kuwaelimisha Wabunge na wananchi kutambua kwamba shughuli za miradi hiyo kwa nchi nzima zinaendelea, tofauti na kila Mbunge kujali ufahamu wa eneo lake peke yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. NURU AWADH BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alitoa shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa ili kuwawezesha wananchi walio na kipato duni kujikwamua katika hali mbaya ya maisha.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililojiteza fedha hizi hazikuwafikia walengwa ambaio ni wajasiriamali wadogo wadogo, badala yake wengi waliopata fedha hizo ni wale wenye uwezo wa kipato. Hii ni sawa na ile methali isemayo: “Aliyenacho ndiye aongezwaye.”

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa limejiteza katika hatua za awali za kuombea mikopo hiyo, inaelekea wananchi wanakatishwa tamaa na viongozi wa ngazi za chini sehemu ambazo mikopo inaanzia kuombwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia pia kuhusu suala la ukaguzi wa mizigo inayoingia katika bandari yetu ya Dar es Salaam. Hii iangaliwe sana, kwa kuwaruhusu wafanyabiashara maarufu walipao kodi vizuri kutokaguliwa mizigo yao kuna athari zifuatazo:-

- (i) Kupitisha vitu hatari kama silaha.
- (ii) Kupitisha dawa za kulevyaa na ikawa ndio chanzo cha waathirika wa dawa za kulevyaa kuongezeka na kukosa nguvu kazi ya vijana ambaio ndio tegemea kubwa la Taifa letu.

(iii) Chanzo cha wao nao kuanzisha biashara ndani ya biashara. Hii wanaweza kutumiwa na wafanyabiashara wenzao ambao hawana sifa zinazotakiwa na kuwabebea mizigo yao na malipo yakiwaendea hao wafanyabiashara wakubwa wenyе sifa zitakiwazo.

Mheshimiwa Spika, hii pia itasababisha kulikosesha Taifa faida/kipato ambacho kitazidi kuididimiza nchi kutohana na kushuka kwa uchumi.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Spika, narejea niliyoyaeleza Bungeni, siamini kwamba hata kama tukifanya mabadiliko yote yaliyopendekezwa na Jumuiya ya Taasisi za Fedha nchini taasisi hizi zitajikita kwa nguvu inayotegemewa kwenye sekta hii ya *mortgage finance*.

Taasisi hizi zimezoea kutengeneza faida kilaini na *mortgage finance* ni kazi ya kutoa jasho na ya muda mrefu. Kinachohitajika ni msukumo wa makusudi wenyе nguvu za kisheria kama ilivyo katika nchi nyingine. Waziri atukuwa tayari kutunga sheria ndogo itakayoelekeza taasisi hizi zitumie angalau asilimia 10 kwa mwaka kuwa *mortgage finance* (mikopo ya miaka 20 na zaidi)? Kama hatayaweza basi watakiwe *ku-deposit* asilimia hiyo 10 *BoT* ili izipeleke fedha hizo kwenye taasisi zenye uwezo wa kuzitumia kwa ajili ya *mortgage finance*. Kama taasisi hizi zitahitaji vivutio Serikali isisite kutoa vivutio vinavyostahili.

Kuhusu sheria ya *Condominium and Sectional Properties Act*, hii sio hoja ya *Tanzania Bankers Association* ni hoja yetu sote. Wote tulikuwa tunajua sheria hii inahitajika. Serikali iharakishe kuleta Muswada huu katika Bunge lijalo kwenye *Fast Track* ili tuonekane tunashughulikia jambo hili kwa kasi na nguvu.

Pia, naipongeza na kuishukuru Serikali na hasa Waziri Mkuu kwa kutuhakikishia kwamba Serikali inatambua umuhimu wa Kiwanda cha *General Tyre*, Arusha kwenye uchumi wetu.

Serikali imeshughulikia matatizo ya *General Tyre* kwa mtazamo wa kukisaidia kisisitishe uzalishaji. Tunaomba kama tulivyoahidiwa *guarantee* ya mkopo unaotakiwa iharakishwe kutolewa ili uzalishaji uendelee. Mashamba ya Muheza, Kilombero na Zanzibar ya *Rubber* uwezekano uangaliwe ili mashamba hayo yawe sehemu ya mkakati wa makusudi wa kuendeleza uzalishaji wa *rubber* kwa ajili ya matumizi ya kiwanda chetu cha *General Tyre*, Arusha na *for export*.

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja.

Kulingana na Bajeti hii ambayo ni ya pili kwa Serikali ya Awamu ya Nne, Bajeti ambayo inatoa mwamko mpya katika nchi za Kiafrika maana ya kuondokana na Bajeti tegemezi.

Pamoja na mazuri hayo tuangalie sana vyanzo vya mapato katika nchi kutoruhusu ukwepaji wa kodi, kuangalia sana mikataba ambayo inatoa mianya ya kutolipa kodi. Lakini pia kuhusu suala la mafuta napenda kutoa maoni kuwa katika Bajeti iliyopita

Serikali ilisamehe kodi katika mafuta. Nadhani kwa muono wangu hakuna shida ila Serikali ndio ina shida kwa sababu walipoondo *VAT* bado bei za mafuta hazikushuka na Serikali ilikuwa kimya.

Je, sasa inapoongeza kodi hawaoni kuwa wafanyabiashara hawataruhusiwa kuongeza bei za mafuta? Hilo ndilo litakalokuwa la maana zaidi ili kuwa na tija na kutowakandamiza wananchi zaidi katika ununuzi wa mafuta maana walishaondolewa kodi, bei hazikupungua na je, wakiongezewa bei wataongeza?

Mheshimiwa Spika, Serikali iwe makini kwa hili kwa sababu lazima Serikali iseme wazi kwa wananchi wanatakiwa wanunue mafuta hayo kwa kiasi gani ili wananchi watambue hivyo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TRC* napenda kuwapongeza watendaji. Kwa kutenga 49% na katika Shirika hili Serikali kuwa na mkono wake humo na hayo ndio maendeleo ya wananchi katika nchi yao. Napongeza sana kwa hili la vyombo vyaa usafiri kuwa ndani ya mikono ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu kwa kupata nafasi ya kuchangia katika hotuba hii. Awali ya yote napenda kuipongeza Timu ya *Taifa Stars* kwa ushindi iliyoupata. Vile vile napenda kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji na Naibu Mawaziri pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchangia kuhusu ongezeko la kodi katika mafuta. Nitaanza na mafuta ya taa, ukizingatia hasa kule vijijini, kwa sasa Taifa tunapiga kelele kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi mafuta ya taa yalivyoongezewa kodi, kwa hakika wananchi walio vijijini watarudi kukata miti kwa ajili ya matumizi ya kupikia. Ningeshauri kodi hii iliyopanda ifutwe kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupanda kwa kodi ya mafuta ya petroli, itaathiri kila mmoja wetu. Bei ya kila kitu itapanda juu na huku Serikali inasisitiza tupate maisha bora kwa kila mtanzania. Wakulima waliopo vijijini watasafirishaje mazao yao? Petroli ipande, kodi ya magari ipande! Nafikiri gari zenye *1500cc – 2500cc* ndizo zitozwe shilingi 80,000.

Mheshimiwa Spika, kupanda kwa mafuta ya magari, ningeshauri kudhibiti upandaji wa bei. Serikali iimarishe Shirika la *TPDC* waagize mafuta na pale *TIPPER* pafanye kazi, wahifadhi pale na *TPDC* wawapangie bei ya kuuza.

Kuhusu kuperomoka kwa shilingi ya Tanzania, kwenye sekta ya utalii, Serikali inapoteza fedha nyingi. Watalii wote wanaoingia nchini, malipo yao yote yafanywe kwa *local currency* na siyo dola. Hii itapandisha hadhi *currency* yetu. Mbona nchi nyingine

duniani wanatoza kwa kutumia *currency* iliyopo? Hapa nchini hoteli, *Park Fees hata licence* kwa *local tour oparetion* zinalipwa kwa *US dollars*. Naomba majibu, ni kwa nini tunatoza vitu hivi kwa kutumia *currency* za kigeni hasa *US dollar*?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri wa Fedha imesisitiza mikakati ya kukusanya kodi, lakini mimi nitapinga huu mkakati wa kuondoa vitu bandarini kwa kupitia *fast tracking* bila ukaguzi kwa vitu vinavyoagizwa na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, huu unaweza kuwa ndio mwanzo mkubwa wa kutopata kodi na mwanya wa kupitisha kila aina ya vitu viovu kama dawa za kulevya na kadhalika. Nafikiri njia nzuri ni lazima vitu vyote vikaguliwe na ushuru ulipwe ipasavyo. Kuna vitu vingi tu vya ku-*check* mizigo bila kufungua kwa kutumia teknolojia za kisasa. Ukifuata utaratibu wa kupitisha bila ku-*check*, hata silaha haramu zinaweza kupata njia ya kupitishia.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia na kutia msisitizo, Serikali iongeze fedha kwenye Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ukitegemea Watanzania asilimia kubwa wanategemea kilimo (80%). Hivyo, fedha ikitolewa ya kutosha, pembejeo ziwe kwa bei nafuu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Serikali iangalie ni jinsi gani ya kuikuza Tanzania kiutalii kwa sababu wenzetu wa nchi jirani wanauzu Mlima Kilimanjaro, Ngorongoro, Serengeti kwa kusema; “*Come and visit these places in East Africa.*” Mfano; “*Club Kili in East Africa.*”

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie mikakati ya wageni kuja moja kwa moja Tanzania na hii itatuongezea mapato mengi ya kigeni.

Mheshimiwa Spika, ushauri, ndege ya *Virgin Atlantic* ambayo ni ndege ya bei rahisi imeanza kutua Nairobi. Serikali ijaribu kutafuta aina ya ndege za Mashirika ya bei nafuu zije nchini Tanzania na wageni watakuja moja kwa moja Tanzania badala ya kupitia Kenya au *South Africa*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha.

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, bado ningependa kutoa ushauri kama ifutavyo:-

Bajeti yoyote ile lengo lake ni kuwapunguzia ugumu wa maisha wananchi wake hasa wananchi wa hali ya chini na wa kawaida ambaao ni wakulima na wafanyabisahara wadogo wadogo. Pamoja na kazi nzuri iliyofanyika, lakini upo upungufu ambaao unamgusa karibu kila Mtanzania katika maisha ya kila siku.

Nionavyo mimi katika kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi wetu hasa walioko vijijini ambaao ndio walio wengi na ndio wanaozalisha zaidi katika Pato la Taifa,

nilitegemea Serikali ingepunguza bei ya mafuta ya dizeli na mafuta ya taa. Mafuta ya dizeli ni nyenzo muhimu sana, kwa mfano, tunasema tuboreshe kilimo cha Watanzania na kilimo bora ni kile ambacho hutumia zana za kisasa kama trekta na zana zingine ambazo hutumia mafuta ambayo ni dizeli. Kama bei ya mafuta haya iko juu, je, wananchi hawa watawezaje kuendeleza kilimo kwa kiasi cha kutosha?

Mheshimiwa Spika, dizeli ndiyo ambayo hutumika kwenye vyombo kama mabasi, malaria na vyombo vya baharini. Hivyo basi, nauli hupanda na kupanda huko kunasababisha na kupanda kwa bei ya vitu vyote ambavyo husafirishwa na vyombo hivyo na hatimaye bei ya vyakula, vifaa vya ujenzi, mavazi na kodi za nyumba hupanda na kuongeza mzigoto kwa wananchi walio wengi amba ni zaidi ya asilimia themanini.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kabisa kwamba Bajeti yetu ni ndogo (hatuna uwezo), lakini zipo bidhaa ambazo zinaweza kuziba pengo la mafuta ili kufidia upungufu unaotokana na mafuta, kwa mfano, sigara, pombe za aina mbalimbali, vinywaji baridi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hicho ni kilio cha wananchi walio wengi, naomba tuzingatie na kuangalia kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, kama ni lazima kupandisha bei ya mafuta, basi ibakie kwenye mafuta ya petroli badala ya dizeli.

Mheshimiwa Spika, saa naomba nizungumzie bei ya mafuta ya taa. Mafuta ya taa ni nyenzo muhimu sana kwani wananchi walio wengi hutumia nishati hii kwa vile umeme na gesi bado mtandao wake haujaenea katika sehemu kubwa ya nchi yetu. Hata kama umeme huo ungefika sehemu hizo, bado wananchi walio wengi hawawezi kumudu bei ya umeme na hivyo nishati muhimu kwao ni mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza ni kile kitendo cha kupunguza bei ya mafuta ya ndege (*Jet Oil*). Haya mafuta ya ndege hayawagusi wananchi moja kwa moja kwani ndege tulizo nazo ni chache sana. Je, suala la misingi ni kupunguza mafuta ya ndege badala ya mafuta ya taa? Isiwe ikawa ni ujanja wa watendaji wachache wa kujinufaisha badala ya kuwasaidia walio wengi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni zimetokea ajali nyingi za kulipuka mafuta katika majumba ya watu, hii inanipa wasiwasi, huenda wajanja wakanunua mafuta ya ndege kwa wingi na kuchanganya na mafuta ya taa ili wapate faida kubwa na madhara yake husababisha milipuko na hii hutokea kwa vile mafuta ya ndege ni mepesi zaidi kuliko mafuta ya taa ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba Serikali ipandishe kodi ya mafuta ya ndege na kupunguza kodi katika mafuta ya taa maana tutakuwa tumewasaidia sana wananchi wetu walio wengi na kwa kufanya hivyo tutapunguza ajali za milipuko ya mafuta isiyokuwa ya kawaida. Naomba Serikali isikilize kilio cha walio wengi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kama baba ni vizuri kusikiliza kilio cha watoto wake ambao sisi ndio wawakilishi wa wananchi hao.

**MHE. KIUMBWA MAKAME MBARAKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini pamoja na wananchi wote wa Mkao huo, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kwanza, niwapongeze Mawaziri wote waliota hotuba hizi mbili kwa jinsi walivyoweza kuziwasilisha vizuri. Pia ninawapongeza watendaji wote wa Wizara walivyoshiriki kwa njia moja ama nyingine jinsi walivyotoa ushirikiano katika kukamilisha Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzuri wa mpango wa makadirio ya fedha uliopo katika hoja hizi mbili na kwa kuwa mengi yameshazungumzwa na wenzangu, mimi nina mchango mdogo tu. Naomba kuchangia suala la wastaafu wa Jumuuya ya Afrika Mashariki iliyovunjika.

Mheshimiwa Spika, wapo wafanyakazi wengi waliofanya kazi katika Jumuuya hiyo na leo hii hawajalipwa fedha zao za mafao kwa muda mrefu na kuleta usumbufu mkubwa katika kufuutilia mafao hayo hasa wale wanaoishi Zanzibar kuja na kurudi Dar es Salaam mara kwa mara bila mafanikio.

Wakati mwingine wanaambiwa mafaili yao hayaonekani na kipindi kimekuwa kirefu sana mpaka wameanza kuchanganyikiwa na kukosa imani. Pia wapo wengine ambao majina yao yametoka magazetini lakini hadi leo hawajapata chochote na walitakiwa kutekeleza taratibu zote zilizostahili.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifanye juhudzi za makusudi ili kulishughulikia tatizo hili ikiwa ni pamoja na kufungua ofisi Zanzibar inayohusiana na masuala haya ili kuweza kufuutilia kwa urahisi zaidi kwa wale walioko Zanzibar, pili, Serikali ifutilie watendaji ambao hupewa majukumu ya kushughulikia haki za wananchi wanaodai mafao yao ili kubainika kwa usumbufu wanaopata wananchi bila mafanikio. Naunga mkono hoja.

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa maandishi mpango wa maendeleo kwa mwaka 2007/2008 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuongeza fedha kwa Wizara ya Miundombinu baada ya Kamati ya Bunge kumuomba Waziri wa Fedha baada ya kuona fedha zilizotengwa hazikidhi kwa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, ili tuongeze mapato zaidi ni muhimu tukaunganisha miundombinu ya nchi yetu kwa kuunganisha barabara za Mkao na Wilaya, hii ndiyo njia mbadala. Pia, kama tunaamini kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wetu, basi tuangalie sana sekta hii, tuboreshe kilimo cha kisasa ili tuuze mazao ndani na nje ya nchi maana uchumi wetu utainuka zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika suala la vyanzo vya utalii, tuboreshe utalii kwa kuangalia zaidi mazao ya misitu. Kuna zao la mbao ambalo jirani zetu Kenya wanachukua Tanzania na kupeleka nje ya nchi yao na kupanua uchumi wao badala ya kutunufaisha sisi wenyewe. Lakini, uvuvi pia na utalii wa ndani, Watanzania wahamasishwe kutembelea sehemu za utalii.

Mheshimiwa Spika, sina tatizo na siku saba kutokana na usumbufu wa *TISCAN* na *TRA*, siku hizo ni kidogo hazitoshelezi, ni kuwaongeza mapato *TISCAN* nao waboreshe ili watu wapate *documents* zao mapema maana itasaidia kuingiza mizigo mingi zaidi na kipato cha Serikali kitaongezeka.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti hii, wananchi wengi wanalamikia kupanda kwa mafuta. Naomba Serikali iangalie upya kwa sababu kupanda kwa mafuta, kila kitu kitapanda na kuwa mzigو mkubwa kwa wananchi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa nianze kutoa rambirambi zangu kwa wafiwa wote pamoja na wananchi wote wa Mkoa wa Singida kwa maafa yaliyotokea kutokana na ajali ya basi la *Mohamed Trans*, tarehe 15 Juni, 2007. Naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshej, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Makatibu Wakuu pamoja na watumishi wote walioshiriki kuandaa Bajeti nzuri pamoja na mwelekeo wa uchumi kwa miaka mitatu ijayo na matokeo ya mwaka 2006. Nawaombea Mungu awape afya njema na nguvu ili waweze kusimamia vyema kwa lengo la kuleta tija kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi napenda kutoa ushauri maeneo kadhaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupanda kwa mafuta ya taa, ni matumaini yangu kuwa kutaathiri watumiaji wa mafuta ya taa ambao ni wananchi wenye kipato kidogo walioko vijijini. Hivyo basi, tutakuwa hatujawasaidia bila kuwapa nishati mbadala kwani watumiaji wa gesi ni wachache sana kwani nayo ni aghali.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali gherama hii ingepelekwa eneo lingine, mfano katika pombe na sigara kwani wananchi wanaotumia pombe au sigara hata wasipotumia hakuna athari yoyote watakayopata tofauti na mafuta ya taa ambayo matumizi yake ni ya lazima hakuna asiyejua hilo.

Mheshimiwa Spika, kupanda kwa dizeli na petroli, naendelea kuisihi Serikali kuwa dizeli na petroli ni muhimu sana kwa Watanzania wote kwani biashara yoyote bila usafiri huwezi ukafanikisha. Mfano, wakulima wa mazao ya biashara wanalima vijijini lakini lazima wasafirishe kwa ajili ya kutafuta soko. Hata mifugo, biashara yake ni lazima usafirishe, mfanyabiashara kusafiri ni lazima.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa dizeli na petroli ikipanda kodi, nauli za abiria na mizigo lazima zitakuwa juu sana. Baya zaidi ni pale Serikali itakaposhindwa kudhibiti mfumuko wa bei za nauli. Naendelea kuiomba Serikali iendelee kuangalia zaidi eneo la kufidia ongezeko la kodi za mafuta.

Mheshimiwa Spika, kushuka kwa uchumi Singida, kupitia ziara ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, imedhihirika wazi kuwa Singida ni ya mwisho kiuchumi. Hii inasikitisha sana kwani natambua kuwa wananchi wa Mkoa wa Singida ni wachapakazi sana.

Naishauri Serikali ifanye utafiti wa kina ili tuweze kuwaeleza wananchi sababu na jitihada za kuinua uchumi kwa mkoa wetu. Kwa maoni yangu ya haraka haraka nadhani hata utoaji wa huduma kwa wananchi kupitia watendaji wetu ni kazi sana kwani huduma ziko mbali na wananchi kwa ukubwa wa vijiji, kata, tarafa, Wilaya na Mkoa pia. Naiomba Serikali itazame upya uwezekano wa kusogeza huduma kwa wananchi kwa kugawa Wilaya zote kwani toka tumepata Uhuru Wilaya hizi hazijagawanywa tena.

Mheshimiwa Spika, Wilaya zote za Mkoa wa Singida ni kubwa sana, watu ni wengi, uwezekano wa kukuza uchumi upo na tayari uongozi wa Wilaya zote na Mkoa umeshajadili kwenye vikao halali vya Wilaya na Mkoa kwa kugawa na kutuma Wizarani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Iramba, Iramba Mashariki - Nduguti, Iramba Magharibi - Kiomboi, Wilaya ya Singida, Singida Kaskazini - Ilongero, Singida Kusini - Ikungi, Singida Manispaa. Wilaya ya Manyoni, Manyoni Mashariki - Manyoni, Manyoni Magharibi - Itigi.

Mheshimiwa Spika, kwa mgao huu, Mkoa wa Singida utakuwa na Wilaya saba badala ya Wilaya tatu. Natambua wazi ufinyu wa Bajeti na waombaji ni wengi, lakini matatizo yanazidiana uzito. Chonde chonde Singida tupewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kuhusu shilingi bilioni moja za Mheshimiwa Rais, napenda kuipongeza Serikali kwa uamuza mzuri wa kuwasaidia wajasiriamali ambao ni wananchi wenye vipato vya chini lakini wana nia ya kuondoa umaskini. Mpango wa Serikali ulikuwa na lengo zuri kabisa kwa wajasiriamali mbalimbali, lakini Benki zilizopewa dhamana hiyo zimeshindwa kuitumia vizuri kwani upatikanaji wa mikopo umekuwa mgumu na mbaya zaidi.

Mheshimiwa Spika, usiri wa wale waliopata ni mkubwa hata Wabunge na viongozi wa Serikali Wilayani na Mikoani imekuwa vigumu kupata takwimu za waliofaulu mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifuutilie kwa karibu kuondoa ukiritimba huu kwani wananchi wengi wameanzisha *SACCOS* ili ziwalettee matunda. Wengi wameanza kukata tamaa ya kuomba mikopo kwa sababu ya usumbufu mkubwa wanaopata yakiwemo masharti magumu. Naomba benki hizi zisimpake matope Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuwa alikuwa na nia njema na thabiti kwa wajasiriamali wenye nia ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gari la Zimamoto Manispaa ya Singida, kumbukumbu zinanipa kuwa niliwahi kuomba fedha za kununulia gari la Zimamoto kwa Manispaa ya Singida baada ya matukio kadhaa ya moto kutokea.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa heshima na mapenzi kwa wana Singida ilitoa fedha hizo kwa awamu mbili yaani shilingi 165,000,000/= na kisha Sh. 200,000,000/= ambapo jumla ilikuwa Sh. 365,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema kuwa wako watendaji wasiojali au kuogopa miiko ya Serikali, hivyo, fedha kiasi cha shilingi 165,000,000/= zilitumika kwa shughuli nyingine. Naiomba Serikali ifuutilie jambo hilo ili watendaji wa aina hii wajulikane.

Aidha, kuhusu ajali ya basi la *Mohamed Trans*, kama tungakuwa na gari za Zimamoto tungeweza kuokoa maisha ya watu hata maiti zingepatikana kuliko tulivyoziwa majivu. Inauma sana hasa mimi na Mkuu wa Mkoa tulioshuhudia tukio hilo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kutamka rasmi kwamba naunga mkono Bajeti hii. Nawatakia utekelezaji mwema.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, Watanzania wamekuwa na imani kubwa na uongozi uliopo madarakani hivi sasa na kujenga matumaini ya kuitoa nchi hii kutoka dimbwi la umaskini, dalili ni wingi wa kura ambazo Chama Tawala kilipata.

Mheshimiwa Spika, kupanga ni kuchagua. Mimi sina matatizo ya Bajeti kwa ujumla na naunga mkono asilimia mia moja na naamini katika dhana nzima ya kuongeza kodi za mafuta na bidhaa nyingine kwa ajili ya kukuza pato la Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba Serikali iangalie tena pendekeso lake la ongezeko la bei ya mafuta ya taa. Hili litaturejesha nyuma miaka ya tisini ambapo sote tu mashahidi, mazingira yanavyoharibika kwa ukataji miti, vyanzo vya maji vinapotea, ukame unazidi. Jitihada zote tulizochukua kuirejesha hali ya mazingira ya nchi itaharibika endapo mafuta ya taa yatakuwa bei juu. Tunaomba kodi hii izingatiwe tena.

Mheshimiwa Spika, sina matatizo na vipaumbele vya Kitaifa kwani kupanga ni kuchagua. Mawazo yangu endapo ningepewa nafasi ya kupendekeza, mimi ningependekeza katika mfumo huu, Elimu, Mawasiliano, Kilimo. Maji na Afya vingefuata baadae na ningetoa asilimia zaidi kama Elimu 20 % badala ya 18%,

Mawasiliano 15% badala ya 12.8%, Kilimo 8.2% badala ya 6.2% na Afya na Maji zikagawana asilimia zilizobaki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu magari kuwa na usajili wa Zanzibar lakini kutumika Bara, nchi hii ni moja ingawa ina Serikali mbili. Maelezo mengi yanetolewa kuhusu hili, lakini hakuna hatua thabiti zinazochukuliwa. Tatizo ni nini? Ni Serikali au watendaji?

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri jambo hili alimalize kwa sababu watendaji wanatekeleza kinyume na maelezo yanayotolewa na Serikali (Mawaziri Bungeni). Naomba Mheshimiwa Waziri aliweke bayana suala hili!

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa majini, si Waziri wa Fedha wala wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji aliyegusia suala hili. Sote ni mashahidi jinsi watu wanavyopoteza maisha yao kwenye bahari na maziwa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri hawakuliweka bayana suala hili. Kwa kweli tunahitaji boti za uokoaji na vile vile kuna haja ya kuangalia mwenendo wa vyombo vyta majini hasa vinavyoishughulisha na kupakia abiria ili kila kimoja kifuate taratibu na sheria zilizopo. Serikali lazima isimamie utekelezaji wa sheria hizo na hapa siyo tu kuwepo kwa sheria hizo bali sheria hizo zitekelezwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi mabaya ya fedha za Halmashauri, pamoja na nia nzuri ya Serikali iliyonayo, kazi kubwa ya Mkuu wa nchi anayofanya ya kutafuta fedha, misaada na kuboresha miundo elekezi ya uchumi, lakini kama watendaji katika Halmashauri hawatadhibitiwa, tunatwanga maji kwenye kinu na hakuna kitakachotendeka. Ahsante na kwa mara nyingine tena naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimezungumza au tuseme nimearifiana na watoa hoja na mpango wa kujibu itakuwa kama ifuatavyo:-

Atatangulia Waziri wa Mipango kwa dakika 40 halafu watafuatia Naibu Mawaziri wa Fedha kwa muda mfupi zaidi na hatimaye Waziri wa Fedha ambaye kwa ujumla pamoja na Manaibu wake ni saa 1:20.

Sasa mwita Mheshimiwa Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii kuhitimisha hoja yangu ya hali ya uchumi wa Taifa letu kwa mwaka 2006 na mwelekeo wa muda wa kati 2007/2008 hadi 2009/2010.

Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba yangu na ile ya Waziri wa Fedha hapa Bungeni. Wapo waliochangia kwa kauli na wapo pia waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Serikali inathamini sana na kuzingatia michango yao yote na itaifanyia kazi kwa makini na kwa haraka ili kuharakisha maendeleo ya Taifa letu.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia moja kwa moja hapa Bungeni ni 83 kwa kauli na waliochangia kwa maandishi ni 56. Hivyo naomba kama ilivyo kawaida yetu niwatambue na ninawatambua hivi kwa niaba ya mwenzangu vilevile kwa sababu hoja nyingi zimeelekezwa kwenye Wizara ya Fedha ili wapate muda wa kutosha wa kujibu hoja, basi mimi nitawataja waliochangia hapa Bungeni.

Waliochangia kwa kauli hapa Bungeni ni Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Balozi Getrude Ibengwe Mongella, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope na Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa. (*Makofii*)

Wengine ni Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mheshimiwa Joyce Nhamanilo Machimu, Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawazwa, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mheshimiwa Dr. Festus Bulugu Limbu, Mheshimiwa Fred Mpandazoe Tungu, Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni, Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo na Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga. (*Makofii*)

Wengine ni Mheshimiwa Aggrey Deaisile Joshua Mwanri, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, Mheshimiwa Elisa David Mollel, Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, Mheshimiwa Balozi Hamis Suedi Kagasheki, Mheshimiwa Felix Christopher Mrema, Mheshimiwa Castor Raphael Ligallama, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah na Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage. (*Makofii*)

Wengine ni Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mheshimiwa Fuya Godwin Kimbita, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Eliatta Namdumpe Switi, Mheshimiwa

Anastazia James Wambura, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe na Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesa. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Richard Said Nyaulawa, Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu, Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mheshimiwa Hadija Saleh Ngozi, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mcemba, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Mwanawetu Said Zarafi na Mheshimiwa Prof. Jumanne Abdallah Maghembe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mcemba, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Dr. Guido Gorogolio Sigonda, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mheshimiwa Zuleikha Yunus Haji, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga na Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Mwaka Abdulrahaman Ramadhan, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Prof. Philemon Mikol Sarungi, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mheshimiwa Dorah Herial Mushi, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Margreth Agness Mkanga, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya na Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Felix Christopher Mrema, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi, Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Janeth Mourice Massaburi na Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan Athuman Ngwilizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maelezo yetu yapo katika *book* hili lenye kurasa 60. Kwa muda niliopewa sitawenza kuyafikia yote, lakini kwa sababu limeshakamilika, tutawagawia ili kila Mheshimiwa Mbunge apate fursa ya kusoma. Tumegawa majibu yetu katika maeneo sita. Kwanza ili kufanikisha maelezo, kwanza ni ukuaji wa uchumi na mwenendo wa uchumi. Pili ukuzaji wa mauzo nje.

Tatu uandaaji na utekelezaji na ufuatiliaji wa mipango. Nne ni uwekezaji na ubinafsishaji. Tano uvezeshaji na kuondoa umaskini, mwisho sita ni raslimali watu na maendeleo. Pamoja na maeneo haya, kuna baadhi ya hoja zilizotolewa ambazo zimeelekezwa moja kwa moja kwenye sekta, hoja za jinsi hii nitazikabidhi kwa Mawaziri wa Sekta husika ili watoe ufafanuzi wa kina wakati Waheshimiwa Wabunge mtakapopata fursa ya kujadili hoja zao. Hivyo basi, naomba nianze na kutoa maelezo yafuatayo kuhusu fungu la kwanza, yaani la Ukuaji wa Uchumi na Mwenendo wa Bei.

Hoja ya kwanza ilikuwa Serikali itumie mikakati endelevu katika kudhibiti mfumuko wa bei. Pili, ilisema sera zinazowekwa hazilengi hali halisi ya malengo yaliyowekwa kwa mfano haiwezekani kufikia lengo la kupunguza mfumuko wa bei kufikia asilimia 4.5 wakati Serikali inaongeza bei ya mafuta. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Kigoda kwa niaba ya Kamati. Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Balozi Hamis Suedi Kagasheki na Mheshimiwa Benson Mwailugula Mpesa.

Sasa maelezo ni kwamba ipo mikakati na taratibu mahsusizi za kudhibiti mfumko wa bei ikiwa ni pamoja na kutumia Sera za Fedha, yaani *Monetary Policy* kwa kudhibiti ujazi wa fedha, yaani *money supply* nchini kuwiana na malengo ya ukuaji wa uchumi. Kubwa zaidi ni kuongeza uzalishaji wa bidhaa hususan chakula ambacho ndicho kinachochangia kiasi kikubwa katika mwenendo wa mfumko wa bei, huchangia asilimia 55.9 katika farihisi ya bei nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, usafirishaji huchangia asilimia 9.7 tu katika farihisi ya bei nchini mwetu na ni dhahiri basi kwamba mwenendo wa bei unatokana zaidi na chakula na kama chakula hakipatikani, basi mfumko wa bei utapanda kwa haraka zaidi. Hivyo ni muhimu kuendelea kuzalisha chakula kingi zaidi hapa nchini ili kuweza kupunguza mfumko wa bei. Pili, mfumko wa bei unaendelea kushuka. Kufikia mwezi Mei 2007 mfumko wa bei ulikuwa asilimia tano kutoka asilimia 7.3 ya mwezi Februari na kutoka asilimia 6.1 ya mwezi Aprili. Kwa hiyo, mwezi Mei mfumko wa bei ni asilimia tanu. Kwa hiyo, kiwango cha mfumko wa bei kinashuka.

Hoja inayofuata ni ya Mheshimiwa Kabwe na Mheshimiwa Vita Kawawa. Uchumi wa Tanzania unaonekana umekua kwa kutumia shilingi ya Tanzania. Lakini unapotumia dola za Marekani uchumi wa nchi unaonyesha kuporomoka. Ukuaji wa pato la Taifa hupimwa kwa kutumia thamani ya sarafu ya ndani ya nchi husika na si kwa kutumia sarafu ya nchi nyingine. Pato la Taifa ni thamani ya bidhaa na huduma zinazozalishwa ndani ya katika kipindi maalum kwa mfano, mwaka mmoja.

Ukuaji wa pato la Taifa la nchi hauwezi kupimwa kwa kigezo cha sarafu ya nchi nyine, kwa kufanya hivyo ili kulinganisha kati ya nchi na nchi kipimo kinachotumika sahihi ni kipimo kinachoitwa *PPP-Purchasing Power Parity* hicho ndiyo kipimo cha kulinganisha pato la Taifa la nchi mbalimbali. Nirudie tena, *okay* ukuaji wa pato la Taifa la nchi hauwezi kupimwa kwa kiwango cha sarafu ya nchi nyine. Kama lengo ni kulinganisha kati ya nchi na nchi, basi kipimo kinachotumika na kinachokubalika kimataifa ni *PPP* kwa kirefu ni *Purchasing Power Parity*, hicho ndicho kinachotumika kwa kulinganisha lakini *you can not use GDP rate* kwa kulinganisha.

Upimaji wa ukuaji wa uchumi wa pato la Taifa unatumia *Base* zilizobadilika za mwaka, yaani mwaka maalum yaani *Constant Price* na *Base Gear* lazima uwe na *Constant Price* na *Base Gear*. Viwango vya ukuaji vinavyoonyesha katika jedwali 1(b) ndani ya hotuba yangu zimetolewa kwa kutumia bei za mwaka 1992 kama *Base Year* na kama *Constant Price Base*. Kwa hiyo, ni muhimu kulizingatia hilo.

Sababu za ukame pekee hazitoshelezi kuelezea kushuka kwa ukuaji wa Sekta ya Kilimo. Ukuaji wa Sekta ya Kilimo unajumuisha Sekta ndogo za mazao, mifugo, uvuvi, misitu na uendaji. Katika mwaka 2006, Sekta ndogo ya mazao ambayo inachangia asilimia 33.4 katika pato la Taifa na Sekta ndogo ya mifugo ilichangia kwa asilimia 5.7 ziliathirika na ukame kama ilivyoonyesha katika hotuba yangu ya hali ya uchumi.

Aidha, Sekta ndogo ya uvuvi nayo iliathirika kutokana na meli nyangi za uvuvi kuchelewa kuingia baharini kulikosababishwa na migogoro kati ya Mabaharia na wamiliki wa meli. Aya ya 200 katika kile kitabu cha hali ya uchumi tumefanunua hili vizuri zaidi. Ni sekta ndogo ya misitu na uwindani pekee ndiyo iliyokuwa hivyo. Ni vyema mtazamo huu ukaeleweka kama sababu zilizochangia kushuka kwa ukuaji wa Sekta ya Kilimo. Kupungua kwa mchangwa sekta ya kilimo kwenye pato la Taifa hakutokani na kukua kwa mchangwa sekta nyinezo bali kushuka kwa uzalishaji wa kilimo nalo hilo sio sahihi.

Kutokana na sekta nyine kuanza kutoa mchangwa mkubwa katika pato la Taifa kama vile Sekta ya Biashara ya na Utalii, Madini, Ujenzi, mchangwa Sekta ya Kilimo katika pato la Taifa umeanza kupungua mwaka hadi mwaka.

Kupungua kwa mchangwa Sekta ya Kilimo mwaka 2006 haumaanishi kuwa uzalishaji ulishuka usipokuwa tu ni kiwango cha ongezeko la mchangwa yaani *Change in the Proportion to overall GDP* ndiyo iliyobadilika ikilinganishwa na kipindi cha mwaka uliotangulia. Kukua kwa Sekta kuna maana ya kasi ya ongezeko, yaani *rate of growth* na kiasi kinachozalishwa toka mwaka hadi mwaka.

Jedwali namba 4(b) ukurasa wa 14 wa kitabu cha hali ya uchumi inaonyesha kuwa kwa wazi mwenendo wa kupungua kwa mchangwa kilimo mwaka hadi mwaka. Jedwali hili ikilinganishwa kwa pamoja na Jedwali namba 4 ukurasa wa 12 wa kitabu hichohicho linaonyesha ukuaji wa Sekta na inaonyesha kuwa kulikuwa na ongezeko ukuaji wa mwaka 2004 ambapo ukuaji wa Sekta hiyo uliongezeka kufikia 5.8% kutoka

4% mwaka 2003. Lakini mchango wa Sekta ya Kilimo ulipungua kutoka 47.7% mwaka 2003 na kufikia 46.3% mwaka 2004. Huu ni uthitisho wa kutosha kwamba kwa mchango wa Sekta hiyo hautokani na kupungua kwa uzalishali, kwani hata ukuaji unapoongezeka bado mchango wa Sekta hiyo unapungua.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo imedharauliwa mpaka Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji anaiita Sekta ndogo wakati mifugo ni dhahabu isiyohitaji uchimbaji. Mheshimiwa Lucal L. Selelili Mbunge wa Nzega. Kwa mujibu wa mwongozo wa kimataifa kuhusu mgawanyo wa Sekta za uzalishaji ule unatumika na *International System of Classifications*, Sekta ya Kilimo imegawanyika katika Sekta ndogo zifuatazo:-

Sekta ndogo ya kwanza ya mazao, Sekta ndogo ya pili ni mifugo na Sekta ndogo ya tatu ni uvuvi na Sekta ya mwisho ni misitu na uwindaji. Hizi ndiyo Sekta ndogo zinazounganisha Sekta ya Kilimo. Hivyo, kwa kufuata utaratibu huu, mifugo ni ndogo sana katika Sekta ya Kilimo. Serikali inaipa umuhimu Sekta hiyo ndogo kama ilivyo Sekta nyingine. Taarifa ya hali ya Uchumi wa Taifa na Mpango havizungumzii uvuvi. Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir.

Mheshimiwa Spika, aya ya 200 ukurasa wa 118 katika Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2006 taarifa na takwimu kuhusu Sekta ndogo ya Uvuvi zimeonyeshwa katika kitabu cha Hali ya Uchumi. Ukuaji wa sekta hiyo katika mwaka 2006 ulikuwa 5% ikilinganishwa na 5.3% mwaka 2005. Mwaka 2006 mapato yatokanayo na Sekta ndogo ya uvuvi yalikuwa shilingi bilioni 9.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 9.8 ya mwaka 2005. Aidha, mauzo ya mazao ya uvuvi nje ya nchi yalikuwa kilo 44,623, hiyo ni samaki hai na mapambo walikuwa 21,741 ambaa walikuwa na thamani ya shilingi bilion 170 na wallingiza ushuru wa shilingi bilioni 6.2.

Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula mchango wa maandishi haukuwekwa wazi ni kwa namna gani Sekta ya Madini inachangia pato la Taifa. Takwimu za uzalishaji wa Sekta ya madini zimeonyeshwa katika ukurasa wa 13 wa kitabu cha hali ya uchumi na mchango wake wa Sekta hiyo unaonyesha pamoja na Sekta nyingine katika jedwali namba 4(b) ukurasa wa 14 wa kitabu hicho. Mchango wa Sekta ya Viwanda katika pato la Taifa Mheshimiwa Kabwe Zitto alisema mchango huu umepanda kutoptera na kushuka kwa uzalishaji katika Sekta ya Kilimo. Jibu ongezeko la mchango wa Viwanda katika pato la Taifa unaashiria mabadiliko katika mfumo wa uchumi wetu. Watu wengi wanaondokana katika shughuli za asilia ikiwemo kilimo na wanajihuisha zaidi na Sekta za Kisasa *Non Farm Activities* na hivyo kuongeza mchango wa Sekta nyingine katika pato la Taifa.

Serikali ipanue uwekezaji katika Sekta ya huduma ili kuongeza mapato ya mauzo ya nje. Mheshimiwa Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni. Jibu Serikali imetoa kipaumbele kwa Sekta ya Miundombinu katika mwaka huu wa fedha na kwa mantiki hiyo maeneo kama vile reli, barabara, utalii na Bandari yamepewa umuhimu wa pekee. Ni dhahiri kwa kufanya hivyo tutakuwa tunaimarisha *transit trade* na vilevile kuboresha huduma za utalii na TEKNOHAMA. Mchango wa bidhaa asilia katika mauzo ya nje ni madogo ukilinganisha na bidhaa zisizo

asilia Mheshimiwa Kabwe Zitto tena. Jibu Tanzania ilianzisha mkakati wa *Export Verification* ili kupanua wigo wa bidhaa zinazouza nje, yaani za asilia na zisizo asilia. Lengo la Serikali ni kuongeza ubora wa aina zote bidhaa ili kukabiliana na ushindani wa Kimataifa na hatimaye kuongeza mapato ya Taifa kutohana na bidhaa zinazouzwa nje. Kwa kuwa mpango ama mkakati thabiti wa kuongeza mazao ya kilimo ili tuweze kuongeza mauzo nje; Mheshimiwa Kabwe Zitto tena, Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Mheshimiwa James Wanyancha, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa na Mheshimiwa Juma Aballah Njwayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaangalia upya suala nzima la utekelezaji wa mkakati wa uuzaji bidhaa nje, yaani *Export Development Strategy* ili kutoa msukumo mkubwa pamoja na Sekta nyingine. Mkakati wa *Agricultural Sector Marketing Development Programme* unalenga moja kwa moja katika kukuza uuzaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi yetu. Serikali itumie Balozi zetu kutangaza uwekezaji na kadhalika. Swali hili aliuliza Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya.

Serikali inaendelea kutumia Ofisi za Ubalozi zetu za nje katika kutangaza utalii. Lakini vilevile jana tulipata maelezo mazuri sana ya Waziri Jumanne Maghembe kuhusu namna tulivyodhamiria kutangaza utalii na sipendi kurudia tena hapo. Balozi zetu katika nchi za nje ziwe na wataalam wa uchumi ili wawewe kutangaza nchi yetu ipate wawezekaji wengi, Mheshimiwa Raphael Chegeni na Mheshimiwa Feteh Mgeni. Suala hili limeanza kutekelezwa chini ya Sera mpya ya Diplomasia ya Uchumi yaani *Economic Diplomacy*.

Kwa kuzingatia umuhimu wa suala hili, Serikali inaanda utaratibu wa kuongeza wataalam zaidi wa uchumi ili kukidhi upatikanaji wataalam hao katika sehemu mbalimbali za Sekta ya Uchumi wetu. Uandaaji wa utekelezaji na ufuatiliaji wa mipango hili kundi la tatu.

Mheshimiwa Spika, ili kuimariswa mipango ya uchumi wa nchi, iundwe Kamisheni ya Mipango na Uchumi ambayo Mwenyekiti wake atakuwa Rais au Waziri Mkuu na Makamishna watokane na watu waliobobea katika masuala ya uchumi, Wizara iwe Sekretarieti ya Kamisheni hiyo, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Paul Kimiti. Muundo unaopendekezwa kuwa na Kamisheni uliwahi kuwepo miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mamlaka inayohusika iliona umuhimu wa kuwa na muundo wa sasa. Muundo huu wa sasa wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ni kwa mujibu wa *Presidential Instrument* ya mwaka 2005. Hata hivyo, mwenye mamlaka ya kubadilisha muundo wa Wizara au Serikali ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuwa na maeneo machache ya kulinusuru Taifa kiuchumi kwa haraka na Bunge lipewe taarifa za utekelezaji kila baada ya miezi tatu. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Ernest Mabina na Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishaainisha maeneo machache ya kipaumbele yatakayochocha ukuaji wa uchumi, yaani *Quick Wins* kama ifuatavyo:- Elimu, Miundombinu, Kilimo, Afya, Nishati na Maji.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuwa na Mpango Mikakati ya kusaidia Mikoa iliyokuwa nyuma kimaendeleo na umuhimu wa kuzingatia hali halisi ya umaskini Kiwilaya kama kigezo cha kugawa rasilimali badala ya kutumia *clarity* za MKUKUTA peke yake, alizungumzia Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Mgana Msindai.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele vilivyowekwa na Serikali vinazingatia Mikoa iliyoyuwa nyuma kimaendeleo kwa kugawa rasilimali katika maeneo yatakayosaidia Mikoa hiyo kukuza uchumi kwa haraka. Kwa mfano, katika elimu, kipaumbele kimojawapo ni ujenzi wa nyumba za Walimu. Katika Afya kipaumbele kimojawapo ni ukarabati wa hospitali za Mikoa. Serikali imekuwa na utaratibu wa kugawa fedha za maendeleo katika Wilaya kwa kuzingatia maeneo ya MKUKUTA na pia idadi ya watu, hali ya umaskini na ukubwa wa eneo ukiondoa hifadhi za misitu na maziwa. Serikali itaendelea kuboresha utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah walizungumzia kuhusu umuhimu wa Serikali kufuutilia matumizi ya fedha zitakazopelekwa katika Halmashauri na sera ya kupeleka madaraka na rasilimali kwa wananchi kupitia sera ya Serikali ya *D by D*.

Serikali inatekeleza Ilani ya Uchaguzi kwa kupeleka madaraka ya wananchi kwa kupeleka rasilimali watu, rasilimali fedha na nyenzo za kufanya kazi. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 fedha nyingi zimepelekwa katika ngazi ya Wilaya. Hivyo, Serikali inaboresha utaratibu wa ufuutiliaji katika ngazi zote.

Aidha, Mabaraza ya Madiwani wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, yanatakiwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mipango na bajeti katika maeneo yao ili kuharakisha maendeleo ya maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kutathmini miradi inayoendelea kabla ya kuandaa mpango wa bajeti. Mheshimiwa Joyce Machimu, hili linafanyika kila mwaka siyo jipya. Hata hii hali ya uchumi tuliyotoa hapa, kitu cha kwanza tulichofanya ni kutathmini hali ya uchumi ya mwaka 2006 na baadaye ndiyo tukafanya mipango.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa Chuo cha Mipango cha Maendeleo Vijijini Dodoma kipewe hadhi inayostahili. Serikali inatekeleza Mpango Mkakati wa Chuo wa muda na wa kati mwaka 2004/2005 hadi 2008/2009 unaolenga kukiboresha Chuo hicho kwa kukiongeza na kuimarisha miundombinu, Maktaba ya kisasa inajengwa, majengo ya taaluma, Utawala pamoja na Ukumbi wa kisasa yaani *Multi Purpose Hall* nao unajengwa. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, uzio wa kiwanja cha ndege cha Bukoba, Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki na Mheshimiwa Savelina Mwijage walizungumzia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwajibu Waheshimiwa Wabunge kuwa, uzio wa waya upo. Labda wanachotaka ni uzio wa ukuta wa matofali. Changamoto kwa kiwanja cha ndege cha Bukoba ni *runway* ile sehemu inapotua ndege ili iwe imara zaidi kama vile ya lami. Serikali itatekeleza hili kadri ya uwezo wa fedha utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kupeleka umeme Zanzibar kupitia Tanga, haikuelezwu katika Taarifa ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Waziri atoe maelezo! Aliyeuliza alikuwa Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha.

Mheshimiwa Spika, maelezo yake ni kwamba, mpango huu uko chini ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na unaendelea vizuri na siyo wa Muungano. Kuhusu Uwekezaji na Ubinafsishaji, Serikali ibuni na kuanzisha vivutio kwa wawekezaji wakubwa na wadogo katika Sekta ya Kilimo Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda. Serikali imeweka vivutio mbalimbali katika Sekta ya Kilimo na vivutio hivyo ni pamoja na kutoza gharama ndogo za kodi ya ardhi kwa ekari kutoka shilingi 600 kwa mwaka hadi sasa shilingi 200. Kusamehe kodi ya vifaa vya kilimo kama vile matrekta na kadhalika. Aidha, upatikanaji wa masoko na mikopo kwa wakulima yanaendelea kuboreshwa kwa kupitia programu mbalimbali za Serikali kama vile MKUMBITA, MKURABITA na *Export Credit Guarantee Scheme*.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji wahamasishwe kuwekeza Tabora na hasa katika usindakaji wa asali Mheshimiwa Mwanne Mchemba. Kituo cha Uwekezaji Tanzania kitaendelea kutangaza vivutio mbalimbabil vilivyopo hapa nchini likiwemo suala la uwekezaji na usindikaji wa asali hususan Mkoani Tabora. Aidha, mafanikio katika eneo hili yatategemea sana utendaji wa Mabaraza ya Biashara ya Mikoa likiwemo Baraza la Biashara la Mkao wa Tabora, *SACCOS* na Vyama vya Ushirika katika kuhamasisha masuala ya uwekezaji katika Mikao yao ukiwemo ufugaji wa nyuki na kurina asali.

Mheshimiwa Spika, ninaruka kidogo kwa sababu ya *time*. Ongezeko la *FBI* ni kidogo na taarifa zinaonyesha bado hatujatumia ipasavyo maliasili yetu, utandawazi na utaalam kuvutia wawekezaji zaidi. Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki na Mheshimiwa Emmanuel Luhahula walitaka maelezo. Uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje yaani *FBI* umekuwa ukiongezeka tangu mageuzi makubwa ya kiuchumi yafanyike.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na taarifa ya Uwekezaji nchini, uwekezaji huu wa moja kwa moja umeongezeka kutoka *dollar* za Kimerakani milioni 330.6 mwaka 2004 hadi *dollar* za Kimarekani milioni 447.6 mwaka 2006. Kwa mwaka 2006 *FBI* inakadirisha kufika *dollar* za Kimarekani milioni 474.5. Ongezeko hilo siyo ndogo katika nchi za Afrika ukiondoka Afrika Kusini na nchi zile zenye mafuta. Itakumbukwa pia kuwa *FBI* katika kipindi cha 1992/1995 ilikuwa wastani wa *dollar* za Kimarekani 90 tu kwa mwaka. Kwa hiyo, ni maendeleo makubwa tumeyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto, sekta ya mafuta na gesi asilia hazikuzungumzwa kabisa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uvezeshaji.

Mheshimiwa Spika, maelezo ni kwamba mafuta na gesi asilia yametolewa katika aya 62 ya hotuba yangu chini ya kipengele cha nishati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto anaendelea bado. Kitabu cha Hali ya Uchumi katika mwaka 2006, kinaonyesha kuwa uzalishaji wa nyama umeongezeka wakati vipande vya ngozi vimepungua, maelezo yatolewe.

Mheshimiwa Spika, maelezo, tofauti ya uzalishaji nyama na idadi ya ngozi imetokana na ukweli kwamba uzalishaji wa nyama unajumuisha nyama ya ng'ombe, kondoo, mbuzi, kuku na nguruwe. Kuku na nguruwe hawatoui ngozi. Aidha, uzalishaji wa nyama unahesabiwa kwa kipimo cha tani wakati ile ya ngozi ni idadi ya vipande. Kwa maana hiyo, kuongezeka kwa uzalishaji wa nyama hakuna uhusiano na kuongezeka kwa vipande vya ngozi. Jedwali 11.4 ya sura 11 ya kitabu cha Hali ya Uchumi inaeleza wazi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Elisa Mollel Sekta binafsi ishirikishwe katika kuandaa miunbombinu safi. Serikali inatambua umuhimu wa Sekta binafsi katika kukuza uchumi. Kwa mantiki hiyo, mchakato wa kuandaa utaratibu wa kisheria na muundo wa Kitaasisi wa miradi ya kushirikisha kati ya Serikali na Sekta Binafsi, yaani *Public-Private Partnership-PPP* hasa kwenye Sekta ya Miundombinu unaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, suala la *Lodge* ya Mikumi. Kwa vile suala hili liko Mahakamani, tunasubiri matokeo ya uamuza wa Mahakama ili ubinafsishaji wa hoteli hiyo uendelee.

Mheshimiwa Spika, Serikali isimamie vizuri utekelezaji wa MKUKUTA hususan programu zinazotekelezwa kwenye Halmashauri, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Serikali inasimamia utekelezaji wa MKUKUTA kupitia Wizara ya Mipango, Uchumi na Uvezeshaji na Wizara ya Fedha na pia kupitia Wizara za Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na kuimarisha Vitengo vya ufuatiliaji na tathmini, yaani *Monitoring and Evaluation Units*, katika Idara za Mipango, Wizara, Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Wilaya Mabaraza ya Madiwani ambayo Waheshimiwa Wabunge ni Wajumbe ndicho chombo kikuu cha kusimamia utekelezaji wa mipango yote ikijumuisha programu za MKUKUTA katika ngazi zao. Kwa hiyo, changamoto iliyopo ni kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji unaoendelea kutekelezwa ili kuweza kufuatilia na kupima mafanikio ya utekelezaji wa malengo ya MKUKUTA na Mpango wa Maendeleo ya *Millennium*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir; wananchi waelimishwe kuhusu programu za kupunguza umaskini kama vile uzalishaji wa chumvi Zanzibar. Hili

tunalfanya, lakini kama nilivyosema, ni majukumu ya Mabaraza ya Madiwani kutazama vizuri utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura alisema hakuna hata mtu mmoja Wilayani Tunduru aliyepata mkopo kutokana na fedha zilizotengwa kwa ajili ya uwezeshaji. Nakubali kule haijafika kwa sababu siyo ya makusudi, kwa sababu zile Taasisi ambazo zinatakiwa kushughulikia suala hili, yaani *NMB* na *CRDB* hawana matawi kule. Kwa hiyo, awamu ya pili, tutahakikisha kwamba nchi nzima itafikiwa kwa sababu tutatumia *SCULT*, tutatumia *Tanzania Postal Bank*, tutatumia *Community Banks* pia. Kwa hiyo, Awamu ya pili, itawafikia wote nchi nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir *TASAF* ina urasimu mkubwa wa kuzipata fedha. Je, kwa nini Serikali hairekebishi haraka tatizo hili? Jibu ni kwamba *TASAF* inafuata taratibu ambazo Serikali imekubaliana na Benki ya Dunia kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatumika kwa miradi inayotekelzwa na wananchi. Utaratibu huu unazihusisha jamii kuibua miradi na kuweka fomu za makusudio za kuanzisha miradi. Fomu hiyo uwekwa saini na Afisa Mtendaji wa Kijiji au Mtaa au Sheha wa Shehia, hujadiliwa kwenye Kamati ya Fedha na Mipango ya Wilaya na baadaye kuwasilishwa *TASAF* Makao Makuu kwa mapitio kwa nia ya kuthibitishwa kuwa taratibu zote zimefuatwa.

Kwa hiyo, ni muhimu hapo kuhakikisha kwamba wananchi wanaibua miradi ile na miradi ile ni yao.

Mheshimiwa Spika, kwa nini kiwango kinachotolewa ni kidogo? Mheshimiwa Mzee Ngwali Zuberi aliuliza. Kiwango kidogo kinatolewa kwa sababu shabaha ya *TASAF* ni kusaidia utekelezaji wa miradi midogo midogo kwa ngazi ya jamii na kwa viwango vya kati ya *dollar* 5,000 mpaka 30,000.

Mheshimiwa Spika, viwango hivyo vimewekwa katika Mkataba kati yetu na Benki ya Dunia. Kwa hiyo, haiwezekani kuvibadilisha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naona muda umepita, elimu kuhusu *TASAF*. Elimu kuhusu *TASAF* tumeitoa kweli na tunaendelea kuitoa, lakini nadhani ni muhimu viongozi wote wa ngazi ya Wilaya kuendelea na wenywewe kutoa elimu hiyo. Hiyo pia inawashirikisha Waheshimiwa Wabunge ili wawahamashe wananchi wao waibua miradi kwa manufaa ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, ahsante sana. Nina hakika jitihada zitafanyika ili kutugawia majibu hayo kwa sababu yanaelekea kufafanua vitu vingi sana ambavyo vilikuwa vinaulizwaulizwa.

Kwa hiyo, Ofisi ya Bunge itakuwa tayari kusaidiana nawe kuona kwamba Waheshimiwa Wabunge ikiwezekana wanapata majibu hayo leo.

Mheshimiwa Spika, sasa ni zamu ya mtoa hoja wa pili, lakini nadhani watatangulia Manaibu Mawaziri wa Fedha. Mheshimiwa Mustafa Mkulo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):**  
Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii nami kuchangia hoja zote mbili zilizowasilishwa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji Mheshimiwa Juma Alifa Ngasongwa.

Awali ya yote, nieleze kabisa kuwa naunga mkono hoja zote mbili kutokana na kusheheni masuala muhimu ya kitaifa yanayolenga kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama chetu cha Mapinduzi, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini na Malengo ya Maendeleo ya Milenia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii nami kuwapa pole na kuwaombea wapone haraka majeruhi wote waliopatwa na ajali mbaya ya gari Mkoani Singida na nawapa pole wafiwa kwa kupoteza ndugu zao wapendwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kuchukua nafasi hii kuchangia baadhi ya hoja zilizojiteza wakati wa kujadili hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha, kwa mwaka wa 2007/08 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ya kwanza, marekebisho ya *TIB* ilikuwa Benki ya Maendeleo ya Tanzania. Serikali imekwishafanya uamuvi wa kuirekebisha Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*) kuwa Benki ya Maendeleo. Mwaka 2006, Serikali iliongeza mtaji wa *TIB* kwa shilingi bilioni 12.7, hivyo kufanya jumla ya mtaji wa Benki ya Rasilimali kufikia shilingi bilioni 24.9. Nyongeza hiyo ya mtaji ilikuwa ni kwa njia ya kubadili fedha zilizokuwa zinasimamiwa na Benki kwa niaba ya Serikali. Nyongeza hiyo ya mtaji imeongeza uwezo wa *TIB* wa kuweza kuwa na vianzio zaidi vya fedha, ambapo katika mwaka 2007 kiasi cha Dola za Marekani milioni 5.0 zilipatikana.

Mheshimiwa Spika, urekebishihi wa Benki ya Rasilimali unaendelea. Hivi sasa kiasi cha mikopo iliyoidhinishwa imefikia shilingi bilioni 30, ambapo zaidi ya asilimia 60 zilizotolewa kwa makampuni madogo madogo na ya kati (*SMEs*).

Aidha, pamoja na gharama kubwa za urekebishihi wa Benki, *TIB* imeendelea kupata faida. *TIB* pia inasimamia mfuko maalum wa Serikali wenye kiasi cha Dola za kimarekani milioni 40 kwa ajili ya uzalishaji wa maua ya kuuza nje ya nchi ili kuongeza mauzo yetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, ya pili, ruzuku kwa Shirika la Umeme Tanzania. Suala la *TANESCO* lilishashughulikiwa na Serikali kwa kuzingatia kuwa ni dharura iliyotokana na

ukame hapa nchini sambamba na bei kubwa ya mafuta katika Soko la Dunia. Bila ya Serikali kuisaidia *TANESCO* kununua umeme, hali ya mgao wa umeme ingekuwa mbaya zaidi na kuathiri uzalishaji, kukua kwa uchumi, mapato ya Serikali, na hasa mfumko wa bei ambao ulikuwa umeshuka hadi kufikia asilimia tano mwezi Mei, 2007.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kulisaidia Shirika kupata fedha kwa ajili ya kununua umeme kutoka kwa wazalishaji binafsi na pia kununua mitambo mipyta, Serikali hivi sasa inaelekeza nguvu zake katika kuiwezesha *TANESCO* kutekeleza mpango wake wa uwekezaji kwa kipindi cha miaka mitano hadi mwaka 2011. Mpango huu, ambao ni sehemu muhimu ya mpango wa kutengemaza hali ya kifedha ya Shirika (*Financial Recovery Plan – FRP*) unahitaji kiasi cha Dola za Kimarekani bilioni 1.3. Tunafanya kazi kwa karibu sana na Menejimenti ya *TANESCO* ili kupata kiasi hicho cha fedha kwa kushirikisha sekta binafsi na Wahisani.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu, ushuru wa nyama toka nje uongezwe. Serikali inaangalia kwa makini namna ya kuhakikisha kuwa viwanda vya ndani vinaimarishwa na kuboreshwa ili kuongeza ajira na pia kuhimili ushindani. Serikali itafanya utafiti na kukusanya ushahidi wa uwezo wa Tanzania kutosheleza soko la nyama la ndani kwa maana ya Afrika Mashariki ili kuwa na hoja ya kuwashawishi wenzetu wakubaliane na hoja ya kuongeza kiwango cha ushuru wa forodha. Huu ndio utaratibu unaotumika kwa nchi zote ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuwa chombo chenye mamlaka ya kubadilisha viwango vya Ushuru wa Forodha ni Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ili kuhakikisha kuwa viwanda vyetu vinalindwa, Serikali itapeleka mapendekezo katika Baraza hilo kuthibitisha kuwa Tanzania inao uwezo wa kutosheleza soko la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, ya nne, kuwa utaratibu mpya wa kuondoa mizigo Bandarini utatoa mwanya kwa wafanyabiashara kukwepa kodi. Hili limezungumzwa na wengi. Kambi ya Upinzani na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamehoji utaratibu mpya wa kuharakisha utoaji wa mizigo bandarini.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu wafanyabiashara wamekuwa wakilalamika kuhusu ucheleweshaji wa kutoa mizigo katika vituo vyetu vya forodha, hususan Bandari ya Dar es Salaam. Bunge hili pia limeeleza mara nyingi umuhimu wa kupunguza mlolongo wa taratibu ndefu za kuondoa mizigo bandarini. Moja ya athari za ucheleweshaji wa mizigo katika Bandari zetu ni kupoteza biashara ya kikanda, (*transit traffic*).

Mheshimiwa Spika, taratibu na kanuni za Forodha Kimataifa na Kitaifa zimekuwa zikitekelezwa kwa usawa kwa waagizaji wote bila kujali kiwango chao cha kulipa kodi kwa hiari (*compliance*). Serikali imeliona tatizo hilo na kuwa wafanyabiashara waaminifu, waadilifu na wenye kuheshimu sheria za kodi wanapewi utofauti na wale ambao wamekuwa wadanganyifu. Kimataifa pia tatizo la urahisishaji wa taratibu za biashara na forodha kwa biashara iliyo “*secure*” na wafanyabiashara wenye hiari na uaminifu ni eneo linalowekewa mkazo kwenye kikanda cha Shirika la

Forodha la Ulimwengu (*World Customs Organization*) ambalo linatarajia kufanya kikao chake mwezi Julai, 2005.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa kuboresha huduma za Forodha bandarini ambao sote kwa pamoja tumekuwa tukidai, nchi 152 wanachama wa Umoja wa Forodha Ulimwenguni (*World Customs Organisation*) walikubaliana juu ya “*Framework on Standards for Facilitated Secure Trade.*” Utaratibu huu unatumika katika nchi nyinigine kama vile Singapore, Malaysia, Zambia, Kenya, Uganda, Afrika ya Kusini na nchi nyingine za Mashariki na Kusini mwa Afrika (*ESA*) kwa kutumia majina mbali mbali ya mfumo huo.

Kwa utaratibu huu, mizigo yote inayoingia nchini itapitia taratibu zote za awali za kiforodha ikiwa ni pamoja na kupitiwa kwa nyaraka zote za msingi ili kuzihakiki na ikibidi kuzipitisha kwenye mtambo wa ukaguzi (*X-ray Scanner*).

Tofauti iliyopo ni kwamba mizigo ya wafanyabiashara waadilifu haitasubiri kukamilisha taratibu zote za ukaguzi (*physical examination*) bandarini. Hii ni katika jitihada za Serikali kuboresha na kurekebisha mfumo wa forodha kwa kuwapa upendeleo ndani ya taratibu za forodha walipa kodi wenye hiari na waadilifu na kuongeza ukaguzi kwa wale ambao sio waadilifu.

Mheshimiwa Spika, *TRA* imefanya maandalizi ya kutosha kutekeleza hatua hii kwa ufanisi. Hadi sasa Mamlaka ya Mapato Tanzania imewatambua wafanyabiashara takriban 80 ambao wanachangia mapato yasiyopungua asilimia 60 ya mapato yote ya *TRA* yanayokusanywa na Idara ya Forodha na kuwaingiza katika utaratibu wa wafanyabiashara wanaolipa kodi kwa hiari (*compliant traders*). Sehemu kubwa ya makampuni haya ni yale ambayo tayari yako chini ya Idara ya Walipakodi Wakubwa na ambao mwenendo na rekodi zao kuhusu ulipaji kodi ni mzuri. Makampuni hayo ni kama *Tanzania Breweries Limited, Tanzania Cigarette Co. Ltd., Tanzania Portland Cement Co. Ltd.*, Makampuni ya CocaCola na mengine.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa mizigo kupitia kwenye mlango wa kijani haimaanishi kwamba mizigo hii itapita bila kufuata taratibu zozote za kiforodha. Taratibu zote za msingi za kiforodha zikiwa ni pamoja na ‘*ku-declare*’ mizigo yote na kulipa kodi husika zinafanyika. Baada ya mizigo kuondolewa bandarini, ukaguzi wa kina, yaani *Post Clearance Audit* utafuata ambao utafanywa na kitengo maalum cha “*Post Clearance Audit Unit*” ambacho kitasimamia na kufuutilia utaratibu huu. Baada ya *Post Clearance Audit*, mfanyabiashara yejote atakayegundulika kukiuka taratibu za forodha i.e. “*under declaration*” atapewa adhabu kali kama zilivyoainishwa kwenye sheria ya forodha pamoja na kuondolewa kwenye utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge wanavyojua, katika mwaka huu wa fedha, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) imetakiwa kukusanya mapato ya karibu shilingi bilioni 300 kwa mwezi. Bila kuwepo na utaratibu mzuri wenye kuhakikisha kuwa mizigo inatolewa haraka na wakati huo huo kulinda mapato ya Serikali, jitihada za kufikia makusanyo yaliyolengwa hazitafanikiwa. Serikali inaona

kuwa utaratibu huu ni mzuri, lakini endapo kutajitokeza matatizo, basi hatua za kurekebisha zitafanyika haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia *package tourism*, Serikali inapoteza mapato mengi, hivyo itafute mbinu za kunufaika na utalii. Serikali imeliona tatizo la nchi kupoteza mapato yake kutokana na mawakala wa utalii kupokea malipo ya watalii na kubakiza sehemu kubwa ya fedha hizo nje ya nchi. Hata hivyo, tumeanza kuchukua hatua mbalimbali za kunufaika na utalii, uwindaji, uvuvi, misitu na maliasili nyinginezo. Hatua za kisera zilizokwishachukuliwa na Serikali hivi sasa kwa lengo la kuongeza manufaa kwa Taifa ni pamoja na kufanya watalii watumie huduma ya wasafirishaji na waongoza watalii (*Tour Guides*) walioandikishwa hapa nchini.

Aidha, Serikali imeona kuwa tatizo kubwa katika Sekta ya Utalii ni gharama za usafirishaji wa watalii ambapo usafiri unachukua karibu asilimia 60 ya *package* nzima. Kwa vile hatuna ndege zetu wenyewe kusafirsha watalii hao katika safari za kimataifa inakuwa vigumu kurekebisha tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika bajeti ya mwaka 2007/2008 Serikali imeanza kutekeleza baadhi ya sera ambapo Serikali imependekeza kuongeza viwango vya ada na tozo mbalimbali ambapo kiasi cha shilingi bilioni 33.616 zinatarajiwu kukusanya kutoka na sekta hii. Katika hali ya soko huru na la ushindani, tunafikiri kuwa tozo na ada mbalimbali ndiyo njia sahihi na rahisi ya kuihakikishia mgao muafaka wa malipo wanayofanya watalii hata kama itakuwa kwa *package tourism*.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha mapato kutoka kwenye sekta hii yatatolewa na Waziri wa Maliasili na Utalii atakapowasilisha bajeti ya Wizara yake hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, liliofuata ni *flow meters* ziwekwe katika Bandari ya Tanga. Uwekaji wa mita za kupima ujazi wa mafuta *flow meters* katika Bandari ya Tanga ulikamilika mwezi Agosti, 2006. Jumla ya *flow meter* tatu zimefungwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania katika Bandari hii.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa aina ya mita hizo ni *mechanical* tofauti na zile zilizofungwa Dar es Salaam ambazo ni *automated*. Kwa bahati mbaya usahihi wa taarifa za mita hizo ulipungua baada ya muda mfupi wa matumizi kwa mita hizo kusoma kiasi pungufu ya kiasi halisi kilicho pitishwa na hivyo kuhitaji kufanyiwa marekebisho. *TRA* imeshawasiliana na Mamlaka ya Bandari Tanzania (*TPA*) ili waweze kuzifanyia marekebisho na kuweka utaratibu wa kufanya matengenezo ya mara kwa mara.

Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania itaendelea kushirikiana na wamiliki wa mita hizo, yaani Mamlaka ya Bandari ya Tanzania katika kutathmini utendaji kazi wa mita hizo na kuhakikisha kuwa hitilafu zozote zinazotokea katika utendaji kazi wa mita hizo zinariotiwa mara moja na kuhakikisha kuwa mita zinafanya kazi ipasavyo. Wizara yangu inawasiliana na Wizara ya Miundombinu ili kuweka mfumo wa umiliki na matengenezo endelevu na hivyo kuhakikisha Serikali inapata manufaa iliyokusudia.

Mheshimiwa Spika, lingine, mifumo miwili ya ulipaji kodi kwa bidhaa zinazotoka Zanzibar unasababisha bidhaa kulipiwa mara mbili. Masuala yote ya uingizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi yanasmamiwa na Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2004. Kifungu namba 135 cha Sheria ya Usimamizi wa Forodha kinafafanua kwamba kodi ambayo haikukusanya au ilikadiriwa pungufu kwa makosa, inapaswa kukusanya pale inapobainika kuwa haikulipwa kikamilifu. Ukusanyaji huu sio maalum kwa mizigo ambayo ilikadiriwa pungufu Zanzibar tu bali kwa sehemu yoyote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa vile taratibu za kuthamini mizigo ki-forodha hazijaoanishwa kati ya Tanzania Bara na Zanzibar pamoja na kuwa viwango vya Ushuru viko sawa, bado kuna ulazima wa kuthamini upya bidhaa zinapotoka upande mmoja wa Muungano kwenda upande mwingine wa Muungano. Hata hivyo, hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kwa nia ya kuoanisha taratibu za kuthamini bidhaa na hivyo kuondoa ulazima wa kuthamini bidhaa zinapohamishiwa upande mwingine wa Muungano. Mamlaka ya Mapato imetoe mwongozo pamoja na maelekezo ya nyaraka zifi zinazotakiwa ili mwagizaji/mhamishaji aweze kutoa au kuhamisha mizigo yake bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, usajili wa magari yaliyosajiliwa Zanzibar yanapokuja Tanzania Bara ni tatizo. Usajili wa magari siyo suala la Muungano kwa kuwa linasimamiwa na sheria mbili tofauti, kila moja ikifanya kazi katika upande mmoja wa Muungano. Kwa upande wa Tanzania Bara, sheria inayotumika ni sheria ya Uandikishaji na Uhamishaji wa Magari ya Mwaka 1972. Aidha, kwa upande wa Zanzibar sheria inayotumika ni ya Vyombo vya Usafiri Barabarani ya mwaka 2003. Hata hivyo, usajili wa magari kutoka Zanzibar hautofautiani na utaratibu unaotumika kwenye usajili wa magari yanayotoka sehemu nyingine yoyote.

Mheshimiwa Spika, kiutaratibu usajili wa magari unaanza pale mwombaji anapowasilisha kwa msajili wa magari, hati zinazoonyesha uhalali wa umiliki wa gari husika ikiwa ni pamoja na uthibitisho kuwa kodi zote zinazohusiana na uingizaji wa gari husika zimelipwa. Baada ya ukaguzi wa nyaraka na kuthibitika kuwa ni sahihi, uandikishaji huchukua sio zaidi ya siku moja. Kwa kuwa zipo sheria mbili tofauti za usajili, utekelezaji wake huonekana kama ni kero kwa wananchi, hivyo suala hili limepelekwa kwenye Tume ya Pamoja ya Kushughulikia Kero za Muungano kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuweka muda maalum wa muingizaji kuendelea kutumia gari iliyohandikishwa kwa upande mmoja wa Muungano wakati mhusika anashughulikia taratibu za usajili, Sheria zote mbili za Usajili wa magari zilizotajwa hapo juu zinatoa muda wa miezi mitatu kuruhusu gari husika kutumika. Naamini muda huo unatosha kukamilisha taratibu hizo na hakuna haja ya kuongeza muda mwingine zaidi.

Mheshimiwa Spika, ushuru wa mafuta ya kula uongezwe ili kulinda soko la ndani la mafuta hayo. Chini ya Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, mafuta ghafi ya kula (*Palm Crude Oil*) hayatozwi Ushuru wa Forodha kwa kuwa yanachukuliwa kama malighafi ya msingi kwa viwanda vya kusindika mafuta ya kula. Hata hivyo, mwaka jana Tanzania iliomba na kukubaliwa kutoza ushuru wa asilima 10% kwenye bidhaa hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hii ni kwa sababu Serikali inafahamu fika umuhimu wa kulinda soko la mafuta pamoja na wakulima hususan wazalishaji wa alizeti, pamba, ufuta na mawese.

Aidha, hivi sasa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki limechukua hatua ya kuunda timu ya wataalamu watakaotathmini athari za mafuta yanayoingizwa nchini kwa viwanda vyetu pamoja na wazalishaji katika soko la Afrika Mashariki. Wakati tunasubiri matokeo ya kazi ya timu hiyo, Tanzania itaendelea kutoza ushuru wa asilimia 10. Nawaomba Waheshimiwa kuvuta subira hadi timu hiyo ikamilishe kazi yake kabla ya kufikiria kuongeza tena au kupunguza ushuru huo. Uzoefu uliodhihiri kutokana na hatua iliyochukuliwa na Serikali mwaka jana na kama walivyoeleza baadhi ya Waheshimiwa Wabunge umeonyesha kwamba kumekuwa na ongezeko la bei ya mbegu za mafuta ambalo ni jambo jema kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, Wamachinga wanatumiwa na Wafanyabiashara wakubwa kukwepa kodi. Katika kukabiliana na matatizo ya ukwepaji kodi hasa katika sekta isiyo rasmi, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanzisha utaratibu wa kuwashughulikia walipakodi kwa kuzingatia maeneo maalum (*Block Management*). Utaratibu huu unaiwezesha Mamlaka kuwatambua na kuwasajili walipakodi katika eneo husika pamoja na kupata taarifa za biashara zao ili kuboresha ukadiriaji kodi.

Aidha, katika kuhakikisha tabia hiyo inadhibitiwa, juhudni mahsusni zinafanywa katika kuwakagua wafanyabiashara wakubwa ili kutambua kodi inayokwepwa kutokana na mauzo yasiyorekodiwa. Zoezi hili limefaidika kutokana na juhudni za Serikali za kuwajengea Machinga maeneo maalum ya kufanya biashara na kuacha kutembeza bidhaa zao barabarani.

Katika juhudni za kuwawezesha wafanyabiashara wadogo walio katika kundi hili, *TRA* imetoe machapisho mbalimbali ya kuelimisha kuhusu uendeshaji mzuri wa biashara.

Mheshimiwa Spika, juhudni zote hizi zitaendelea kufanya ili kuhakikisha wamachinga wanakua na kuwa wafanyabiashara kamili na hawatumiki kuwanufaisha wafanyabiashara wakubwa wanaotaka kukwepa kodi.

Mheshimiwa Spika, pato litokanalo na ajira linatozwa kodi kama faida itokanayo na ajira kwa mujibu wa sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, huu ni utaratibu unaotumika kote ulimwenguni. Mwajiriwa anayo haki ya kudai na kupewa punguzo la gharama zozote anazoweza kuwa ameingia katika kutekeleza wajibu unaompatia kipato. Kwa kuwa kodi kwenye mshahara hukatwa

na mwajiri moja kwa moja, mfanyakazi anayedai punguzo la mapato kutokana na gharama alizolipa hana budi kujaza *return* ya mapato na kutozwa kodi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mfumo huo wa kawaida, wakati wa kutunga sheria mpya ya Kodi ya Mapato mwaka 2004, Serikali iliamua kuwapunguzia zaidi mzigo wa kodi waajiriwa kwa kusamehe kodi kwenye pato la ajira litokanalo na:-

- (i) Huduma ya chakula inayotolewa na mwajiri katika eneo la kazi bila ubaguzi;
- (ii) Huduma za matibabu na malipo ya bima ya afya kwa mwajiriwa na mke/mme na hadi watoto wanne;
- (iii) Malipo ya nauli ya mwajiriwa, mke/mme na watoto wanne wakati anapoajiriwa kwa mara ya kwanza na anapostaafu;
- (iv) Michango ya mwajiriwa kwenye mifuko ya pensheni iliyosajiliwa na Kamishna; na
- (v) Malipo ya mafao kutoka katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iliyosajiliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004 ibadilishwe ili isaidie ongezeko la Usafirishaji wa mizigo. Usafirishaji wa mizigo kwenda nje ya nchi kupitia usafiri wa ndege zinazomilikiwa na wafanyabiashara wasio wakazi wa Tanzania hutozwa Kodi ya Mapato kwa kiwango cha asilimia tano ya gharama yote ya usafirishaji. Kodi hii ilikuwepo katika miaka ya nyuma chini ya sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 1973.

Mheshimiwa Spika, ushahidi uliopo unaonyesha kuwa kupungua kwa ndege za mizigo Mwanza hautokani na Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 kwani kiwango cha asilimia tano kinatumika katika viwanja vingine vya ndege kama vile viwanja vya kimataifa vya Kilimanjaro na Dar es Salaam. Viwanja hivi vinatumwa sana na wafanyabiashara katika usafirishaji wa bidhaa mbalimbali kama vile maua na samaki aina ya *prawns* na tangu kiwango hiki kianze kutumika, hakuna ushahidi wowote kuonyesha upungufu wa ndege katika viwanja hivi. Kwa hali hiyo, ni vyema utafiti wa kina ufanyike ili kubaini ni kwa nini ndege za kusafirisha mizigo zimepungua katika uwanja wa ndege wa Mwanza badala ya kuhusisha upungufu huo wa ndege na suala la utozaji kodi.

Mheshimiwa Spika, kulingana na takwimu za *TRA* Mkoa wa Mwanza, zimeonyesha kuwa idadi ya ndege zilizotua Mwanza kwa ajili ya kubeba minofu ya samaki katika kipindi cha Januari, 2007 hadi Mei, 2007 zilikuwa ni 45 (kubwa 19 ndogo 26) na siyo ndege mbili kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIB):**  
Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii nami

kuchangia hoja zote mbili zilizowasilishwa na Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji - Mheshimiwa Juma Alifa Ngasongwa .Awali ya yote, nieleze kuwa naunga mkono hoja zote mbili zilizoandaliwa kwa umahiri mkubwa na kwa kuzingatia masuala muhimu ya kitaifa yanayolenga kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama chetu cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii nami kuwapongeza wachezaji wetu wa Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu, Taifa *Stars* kwa kufanya vyema katika mchezo wao wa hivi karibuni na kutoa matumaini ya kusonga mbele katika safari ya kwenda Ghana mwakani. Ni vijana wetu wamethibitisha kuwa chochote kinachowezekana kama kunakuwepo na dhamira ya dhati.

Kwa upande mwingine, nachukua nafasi hii kuwapa pole wale wote waliopatwa na ajali mbaya ya gari mkoani Singida. Naomba Mwenyezi Mungu awape nafuu ya haraka waliojeruhiwa. Aidha, nawapa pole wafiwa wote kwa msiba huo uliowakuta. Mwenyezi Mungu awalaze pema Peponi Marehemu wote waliofariki katika ajali hiyo. Amen.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kuchukua nafasi hii kuchangia baadhi ya hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili hotuba ya bajeti kwa mwaka wa 2007/2008 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja kuhusu uwezo wa Halmashauri kusimamia fedha za umma, hasa kutokana na kuwa na akaunti nyingi za Benki ni hafifu. Tatizo la usimamizi hafifu wa fedha katika Halmashauri liko wazi kwa kila mtu sasa, ikiwemo Wizara ya Fedha.

Hatua zinazochukuliwa kukabiliana na hali hii ni pamoja na hizi zifuatazo:-

- (i) Ajira ya Wahasibu 207 na Wakaguzi wa Ndani 64 mwaka 2006 na wengine zaidi ya 600 wanategemewa kuajiriwa hivi karibuni;
- (ii) Kuimarisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kutekeleza kikamilifu majukumu yake katika ngazi zote za Serikali, ikiwemo ya Halmashauri;
- (iii) Kuundwa kwa kitengo maalum cha kufuatilia matumizi ya Serikali (*Expenditure Tracking Unit*) katika Wizara ya Fedha ili kufualtilia kwa karibu sana matumizi ya fedha katika Halmashauri;
- (iv) Katika kuhakikisha kuwa fedha zimetengwa kulingana na majukumu (*finance follows functions*), Serikali imeamua kutekeleza uamuzi wake wa kupeleka madaraka kwa wananchi kwa kuhamisha fedha, rasilimali watu, pamoja na vitendea kazi kutoka Wizarani kwenda kwenye Halmashauri;

Katika kutekeleza uamuzi huo, makadirio ya fedha ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo kwa mwaka 2007/2008 zimeongezeka kwa asilimia 46 ikilinganishwa na mwaka 2006/2007;

- (v) Serikali itaendelea kuhimiza Halmashauri kutoa taarifa za mapato na matumizi na kuhamasisha wananchi kuhoji matumizi ya Halmashauri kila mgao wa fedha unapokwenda kwenye Halmashauri hizo; na
- (vi) Serikali itaendelea kujenga uwezo wa Halmashauri kwa kutoa ruzuku ya maendeleo ya uwezeshaji (*capacity building grant*). Mafunzo haya yatahusisha ngazi zote za Halmashauri mpaka watendaji wa Vijiji/Mitaa.

Mheshimiwa Spika, mchango wa Sekta binafsi katika kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi ni muhimu sana. Kama nilivyoeleza katika Hotuba ya Bajeti, Serikali iko wazi kwa sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa barabara kwa mpango wa *Build Own, Operate and Transfer (BOOT)*. Hii ni moja ya malengo makuu ya kutungwa kwa Sheria mpya ya barabara ambayo ilipitishwa na Bunge hili Aprili, 2007.

Mheshimiwa Spika, misaada na mikopo itengwe kwenye sekta ambazo zitatuwekea uwezo wa kujitegemea. Kwa mwaka wa fedha 2007/2008, tunatarajia kupata misaada na mikopo nafuu ya jumla ya Shilingi bilioni 2,549.249.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 881.320 ni misaada na mikopo ya ki-bajeti, Shilingi bilioni 273.194 ni misaada na mikopo ya ki-sekta Shilingi bilioni 1,188.698 ni misaada na mikopo inayokwenda moja kwa moja kwenye miradi na shilingi bilioni 206.037 ni misamaha ya madeni.

Misaada na mikopo hii imeelekezwa kwenye sekta za kipaumbele ambazo zinaweza kutujengea uwezo wa kujitegemea. Sekta zilizopewa kipaumbele ni Elimu asilimia 18, Miundombinu asilimia 12.8, Afya asilimia 10, Kilimo asilimia 6.2 na maji asilimia 5.1. Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa misaada na mikopo inaelekezwa kwenye maeneo na sekta za kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa shughuli za manunuza katika taasisi za umma hasa Serikali za Mitaa. Misaada na mikopo itengwe kwenye sekta ambazo zitatuwekea uwezo wa kujitegemea. Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuza wa Umma imeandaa utaratibu wa kudhibiti na kukagua shughuli za ununuza za taasisi za umma. Chini ya utaratibu huo kila taasisi itakuwa inawakilisha kwa Mamlaka mpango wa manunuza wa mwaka na ripoti za utekelezaji wa mpango huo kila mwezi. Mamlaka nayo itatumwa wakaguzi kwenda kwenye taasisi kufanya ukaguzi wa taarifa zilizowasilishwa.

Vile vile, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuza wa Umma imekuwa ikiendesha mafunzo kwa Watendaji wa Taasisi za Umma kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Ununuza na Kanuni zake. Katika mwaka wa fedha ujao mkazo utawekwa kuwaelimisha watendaji wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iruhusu sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa barabara ili kuongeza kasi ya upatikanaji wa miundombinu hiyo muhimu.

Mchango wa Sekta binafsi katika kuongeza kazi ya ukuaji wa uchumi ni muhimu sana, kama nilivyoeleza katika Hotuba ya Bajeti, Serikali iko wazi kwa sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa barabara kwa mpango wa *Build Own, Operate and Transfer (BOOT)* kama nilivyo sema hapo mwanzo na kama alivyosema Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Hii ni moja ya malengo makuu ya kutungwa kwa Sheria mpya ya barabara, ambayo ilipitishwa na Bunge hili mwezi Aprili, 2007. Kwa hiyo nawaomba Waheshimiwa Wabunge kusaidiana na Serikali kutafuta wawekezaji walio tayari kushiriki katika mpango huo.

Mheshimiwa Spika, SMZ kuwa na *access* ya mikopo moja kwa moja hasa mikopo nafuu ya Benki ya Dunia. Kwa utaratibu uliopo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaweza kuzungumza na Wahisani moja kwa moja kwa lengo la kupata misaada (*grants*). Kuhusu mikopo, Serikali ya Muungano kwa niaba ya SMZ huongea na wahisani ili kupata mikopo nafuu ya kutelekeza miradi mbalimbali ya maendeleo. Ili kufanikisha jukumu hili kuhusiana na mradi upande wa Zanzibar, Wizara ya Fedha ya Serikali ya Muungano hushirikiana nyema na Wizara ya Fedha na Uchumi ya SMZ pamoja na sekta zinazohusika kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pamoja na misaada inayoweza kutolewa kwa SMZ moja kwa moja, SMZ inapata gawio la asilimia 4.5 ya fedha za misaada ya Bajeti inayotolewa na wafadhili mbalimbali kwa nchi yetu. Benki ya Dunia chini ya mpango wa pili wa kusaidia kupunguza umasikini (*Poverty Reduction Support Credit II*) ilitoa msaada (*grant*) wa Dola za Kimarekani milioni 90 kati ya Dola za Kimarekani milioni 150 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya mpango huo. SMZ ilipewa gawio la asilimia 4.5 ya kiasi hicho. Baada ya mpango huu wa pili, Tanzania haikuendelea tena kupewa misaada (*grants*) na Benki hiyo kutokana na deni lake kuwa katika kiwango kinachohimilika.

Aidha, SMZ imeendelea kupata fedha kutoka Benki ya Dunia kwa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ile yenye sura ya Kitaifa kama vile *Tanzania Social Action Fund (TASAF)*, *Participatory Agricultural Development and Empowerment Project (PADEP)*, na *Marine and Coastal Environmental Management Project (MACEMP)*. Chini ya miradi hii SMZ imetengewa fedha kama ifuatavyo:-

<i>TASAF II,</i>	Dola za Kimarekani milioni 2.5
<i>PADEP,</i>	Dola za Kimarekani milioni 4.5
<i>MACEMP,</i>	Dola za Kimarekani milioni 3

Mheshimiwa Spika, SMZ vile vile inatarajia kupata mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Kimarekani milioni 42 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya *Zanzibar Basic Education Improvement Project*.

Mkataba kwa ajili ya mradi huu unatarajiwa kusainiwa tarehe 25/06/2007 huko Zanzibar. Kwa hiyo, *SMZ* itaendelea kufaidika na mikopo ya Benki ya Dunia na wafadhili wengine kufuatana na miradi itakavyokuwa inaibuliwa kwa mujibu wa malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA).

Mheshimiwa Spika, je, Mpango wa *MMC* umezingatia mradi wa maji wa Geita?

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Geita ni moja ya miradi inayotarajiwa kufadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia shirika lake la *Millenium Challenge Corporation (MCC)*.

Uchambuzi wa mradi huu umesafanywa na kuwasilishwa *MCC*. Ni matarajio yetu kwamba katika *Compact Programme* ya *MCC* inayoandalishiwa na mkataba wake unaotarajiwa kusainiwa kabla ya mwezi Desemba, 2007, utakuwa umezingatia mahitaji ya mradi huu. Kiasi kitakachokuwa kimetengwa kwa ajili ya mradi huu kitafahamika baada ya mkataba kusainiwa.

Mheshimiwa Spika, malipo ya pensheni kupitia mifuko mbalimbali ya jamii ni sahihi, ila elimu kwa wastaifu itolewe. Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na mifuko ya jamii itawaelimisha wananchi wote kwa ujumla wakiwemo wastaifu wenye na wadau wengine kwa kutumia matangazo kwenye vyombo vya habari, vituo vya redio zilizoko mikoani, mbao za matangazo, magazeti, vipeperushi na katika maonyesho ya kitaifa sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaanza kutoa taarifa wakati wastaifu watakapokuwa wanalipwa pensheni yao ya mwezi wa Saba 2007, ambapo Benki zinazolipa na Hazina Ndogo katika mikoa yote watahusika. Shughuli hizi pamoja na uratibu, uhakiki wa mifuko yenye kazi zitafanyika katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2007.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha viwango vya pensheni kwa wastaifu kadri muda unavyopita, hasa kwa wale walio nje ya utaratibu wa mifuko ya hifadhi ya jamii kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, viwango vya pensheni vimekuwa vikifanyiwa marekebisho mara kwa mara, kwa kadri uwezo wa Serikali unavyoongezeka. Utaratibu huu utaendelea kutumika kila hali inaporuhusu.

Mheshimiwa Spika, suala la pensheni kwa wastaifu ni suala zito sana katika menejimenti ya uchumi. Kwa upande mmoja linahusu mishahara na huduma nyinginezo anazopewa mtumishi katika kipindi chake cha utumishi na kwa upande mwagine tunalazimika kuzingatia akiba iliyopo kwa ajili ya kulipia uzalishaji uliofanyika siku za nyuma.

Katika hali hii, pensheni kwa vizazi vilivytangulia hazina budi kuzingatia uwezo wa kizazi kipyta, pamoja na mahitaji ya kudumu kwa kizazi hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili hii, marekebisho makubwa ya mfumo wa hifadhi ya jamii, ikiwemo viwango vya pensheni, hayana budi kuangaliwa na utafiti wa kina ilikuwa na uwiano mzuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali itenye fedha maalum kwa ajili ya Mikoa iliyo nyuma Kimaendeleo. Nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna Mikoa ambayo iko nyuma kimaendeleo kwa vigezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa MKUKUTA *Annual Progress Report* pamoja na Taarifa ya Hali ya Umaskini (*PHDR*) unaonyesha kuwa mikoa tofauti iko nyuma kimaendeleo kutegemea kigezo kinachotumika.

Mheshimiwa Spika, Mkoa ulio nyuma kwa kigezo cha umaskini wa kipato unaweza ukawa sio maskini kwa kigezo cha huduma za jamii na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatuna budi kuzingatia vigezo vinavyotumika kupima umaskini ili kuweka mkakati sahihi wa jinsi ya kuondoa umaskini huo.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ya hoja za Waheshimiwa Wabunge walipojadili bajeti ya mwaka 2006/2007 alilikumbusha Bunge lako Tukufu utaratibu unaotumika kugawa fedha kwa ajili ya Halmashauri za Wilaya na sababu zilizosababisha kuwa na utaratibu maalum.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ultokana na hisia zilizo jitekeza miaka ya nyuma kwamba ugawaji uliokuwepo hapo mwanzo haukuwa na misingi ya haki na usawa, haukuzingatia mikoa na Halmashauri zilizo nyuma kimaendeleo na hivyo tukakubaliana kuwa na njia mbadala.

Mheshimiwa Spika, vigezo vinavyotumika kugawa rasilimali vinazingatia kielelezo cha umaskini katika mkoa au Halmashauri husika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lengo ni kuboresha ugawaji wa rasilimali na kuondoa kasoro zilizokuwepo. Kama Bunge lako linadhani kuna utaratibu mwingine mzuri zaidi, Wizara yangu iko tayari kupokea maoni hayo na kuyafanya kazi kadri itakavyooneka inafaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipokea taarifa kutoka Mikoa mbalimbali kuitia Wizara ya Miundombinu ikionyesha uharibifu wa barabara nyingi katika Mikoa husika.

Mheshimiwa Serikali iliagiza kuwa pale matengenezo yatakapofanyika na muda wa kumlipa mkandarasi umefika, *Certificate* ya maombi ya fedha iletwe Hazina ili kuweza kutoa fedha. Wizara ya Fedha iliagiza kuwa fedha zitatolewa kulingana na kazi iliyofanyika na sio vinginevyo. Mpaka leo Wizara ya Fedha imeishatoa jumla ya Shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya matengezo ya barabara.

Mikoa iliyowasilisha “*Certificate*” zao Wizara ya Mindombinu na kuletwa Hazina kwa ajili ya kutoa fedha ni kama ifuatavyo:-

<b>MKOA</b>	<b>KIASI CHA FEDHA</b>
Pwani	372,374,000.00
Singida	478,413,000.00
Tabora	757,403,594.00
Kagera	99,298,667.50
Kigoma	123,184,615.00
Kilimanjaro	42,363,900.00
Manyara	112,424,716.00
Tanga	167,761,502.00
Iringa	234,503,956.80
Shinyanga	135,367,078.75
Mara	216,766,277.50
Dodoma	124,680,600.00
Lindi	104,117,460.00
Mtwara	179,874,000.00
Mwanza	53,212,500.00
Morogoro	289,722,000.00
Dar es Salaam	309,593,185.00
<b>Jumla</b>	<b>3,801,061,052.55</b>

Mheshimiwa Spika, napenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa fedha za Sekta ya maji zinakuwa kwenye Wizara husika. Kwa mwaka 2006/2007 Bunge letu lilipitisha Mradi wa *Rural Water Supply and Sanitation* fungu 49 kifungu kidogo cha 4001 wenye kiasi cha shilingi 21,965.7 milioni ikiwa mkopo toka *African Development Bank (ADB)*. Jina la *Quick Wins* lilitumika kuelezea mradi huu likiwa na maana kwamba utekelezaji wa mradi ungeleta maendeleo ya haraka katika maeneo yanayohusika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha taratibu zote, nchi yetu imepokea fedha za mradi huu tarehe 14 Juni, 2007 katika Akaunti ya mradi husika. Tarehe 19 Juni, 2007 *Thematic Working Group* ya Sekta ya Maji ilikutana na kukubali kuhamisha fedha hizo kwenda Benki Kuu kwenye Akaunti ya Serikali. Kwa kuzingatia hali hiyo, fedha hizo zilikuwa hazijaletwa Hazina kwa ajili ya kutumwa kwenda kwenye Halmashauri husika.

Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa mara utaratibu wa kuzihamisha utakapokuwa tayari zitakwenda mara moja.

Mheshimiwa Spika, uhamisho wa fedha kati ya fungu na fungu au ndani ya fungu (*Reallocation*) kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo, Waziri wa Fedha amepewa madaraka ya kuhamisha fedha ndani ya fungu ambayo hayatazidi kiwango kilichoidhinishwa na Bunge kutumika kwa mwaka husika. Sheria hii iliwekwa ili kukidhi dharura zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, siamini kuwa itakuwa busara kuitisha Bunge kwa ajili ya kufanya uhamisho wa fedha pindi ukame, njaa au dharura inapotokea. Sheria ilipitishwa ili kuiwezesha Serikali kufanya kazi kwa kuzingatia mahitaji halisi ya fedha ndani ya Ofisi.

Mheshimiwa Spika, naomba ieeweke kuwa uhamisho huu hufanywa kwa mambo ambayo ni ya dharura na muhimu tu na sio kwa kila kitu. Kwa kuelewa umuhimu wa kulishirikisha wa Bunge katika kusimamia matumizi ya rasilimali za Taifa, Sheria hiyo inamtaka Waziri wa fedha kuwasilisha taarifa ya uhamisho alioufanya kwa ajili ya kuidhinishwa. Ieeweke kuwa kinachofanyika ni kufanya uhamisho kukidhi mahitaji ya dharura tu.

Mheshimiwa Spika, Fedha za Maendeleo zinazotengwa kwenye bajeti zinagawanywa kwenye makundi mawili yaani zinazotokana na mapato yetu ya ndani na fedha kutoka nje ya nchi yaani zinazotolewa na wafadhili.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za ndani, Serikali inajitahidi sana kutoa fedha zote kama zilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu isipokuwa pale ambapo Mapato ya ndani yanapungua na hivyo kupunguza uwezo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha kutoka nje, hatuna matatizo na fedha zinazotolewa na wafadhili wetu kwa utaratibu wa mfuko wa pamoja *Basket Fund* na *General Budget Support (GBS)*. Fedha za Maendeleo kutoka kwa Wafadhili zinazotuleta matatizo na kuleta hoja nyingi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge hasa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*) ni zile zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi (*Direct to Project Fund – D Funds*), bila kupitia kwenye utaratibu wa Serikali (*Exchequer*).

Mheshimiwa Spika, fedha zinazoletwa kwa utaratibu huu hupelekwa moja kwa moja kwenye Miradi, kwa njia ya vifaa, huduma na mara nyingine fedha. Hazina huwa haina taarifa ya kupokelewa kwa vifaa au huduma hizo na kushindwa kuziweka kwenye vitabu vyta Serikali, kwa sababu ya kukosa taarifa ya kupokelewa kwa vifaa/huduma hizo.

Kwa vifaa au huduma zinazopokelewa na taarifa kuleta Hazina, Vifaa na huduma hizo hurekebishwa baadaye katika vitabu vyta Serikali na ndiyo maana huwa inapelekwa *PAC* na kuonekana kwamba fedha zile kama bado hazijaingia katika Mfuko wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili linatokana na Wafadhili wetu kutotoa nyaraka zinazoonyesha thamani ya vifaa na huduma wanazozipeleka moja kwa moja kwenye miradi na hivyo uongozi wa Wizara/Idara/Mikoa inayopokea vifaa na huduma hizo kutokuwa na uwezo wa kutoa taarifa Hazina kwa kukosa nyaraka.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili limesababisha kumbukumbu zilizoko Hazina kuonyesha kuwa fedha kutoka nje ya nchi hazikupokelewa na kuleta maswali mengi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wanapopitia Hesabu za Wizara/Idara na Mikoa.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya vifaa na huduma huwa vimepokelewa, lakini upatikanaji wa taarifa na nyaraka ni chanzo kikubwa kinachosababisha fedha hizo zioneokane hazikutolewa.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kutatua tatizo hili, Serikali imekuwa ikiwashawishi wafadhili kuleta taarifa ya vifaa na huduma wanazozipeleka moja kwa moja kwenye miradi, ili taarifa hizo zitumike katika ufuutiliaji wa nyaraka kwenye miradi husika na hivyo kuwezesha kurekodi kwenye vitabu vyta Serikali.

Mheshimiwa Spika, wafadhili walikubali kutoa taarifa hizo, lakini bado utekelezaji haujaza matokeo mazuri. Serikali itaendelea juhudi za kuwashawishi Wafadhili kutoa taarifa Hazina kila wanapotuma vifaa na huduma moja kwa moja kwenye miradi ili kuwezesha fedha hizo kuingizwa kwenye vitabu vyta Serikali na hivyo kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge na Serikali kuwa na kumbukumbu zilizokamilika.

Mheshimiwa Spika, faida inayotarajia kupatikana kwa kuhamishia ulipaji wa mafao ya wastaifu kwenye mifuko.

Uamuzi wa Serikali wa kuhamishia utoaji wa huduma kwa Wastaifu kwenye mifuko utatarajiwa kuwa na baadhi ya faida zifuatazo:-

- (a) Watumishi wa mifuko ni wataalamu waliobobe kutoa huduma bora kwa wastaifu kwani ni taaluma waliyosomea, tofauti na watumishi wa Hazina wanaotoa huduma hiyo sasa amba ni wataalam katika fani ya Uhasibu. Kwa kuhamishia huduma ya wastaifu kwenye mifuko, wastaifu watapata huduma bora zaidi.
- (b) Utoaji wa huduma kwa wastaifu kuitia mifuko ya pensheni kutapunguza muda unaotumika kuandaa malipo hadi kulipa mafao ya mstaa fu na hivyo kumwondolea kero mstaa fu.
- (c) Wastaifu watafaidika na riba inayotolewa na mifuko.
- (d) Uboreshaji wa mafao kwa wastaifu utakapotokea utawahusisha wastaifu wote wanaohudumiwa na mifuko husika na sio wastaifu wa serikali tu.

- (e) Hazina itabaki na jukumu la Usimamizi wa Mifuko hii badala ya hali ilivyo sasa, yaani kusimamia na kuwa Mlipaji wa mafao. Hivyo usimamizi wa mifuko utakuwa wa ufanisi zaidi na hivyo kuboresha huduma kwa Wastaifu.
- (f) Baadhi ya wastaifu walikuwa wanalipwa mafao yao sehemu mbili tofauti yaani kwenye mifuko na Hazina. Katika utaratibu huu wa kulipwa mafao yao na mifuko, usumbufu wa kufuutilia malipo sehemu mbili tofauti utaondolewa kwa kulipwa sehemu moja tu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya mifuko hii haijanza kutoa huduma kwa Wastaifu, mifuko itafungua ofisi katika maeneo ambayo hawana ofisi ili kuwezesha utoaji wa huduma uwe wa kiwango tunachotarajia. Baadhi ya mifuko inazo ofisi kwa kila Mkoa na baadhi wanazo ofisi katika Kanda.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ufunguaji wa ofisi, mifuko hii kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Wadau wengine, itatoa elimu kwa Watanzania wote kuhusu mabadiliko ambayo yanafanyika ikiwa ni pamoja na faida ya kuhamishiwa kwenye mifuko. Hivyo maandalizi yote ambayo ni ya lazima na muhimu yatafanyika kabla ya huduma kuanza kutolewa na mifuko.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa hatua ambazo zinatakiwa kuchukuliwa dhidi ya wale wote wanobainika kuiba fedha za Umma, kila Afisa Mhasibu anapaswa kutoa taarifa za wizi na ubadhilifu kwenye vyombo vyaya dola mara wizi au ubadhirifu unapogunduliwa ili sheria ichukue mkondo wake.

Baada ya taarifa hiyo kutolewa, ni wajibu wa Afisa Mhasibu Mhusika kufuutilia kwa karibu ili kujua hatma ya kesi zote ambazo zipo Mhakamani. Maafisa Wahasibu wanapaswa kutoa taarifa ya hatua zote zinazochukuliwa kwenye mamlaka zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, kwa Maafisa wote wanaohusika na uzembe, au kushindwa kuwajibika katika maeneo yao ya kazi, kanuni za fedha zinawapa maafisa Wahasibu uwezo wa kutoa adhabu. Kanuni hizi za fedha zinatakiwa zitumiwe ipasavyo katika usimamizi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji wa mishahara ya Wahasibu na Wakaguzi, inategemea sana uwezo wa Serikali wa kukusanya mapato ya ndani. Wahasibu na Wakaguzi wa ndani mishahara yao huboreshwa sambamba na mishahara ya watumishi wengine wote wa Serikali.

Hata hivyo kutokana na umuhimu wa kazi za Uhaisibu na Ukaguzi wa ndani, Serikali ilipandisha hadhi za vitengo vyya Uhaisibu na Ukaguzi wa ndani kuwa idara kamili kuanzia Julai, 2007. Aidha, Serikali iliboresha mishahara ya Wahasibu Wakuu wote na Wakaguzi Wakuu wa Ndani wa Wizara/Idara za Serikali Kuu kuwa kwenye ngazi ya *TGS K.*

Mheshimiwa Spika, Serikali bado inaendelea na utaratibu wa kuboresha mishahara ya Wahasibu na Wakaguzi wengine wallobaki. Nia ya Serikali ni kuboresha mishahara ya Watumishi wake wote, lakini kikwazo kikubwa ni uwezo mdogo tulionao wa kuwa na bajeti tegemezi.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa fedha kwenye Halmashauri na uwingi wa akaunti wanazoshindwa kuzisimamia. Ni ukweli ulio wazi kwamba karibu Halmashauri zote zina akaunti nyingi ambazo zinawaleta matatizo ya namna ya kuzisimamia na kuzifanya Usuluhihi wa Hesabu za Benki.

Mheshimiwa Spika, uwingi wa akaunti unatokana na uamuza wa kuwa na akaunti kwa kila sekta kama vile maji, afya, barabara, elimu na kadhalika. Achilia mbali akaunti za matumizi ya kawaida na Amana ambazo fedha zake zinapalekwa kwenye Halmashauri. Aidha, miradi inayofadhiliwa na wafadhili hufunguliwa akaunti moja kwa kila mradi kutokana na matakwa ya wafadhili. Utaratibu huu umesababisha Halmashauri kuwa na utitiri wa akaunti ambazo inawawia vigumu kuzisimamia na kutoa mwanya wa kuweza kutumika vibaya na baadhi ya watumishi wasiokuwa waaminifu.

Mheshimiwa Spika, katika Serikali Kuu miaka ya kabla ya 2000 kulikuwa na tatizo kama hili lakini lilitatuliwa baada ya Serikali kuamua kufunga baadhi ya akaunti na kubakiza zile tu ambazo zilikuwa muhimu. Uamuza huu umeisaidia sana Serikali Kuu kuwa na akaunti ambazo ni rahisi kuzisimamia. Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI tutakaa na kulitafutu ufumbuzi tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wastaafu wa iliyokuwa Jumuia ya Afrika Mashariki, ni kwamba sio wote waliowahi kufanya kazi katika jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika, walikuwa wanahuksika au kustahili malipo ya mafao ya jumuiya hiyo. Malipo haya yaliwhusu wale tu ambao walikuwa katika ajira tarehe 30, Juni, 1977 wakati Jumuia ya Afrika Mashariki inavunjika.

Ni kweli pia kuwa malipo haya yalitegemea zaidi kumbukumbu binafsi zilizopatikana katika majalada ya kila mtumishi binafsi. Baada ya uchambuzi wa zaidi ya majalada 44,807, yalipatikana majalada 31,612 ambayo wastaafu walikuwa wanastahili kulipwa mafao haya kufuatana na vigezo vilivyokuwa vimewekwa na muongozo wa *BLM* na hati ya makubaliano (*Deed of Settlement*). Matangazo mbalimbali yamekuwa yakitolewa tangu tulipoanza malipo mpaka sasa, kwa madhumuni ya kuwataarifu wastaafu na umma kwa ujumla juu ya taarifa mbalimbali za utekelezaji na mabadiliko yanayojitokeza kila kunapokuwa na mabadiliko katika taratibu za malipo hayo.

Mheshimiwa Spika, taarifa kwenye matangazo hayo ilihu pia majalada yalikuwa na nyaraka pungufu na kuwataka wastaafu wenye uwezo wa kukamilisha nyaraka za madai yao waweze kufanya hivyo, kwa lengo la kukamilisha taratibu za malipo. Kukosekana kwa majalada kwenye mashirika ya iliyokuwa jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika, ilikuwa ni sababu kuu ya kutokamilika kwa taratibu za malipo ya wastaafu hao. Aidha, kushindwa kwa mashirika husika kuzithibitisha nyaraka za

wastaafu na kuziwasilisha Hazina katika muda uliotakiwa ni sababu nyingine kubwa iliyooungeza ugumu wa kushughulikia madai ya wastaafu.

Mheshimiwa Spika, idadi iliyowasilisha na Dr. Umbritch kwa ajili ya malipo ilikuwa ni 28,831. Lakini baada ya uchambuzi, Serikali imelipa jumla ya wastaafu 36,405 hadi kufikia tarehe 20/06/2007. Katika idadi hiyo, malipo ya mirathi ni 7,666, na malipo mapya ni 4,793. Bado wastaafu 6,888 kati ya idadi ya waliolipwa, hawajajitokeza kuchukua mafao yao licha ya majina yao kutangazwa kwenye magazeti mara kadhaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali bado inaendelea kuwahudumia wastaafu katika kituo cha kutoa huduma kupitia ofisi za Mtaa wa Mkwepu kwenye jengo la Posta mkabala na Benki ya Posta. Tunaendelea kupokea nyaraka, malalamiko ya wastaafu na huduma ya kutoa hundi za malipo. Aidha, huduma hiyo hutolewa katika ofisi za Hazina katika jengo la Sukari ghorofa ya tano. Mstaafu yejote mwenye matatizo ya malipo anaombwa kuwasilisha madai yake katika mojawapo ya ofisi nilizozitaja hapo juu. Kwa wale walioko Mikoani wawasilishe madai yao kwenye ofisi za Hazina ndogo katika Mikoa yao.

Mheshimiwa Spika, Vitengo vya Ununuzi kuwa Vitengo vinavyojitegemea katika Wizara na Taasisi za Umma, Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004 imainishwa kuundwa kwa vitengo vya ununuzi ambavyo vinajitegemea na vitakavyokuwa vinasimamia shughuli zote za manunuzi za taasisi husika. Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma inafuatilia utekelezaji wa sheria kwa kuhakikisha kuwa kila taasisi inaunda vitengo hivyo na pia itahakikisha kuwa vitengo hivyo vina wafanyakazi na vitendea kazi vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna baadhi yenu mmekuwa mkiuliza hoja ni ipi? Hoja ni ya kupitisha bajeti. Ndiyo hoja. Ndani yake kuna Mpango. Kwa hiyo, tutakapomaliza kitakachopigiwa kura ni hoja ya bajeti ambayo ikikubalika maana yake na ule Mpango wa Serikali umekubalika.

Kwa hiyo, hoja kuu ni moja nayo ni bajeti na sasa namwita Mtoa hoja hiyo kuu ambayo ni Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa Naibu Spika na pia Mwenyekiti Mheshimiwa Jenista Mhagama, kwa jinsi mlivyosimamia na kuongoza Bunge wakati wa majadiliano ya hoja ya Serikali niliyoitoa tarehe 14 Juni, 2007 kuhusu Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2007/2008.

Aidha, nawashukuru kipekee, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi - Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kuwasilisha kwa ufasaha maoni ya Kamati yake. Vile vile, namshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Msemaji Mkuu wa Kambi hiyo katika masuala ya fedha -

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi na pia Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto - Mbunge wa Kigoma Kaskazini, ambaye ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu masuala ya Mipango na Uchumi, kwa maoni na ushauri wao juu ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niwashukuru wote waliochangia kwa njia mbalimbali, wakiwemo wale waliota maoni yao kwa kuzungumza hapa Bungeni, waliota maoni yao kwa maandishi na wale waliota maoni yao nje ya Bunge hili walikuwa wameeleza maoni yao, wote nasema kwamba michango yao ni mizuri ambayo kwa kweli kama vile ninavyosema siku zote itatusaidia sana katika utekelezaji wa Bajeti hii, pia katika kuandaajaa bajeti za siku za usoni. Kwa hiyo, nasema ahsanteni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri Ngasongwa ametaja majina yote ya wale ambaa waliozungumza na kuandika na naomba nichukuliwe kama vile mimi pia nimetaja. Lakini nimepata *vi-note* hapa kwamba kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge majina yao hayakutajwa. Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya, amechangia kwa maandishi, naye hakutajwa. Mheshimiwa Zulekha Haji - Mbunge wa Viti Maalum alitoa mchango wake kwa maandishi na pia napenda kurekebisha kuwa aliyechangia ni Khadija Salum Ally-Qassmy na sio Khadija Salehe Ngozi. Kama kuna wengine waliochangia na majina yao hayakuwekwa, basi tunaomba watuandikie na tutayachukua na kuyaingiza kwenye *Hansard* naamini.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inathamini michango yote ya Waheshimiwa Wabunge na inaichukua kama nyenzo muhimu ya kuboresha utekelezaji wa Bajeti hii ili malengo yake yafikiwe.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe maelezo kuhusu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Napenda kusema kwamba nitakuwa najidanganya au tunajidanganya nikisema kwamba hoja zote nitaweza kuzijibu katika muda huu mfupi. Kwa hivi nitakachofanya ni kwamba kwa hoja zote tutatengeneza majibu na Waheshimiwa Wabunge watapata maelezo hayo kwenye kijitabu.

Napenda pia kwa mara nyingine nitoe shukrani za dhati kwa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa maoni na ushauri wake ambaa unaipa Serikali changamoto na ari ya kufanya vizuri zaidi na zaidi ili kupata matokeo yanayotarajiwa na wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya maoni na mapendekezo yaliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, yalijadiliwa Dar es Salaam tulipokutana na Kamati na kwa kweli tumeyazingatia katika bajeti hii.

Mapendekezo ya Kamati ambayo Serikali imeyazingatia moja kwa moja katika bajeti hii ni pamoa na umuhimu wa kuimarisha usimamizi wa matumzi ya fedha katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa; kufuatilia matokeo ya matumizi ya fedha katika

Halmashauri, ushirikishwaji wa wananchi katika mipango na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, pamoja na suala zima la uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati uliotolewa Bungeni kuhusu umuhimu wa kuongeza ushindani katika biashara ya mafuta ili kupunguza makali ya ongezeko la bei ya mafuta pia umezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, yapo pia maoni ya Kamati kuhusu udhibiti katika kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzio visivyo vya kodi, kusimamia kanuni na taratibu za ununuzi wa umma.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuboresha mifuko ya dhamana kwa ajili ya kuwezesha wananchi kupata mikopo, kuharakisha upatikanaji wa mikopo ya nyumba na ya kukodi rasilimali; maoni kuhusu kodi ya mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa, pamoja na ada ya leseni za magari, ambayo yamechangiwa pia na Waheshimiwa Wabunge wengi, yote tumeyazingatia.

Aidha, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi alishauri kwamba utaratibu wa misamaha ya kodi za mafuta, gesi na misamaha mingine ziangaliwe upya kwa lengo la kuziba mianya ya kukwepa kodi. Hili pia limezingatiwa kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imeishauri Serikali ichukue hatua za kupunguza makali yanayoweza kutokea kutohana na ongezeko la kodi ya mafuta, hasa petroli na dizeli. Napenda kulihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba ushauri huu pia utazingatiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya 2007/2008 Serikali imejikita katika mambo makuu manne au matano:-

(i) Jambo la kwanza ni kuongeza mapato ya ndani ili kuimarisha uwezo wa Taifa wa kugharamia vipaumbele katika maendeleo ya nchi yetu.

Dhana kubwa hapa ni kwamba mahitaji ya msingi yagharamiwe na mapato yetu wenywewe na misaada na mikopo ya nje iwe inajazia pale ambapo uwezo wetu umefikia kikomo, hasa kuwekeza kwenye vipaumbele vitakavyoibua maendeleo na kutuwezesha kujitegemea siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, hakuna jambo zuri kama suala la kujitegemea. Kwa sababu tunapopanga hapa barabara kama tunategemea Wahisani, kama kuna mabadiliko yoyote hata uchaguzi nakumbuka wakati ule Canada tulipanga, lakini kulikuwa na uchaguzi Canada kukatokea na mabadiliko fedha hazikuja kwa wakati. Tunapanga hapa ndio ukweli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tujaribu kujitegemea fedha zetu wenywewe tutumie kwa ajili ya maendeleo yetu, fedha zetu wenywewe tutumie kwa ajili ya barabara zetu.

Kwa hivyo basi, kwa mara ya kwanza katika historia yetu mapato ya ndani yanaongezeka kwa zaidi ya asilimia 30, na yanafikia asilimia 18 ya Pato la Taifa. Ingawa ongezeko hili bado halitufikishi katika kiwango kinachotosheleza mahitaji, kinachokadiriwa kuwa shilingi trilioni 12 kwa mwaka wa 2007/2008, ongezeko hili ni hatua kubwa. (*Makofi*)

Bajeti hii pia inalenga kuharakisha utekelezaji wa mpango wa awamu ya Pili wa Mageuzi katika Sekta ya Fedha – hasa sekta ndogo ya benki, ambayo kwa kweli ni chanzo kikubwa cha mapato kwa njia ya amana za wananchi, na mikopo kwa wajasiriamali. Hivi sasa amana *deposits* au amana kwenye vyombo vya fedha nchini zinafikia shilingi trilioni sita, ambazo kama zikikopeshwa kwa wajasiriamali na wananchi ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya nchi. Hili ndilo tunali-*address* katika Bajeti hii.

Jambo la pili kubwa katika Bajeti hii ni kuzingatia vipaumbele vichache ambavyo vimepatiwa mgao mkubwa, - elimu, miundombinu, afya, kilimo na maji. Vipaumbele hivi ni msingi mkubwa wa kuchochea maendeleo ya nchi yetu, kama yalivyoainishwa katika MKUKUTA na katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi. (*Makofi*)

Jambo la tatu kubwa ni kwamba tumedhamiria kwa dhati kutokukopa kutoka soko la fedha la ndani kupitia dhamana za Serikali, na kwa maana hiyo kupunguza ushiriki wa Serikali katika soko hili. Kamati iliyoundwa ya kusimamia mzunguko wa fedha za Serikali (*Cash Management Committee*) itashauri kuhusu maboresho yanayotakiwa katika uendeshaji wa soko la fedha na dhamana (*treasury bill market*), kwa lengo la kushusha riba katika soko hilo na hatimaye kushusha riba za mikopo zinazotozwa na vyombo vya fedha. Serikali ndiyo mkopaji mkuu. Trilioni 6.0 kama Serikali haita kopa Mabenki haya itabidi wakopeshe na watakopesha wapi? Itabidi kuwe na ushindani na kwa maana hiyo hata kushusha riba. Itabidi wakoposhe kwa wananchi na kwa wajasiliamali na ndiyo maana Serikali imeamua kwa kipindi hiki kwamba isikope. (*Makofi*)

Jambo kubwa la nne katika Bajeti hii ni kupeleka madaraka, pamoja na raslimali fedha na raslimali watu kwa wananchi kwa njia ya “*D by D*”. Sambamba na hatua hii, Serikali, kupitia Bajeti hii ya 2007/2008, inaendelea kuimarisha uwezo wa Halmashauri wa kupanga na kusimamia mapato na matumizi ya umma. Hili limekuwa tatizo lakini tutalifanya na tunaamini kwamba fedha zikienda kwa wananchi maendeleo makubwa yataweza kupatikana hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kuzipatia Halmashauri wataalam wa Uhaisibu na Ukaguzi, kusomesha wataalam wa ununuzi wa umma, kuzipatia Halmashauri vitendea kazi, na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo tumeliangalia katika Bajeti hii ni kupunguza kodi kwa wafanyakazi wa kipato cha chini pamoja na nyongeza ndogo ya mishahara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niliona nifafanue haya mambo makubwa kwa kuwa wakati wa kujadili Bajeti hii, nilihisi kwamba baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa hawakupata uelewa sahihi kuhusu maudhui na mwelekeo wa Bajeti ya 2007/2008. Kwa

mfano, kuna Waheshimiwa Wabunge kutoka Kambi ya Upinzani waliosema kwamba Bajeti ya 2007/2008 ni marudio tu ya Bajeti zilizopita.

Hii sio kweli hata kidogo! Pamoja na mambo haya manne makubwa niliyosema, ni vizuri tuwe wakweli na tukubali kwamba kwa mara ya kwanza, matayarisho ya Muongozo wa Bajeti ya 2007/2008 yalihusisha Waheshimiwa Wabunge na kwamba maoni yao yamezingatiwa katika Bajeti hii. Bajeti hii pia kwa mara ya kwanza imetambua umuhimu wa Bunge kuwa na Mfuko wake (*National Assembly Fund*) badala ya Fungu (*Vote 42*); mfuko ambao utasimamiwa moja kwa moja na Ofisi ya Spika. (*Makofsi*)

Aidha, Bajeti hii imezingatia matayarisho ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ambao kama nilivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu ataeleza tunaamini kwamba Mfuko huu utasaidia sana maendeleo yetu. Haya sio mambo ya marudio, ni mapya kabisa.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutumia fursa hii kusema kwamba Serikali imesikitika jinsi baadhi ya vyombo vya habari vya Tanzania vilivyopotosha dhana nzima ya Bajeti hii. Badala ya kusaidia wananchi kuilewa Bajeti hii vyombo hivyo vya habari vimewapotosha, na kuwachochea walalamike.

Tokea nilivyosoma Bajeti siku ya Alhamis, Ijumaa, Jumamosi, Jumapili yote yaliyoandikwa ni kuchochea na sio sahihi hata kidogo! Kama nilivyoeleza na kuibua yale ambayo tuliyoyazungumza wamechukua jambo moja lakini badala ya kuelimisha wananchi hawakufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza pia kwamba vyombo vya habari vya nje vimeielezea Bajeti hii kwa usahihi na kwa ufundi zaidi ya vyombo vyetu. Kasomeni vyombo vya nje hata *BBC London, East African* na kadhalika wameeleza kwa ufundi zaidi Uzalendo wa kutetea maslahi ya Taifa lenu uko wapi hapa? (*Makofsi*)

Mambo yanayozungumzwa hapa lakini mambo yanayoandikwa tofauti na ya ajabu kabisa! Yaani hapa mtu anatetea kwa mfano Mheshimiwa Mwanri kazungumza vingine kabisa lakini siku ya pili kimeandikwa tofauti kabisa. Hata leo asubuhi nasikiliza, kweli kabisa sio sawa na vijana hawa wengine tumezungumza nao. Wao wanapeleka *story* sawasawa lakini *Editors* wanabadilisha. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, wakati wakichangia mjadala baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walisema kwamba hii ni Bajeti ya kufunga mikanda. Mimi sijasema kwamba Watanzania wafunge mikanda na wala siyo sera ya Chama cha Mapinduzi. Haipo kwenye Bajeti yangu na jana mse maji mmoja upande wa Upinzani alisema hivyo. Sio sahihi! Sio kweli! Tuseme ukweli jamani! Kwa sababu kama Bajeti ya kufunga mkanda kwanza ingekuwa ndogo sana. Tumetoka trilioni 4 mpaka 6.0 hiyo sio kufunga mkanda. Bajeti ya kufunga mkanda isingekuwa na elimu asilimia 18, isingepunguza kodi ya wafanyakazi wa kima cha chini.

Kwa hivyo kuna mambo mengi ambayo nasema sio Bajeti ya kufunga mkanda ni Bajeti ya kuanza kujitegemea. Tujitegemee sisi wenyewe tuanze na wananchi na hakika wako tayari kufanya hivyo. Wapo tayari mmoja mmoja kuchangia maendeleo yao, ili tutembee kwa *ku-pride* kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika ninalewa kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi walikuwa na wasiasi kuhusu bei ya mafuta na hasa mafuta ya taa. Lakini nasema kwamba hakuna haja ya kufunga mikanda, kwani chakula tunacho, mishahara inapanda, barabara zinajengwa na zinatoa ajira, watoto wetu wanakwenda shule, madawa yapo, reli ya kati itakarabatiwa na usafiri wa barabara utakuwa rahisi na mambo mengi mazuri katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nilichosema mimi ni kwamba, Kupanga ni Kuchagua. Tumechagua vipaumbele vichache ili tujenge msingi imara wa kukuza uchumi, ili tuongeze mapato ya wananchi, mapato ya Serikali, na Pato la Taifa kwa ujumla. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Kiongozi na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa maelezo yake kwamba Kambi ya Upinzani itashiriki kikamilifu katika juhudzi za kuondoa umaskini wa Watanzania. Aidha, napenda kumnuuu Mheshimiwa Hamad kama ifuatavyo: nanukuu: "Mara hii, tumezama kwa undani zaidi ili kutoa ushauri na suluhisho kwa mtazamo wetu. Kutokana na muda na uzoefu mdogo tulionao, tunaomba radhi kama kuna mapungufu katika kutoa ushauri wetu, uwe wa kimaandishi au kitakwimu. Nia yetu ni kumsaidia Mtanzania aondokane na umaskini wa kila aina." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba yako mapungufu mengi katika hoja na takwimu zilizowasilishwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani na Msemaji Mkuu wa Kambi hiyo, lakini kwa kuwa wameomba radhi, hatuna budi kuwasamehe na kuwapa fursa ya kuendelea kujifunza, ili kwa pamoja tushirikiane kulijenga Taifa letu. Serikali imefarijika pia kuona kwamba baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wa Kambi ya Upinzani wanabebe Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Elimu haina mwisho, nawaomba waendelee kujifunza kutoka CCM. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu na kutoa maelezo kuhusu baadhi ya hoja na mapendekezo ya Kambi ya Upinzani ili kuondoa utata ambao unaweza kuwachanganya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Msemaji Mkuu wa Fedha alisema eti mfumo wetu wa Bajeti bado hauko wazi kiasi cha Wabunge kushindwa kufuutilia vifungu vya mapato na matumizi. Nashangaa kwamba Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed hawezo kufuutilia na kujua fungu linaloitwa *O/C* na *Employment Allowance*. Maelezo kuhusu hoja hii yameshatolewa mara nyingi kuitia Kamati ya Fedha na Uchumi ambako mtoa hoja ni mjumbe. Namwomba Mheshimiwa Hamad Rashid, ndugu yangu, ni mjumbe wa Kamati hiyo. Lakini kama kuna taarifa nyingine Mheshimiwa Hamad Rashid angependa kuzijua, basi mimi niko tayari na naahidi kabisa tutashirkiana katika kumpatia.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani kuitia Hotuba ya Kiongozi wao, imehojoj ongezeko la matumizi ya kawaida kuliko matumizi ya maendeleo na kwamba eti hii ni kasoro kubwa. Hoja hii na kweli kama alivyo sema mwenyewe Mheshimiwa Rashid kwamba pale ambapo wameeleza sivyo, basi wanaomba radhi. Inadhihirisha kwamba pengine katika hili nalo hawakulielewa.

Mifano michache itasaidia kutoa maelezo kuhusu hoja hii. Katika Bajeti za nchi zinazoendelea kama Tanzania, tofauti kati ya Bajeti ya maendeleo na Bajeti ya kawaida ni ndogo sana na wakati mwingine haina maana kubwa. Kwa mfano, fedha za mfuko wa barabara (*Road Fund*) ambazo ni za matengenezo ya barabara (*maintenance*) ziko kwenye Bajeti ya kawaida. Katika Bajeti ya mwaka 2007/2008, fedha hizo zimeongezwa mara mbili. Hivyo ukijenga barabara mpya, baada ya miaka kadhaa itaongeza Bajeti ya kawaida kwa ajili ya matengenezo.

Mfano mwingine, ukijenga madarasa mapya, ukasajili wanafunzi wengi, utahitaji waalimu ambao watalipwa mishahara ambayo iko kwenye Bajeti ya kawaida, vivyo hivyo vifaa vya kufundishia, madaftari, na kadhalika. Ukjenga zahanati au vituo vya afya au hospitali, utaajiri madaktari, wauguzi na watumishi wengine wa afya. Mishahara yao na vitendea kazi vyao vinalipiwa kutoka Bajeti ya kawaida. Aidha, pamoja na mishahara ya watumishi wote wa Serikali, malipo ya madeni na pensheni yote yako kwenye Bajeti ya kawaida. Kwa maelezo haya, Bajeti ya Serikali ikiongezeka, basi Bajeti ya kawaida nayo inaongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kiongozi wa Upinzani Bungeni pamoja na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wametaka maelezo kuhusu Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama nilivyoeleza katika Hotuba yangu ya Bajeti, Tume hii imewasilisha Serikalini mapendekezo yake kuhusu vigezo vya kugawana mapato na pia kuchangia gharama za Muungano. Taarifa hiyo inafanyiwa mapitio ambayo yako katika hatua za mwisho. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wawe na subira kwani Mapendekezo ya Tume ni mengi na yanahitaji uchambuzi wa kina na majadiliano kati ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kabla ya kufanyiwa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani vile vile imependekeza hatua za mapato kutokana na uvunaji wa maliasili, utalii, uvuvi, misitu, na kadhalika. Jana kwa kweli Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ameeleza vizuri sana kwamba mipango kama hiyo Serikali inafanya. Kwa hiyo, kwa kweli kwa upande wa upinzani kuelezea sio kwamba jambo jipywa ambalo Serikali halijafikiria, lakini ni jambo ambalo Serikali pia imeanza kulitekeleza na Waziri amelieleza vizuri, lakini tunashukuru pia kwamba upande wa upinzani umelileta suala hilo.

Hata hivyo, niseme imekuwa vigumu kuangalia zile takwimu zao ambazo wamezileta. Hata hivyo, Serikali imeshafanya tathmini ya Sekta hii ya Maliasili na Utalii na imechukua hatua za kuongeza mapato ya Serikali katika Bajeti hii ya 2007/2008.

Katika Bajeti ya 2007/2008 Serikali inatarajia kukusanya mapato ya shilingi bilioni 74 kutoka kwenye Sekta ya Maliasili na Utalii. Maelezo zaidi yako kwenye Muswada wa Sheria ya Fedha na pia Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii atapata nafasi ya kuelezea zaidi. Lakini nasema ni jambo ambalo Serikali imeshaanza kulitekeleza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imetua mapendekezo juu ya mfumo wa Bajeti na hasa kuhusu vyanzo vingi vya mapato. Mengi ya mapendekezo ya Kambi ya Upinzani kuhusu mapato na kwa kweli ni orodha isiyo na uchambuzi wa kina na ambayo inahitaji kufanyiwa kazi zaidi.

Aidha, mengi ya mapendekezo hayo hayatekelezeki kwa kuwa hayana uwiano na hali halisi. Kwa mfano, Kambi ya Upinzani inapinda ongezeko la kodi kwenye mafuta kwa kuhofia kwamba litaongeza bei ya mafuta. Lakini wakati huo huo wanataka turejeshe *VAT* kwenye mafuta kama hatua ya kuongeza mapato. Ndugu zetu hawa wamesahau kwamba ni mwaka jana tu tuliondoa *VAT* kwenye mafuta kwa kuwa inaongeza mzigo wa kodi kila bei zinapopanda katika Soko la Dunia. Sasa tena mnataka tufanye hivi ili tuwaongezee mzigo wananchi?

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya mpango mbadala wa mapato unaopendekezwa na Kambi ya Upinzani mimi naona kwa kweli haujafanyiwa kazi. Kama alivyoeleza ndugu yangu Mheshimiwa Hamad Rashid ni kwamba uelewa kidogo kwa hivyo tutashirikiana kwa pamoja ili tuweze kusonga mbele.

Napenda niwakumbushe Kambi ya Upinzani kwamba Serikali haiamki tu na kuamua kutunga sera, kuna utaratibu ambaa unafanyika. Serikali imejenga utaratibu na uzoefu wa muda mrefu wa kutafiti masuala ya kodi na mapato kwa ujumla na kuhusisha wadau wa ndani na nje ya Sekta ya Umma, wakiwemo walipa kodi wenyewe, wataalam wa masuala ya kodi waliobobe, wachumi na kadhalika. Hawa ndio wanaoshauri Serikali kila mwaka kuhusu mfumo wa mapato ya Serikali na hivi sasa pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wakiwemo wa Upande wa Upinzani. Utaratibu huu ndio umetuwezesha kukusanya mapato hadi kufikia shilingi 260 bilioni kwa mwezi. (*Makofî*)

Haiwezekani kwamba Timu hiyo ya Wataalam ambaa ni pamoja na *TRA* yenye, imeshindwa kuona vyanzo vya mapato makubwa vinavyopendekezwa na Kambi ya Upinzani. Nashauri Kambi ya Upinzani kwa kweli turudi tuangalie upya mapendekezo haya kwa kushirikiana na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imehoji misamaha ya kodi na kudai kwamba haitolewi kwa utaratibu ulio wazi. Ningependa kumkumbusha Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwamba misamaha ya kodi inatokana na sheria zilizotungwa na Bunge, zenyelengo la kuhamasisha uwekezaji, katika uchumi na katika huduma za jamii. Usimamizi wa misamaha hiyo uko wazi na kama kuna ushahidi kwamba hivyo ninavyosema sivyo, nitafurahi kupata ushahidi huo. Hata hivyo, Serikali inafanya tathmini ili kubaini maeneo ya misamaha ya kodi ambayo hayana tena tija ili

kupendekeza marekebisho ya sheria husika kuondoa misamaha hiyo. Zoezi hili limeanza tangu mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani pia alihoji kiasi cha shilingi bilioni 15 kinachokadiria kuingia kwenye Bajeti kutokana na mauzo ya asilimia 21 ya hisa za Serikali katika Benki ya *NMB*. Ni kweli kwamba hisa hizo zitauza kwa thamani zaidi ya shilingi bilioni 15. Lakini kiasi hicho ndicho kitakachoingia katika Bajeti ya 2007/2008 baada ya kuondoa gharama zote za kufanikisha zaezi hilo na akiba ambayo inakaa katika mfumo wa upinafsishaji katika *PSRC*.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pia impendekeza kutoza kodi katika posho wanazopata Waheshimiwa Wabunge kwa kuhudhuria Vikao vya Bunge. Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 inatoza kodi ya mapato ya ajira isipokuwa posho zilizoainishwa katika kifungu cha 7(3) ambayo ni pamoja na posho za kufidia gharama za kufanyakazi nje ya kituo cha kazi.

Pendekezo la Kambi ya Upinzani linapingana na dhana nzima ya kutoza Kodi ya Mapato. Nina uhakika kwamba Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kwamba posho wanazolipwa ni posho ya kujikimu kwa kuwa ni ya kulipia gharama za wao kukaa hapa Dodoma. Hivyo ndivyo ilivyo pia kwa wafanyakazi wanaolipwa posho za kujikimu (*per diem*) wanaposafiri kikazi. Katika mfumo wa Kodi ya Mapato, hatutozi kodi marejesho ya gharama. Hilo nalo ni eneo la kujifunza kwa washauri wa Kambi ya Upinzani kuhusu masuala ya kodi.

Mheshimiwa Spika, ningependa nitoe maelezo kuhusu marekebisho ya kodi ya mafuta ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia. Ushuru wa bidhaa ya petroli umeongezwa kwa shilingi 22 kwa kila lita na ushuru wa mafuta kwa ajili ya mfuko wa barabara umeongezwa kwa shilingi 100 kwa lita. Jumla ni shilingi 122 kwa lita.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sehemu kubwa ya ongezeko la ushuru wa mafuta ni yale ya mfuko wa barabara kwa ajili ya kutengeneza barabara zetu ili ziweze kuwa nzuri na kupitika kwa mwaka mzima. Umuhimu wa barabara nzuri kwa uchumi wa nchi unafahamika. Kwa wakulima ambao wanalima barabara mbaya vyakula vinaoza haviwezi kununuliwa. Hata kwa akina mama wajawazito wakati mwininge wanapoteza maisha yao kwa sababu tu barabara mbovu na kwa maana hiyo gari haiwezi kupita, unambeba mama mjamzito kwa machela anakufa njiani na kadhalika. Hilo linajulakana. Kwa hiyo suala la barabara hata kama mtu kwa mfano una kiwanja tu sehemu fulani lakini barabara mbovu, thamani ya kiwanja kinakuwa chini, mara ikipita barabara thamani ya kiwanja kule kinakuwa juu bila kuweka kitu chochote kwenye kiwanja hicho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwininge, utafiti uliofanywa kwenye nchi kadhaa za Kiafrika unaonyesha kwamba kwa kila shilingi 100 ambayo haiwekwi kwenye matengenezo ya barabara mbaya, wasafirishaji wanaotumia barabara hizo wanapata

hasara ya shilingi 346 kutokana na ongezeko la gharama za matengenezo ya magari, magurudumu na mafuta mengi wanapotumia barabara mbovu.

Kwa hiyo, barabara zikitengenezwa, gharama za uendeshaji wa magari zitashuka. Wasafirishaji wasingegetegemewa kuongeza nauli kwa kuwa kodi hii inayokwenda kutengeneza barabara inaokoa gharama za uendeshaji wa magari yao. Kwa maana hiyo, ongezeko la kodi ya mafuta linalokwenda kwenye matengenezo ya barabara ni kwa faida ya wananchi, haitakiwi kuwa kero kwa mwananchi. Haitakiwa kuwa kero kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali itakuwa macho na wauzaji wa mafuta na wasafirishaji wa abiria na mizigo ili wasije wakapandisha bei ovyo na kuumiza wananchi. Kwa mfano, kwa sasa bei ya petroli ni shilingi 1,275 kwa lita. Ongezeko la ushuru la shilingi 122 linaweza kuongeza bei ya mafuta hadi shilingi 1,400 kwa lita na sio zaidi. Ili hatua hii isiwe *abused* na wauzaji wa mafuta (pamoja na kwamba wana uhuru) Shirika la *EWURA* litatakiwa kusimamia wauzaji wa mafuta ili kuhakikisha kwamba bei ya petroli na dizeli haipandishwi kiholela na kupita kiwango cha nyongeza ya ushuru. *EWURA* itategemewa kuwa macho na wakali sana kwenye suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiacha wauzaji wa mafuta, wasafirishaji nao wanawenza kutumia huu mwanya wa Serikali kupandisha kidogo ushuru wa mafuta kupandisha sana nauli za mabasi na magari ya mizigo na bidhaa. Hapa napo *SUMATRA* lazima ibebe jukumu lake la kusimamia kikamilifu wasafirishaji ili wasiwanyonge wasafiri na wananchi kwa sababu tu ushuru wa mafuta umeongezwa kidogo ili kupata fedha za kutengeneza barabara.

Tunasema Sh. 100/= kwa lita kwa maana kwamba kama unatoka sehemu moja, kama mtu unatoka Dar es Salaam mjini hadi Tegeta kama kilomita tano kwa hivyo shilingi 500. Kama shilingi 500 na watu unaobeba kwenye gari ukigawanya hapo unapata kama Sh. 10/= kwa kila mtu. Kwa hiyo, hatutegemei kabisa kwamba jambo hili litapandisha bei. Kama nilivyosema *SUMATRA* lazima wafanye kazi zao.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imetaka maelezo kuhusu thamani halisi ya gharama za ujenzi wa majengo ya Benki Kuu (*Twin Towers*), Kampuni ya Mwananchi *Gold*, Kampuni ya Meremeta na Kampuni ya *Alex Stewart Assayers*.

Mheshimiwa Spika, napenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu kwamba maelezo ya kina kuhusu masuala ya gharama za ujenzi wa Benki Kuu, Mwananchi *Gold*, Meremeta na Kampuni ya *Alex Stewart Assayers* niliyatoa hapa Bungeni wakati Bunge hili likijadili Muswada wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania mwezi April, 2006, pamoja na hayo napenda kusema kwamba Kamati ya Fedha na Uchumi nayo pia ilitembelea Benki Kuu na walishatoa maelezo yao kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Wilbrod Slaa - Mbunge wa Karatu, alitoa taarifa kuhusu habari zinazosambazwa katika mtandao wa *internet* zinazomshutumu

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania. Serikali inazo taarifa hizo zinazotoa shutuma mbalimbali dhidi ya Gavana wa Benki Kuu na baadhi ya wafanyabiashara hapa nchini.

Hata hivyo, Serikali haiwezi kutoa tamko lolote kwa kuwa chanzo cha habari hizo hakijathibitishwa na mara nyingi habari za *internet* hazina uhakika kama ni za kweli au za uongo. Aidha, Serikali ina vyombo vyake nya kufuatilia mambo haya.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ilitaka pia maelezo kuhusu tuhuma za ubadhirifu wa fedha katika akaunti ya madeni ya biashara ya nje katika Benki Kuu. Ningependa kutoa maelezo kwamba Serikali ilimuagiza Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kusimamia uchunguzi huu.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekwishaalika kampuni za kimataifa za ukaguzi wa hesabu zilete zabuni zao kwa kazi hiyo. Zoezi hilo linategemewa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, nawashauri Waheshimiwa Wabunge wavute subira ili tupate uhakika baada ya ukaguzi huu kufanywa kwenye Mahesabu yale ya Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika Hotuba yangu ya Bajeti, Serikali imeazimia kwa dhati kuharakisha utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mageuzi ya Sekta ya Fedha ili kukabiliana na changamoto mbalimbali zilizopo katika sekta ya fedha nchini, ikiwa ni pamoja na uwiano usioridhisha kati ya riba za mikopo na amana, upatikanaji wa mikopo ya maendeleo ya muda wa kati na ya muda mrefu, mikopo ya nyumba na rehani, upatikanaji wa huduma za kibenki kwa wananchi wengi hasa wale wa kipato cha chini, na uboreshaji wa mifuko ya dhamana ili iweze kuwanufaisha wajasiri amali wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali itazingatia wajibu wake katika kusimamia utekelezaji wa mageuzi yaliyobaki katika sekta ya fedha, hasa sekta ndogo ya benki, ili yakamilike kwa haraka na kuiwezesha sekta ya fedha kutoa mchango unaotakiwa katika uchumi na maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Mikopo kwa Njia ya Kukodi (*Lease Financing*) taratibu za kuandaa Muswada wa Sheria hiyo Bungeni zinakaribia kukamilika. Muswada huo unategemewa kuwasilishwa mwezi Oktoba/Novemba 2007. Lakini pamoja na kutaka kuwa na sheria mpya, tayari kuna benki ambazo zimeanza kufanya shughuli hizi kwa kutumia Sheria zilizopo hivi sasa. Benki hizo ni pamoja na *Stanbic, Standard Chattered, African Banking Corporation*, nk. Hivyo mikopo ya aina hii inapatikana japo kwa kiwango kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mikopo ya Nyumba (*mortgage financing*), Jumuiya ya vyombo nya fedha imenorodhesha markebishesha yanayotakiwa katika sheria mbalimbali. Marekebishesha yaliyopendekezwa ni pamoja na kifungu cha 10 cha Sheria ya Ardhi ili iwe rahisi kwa benki zinapotaka kuchukua mali ya mkopaji aliyeshindwa kulipa mkopo bila kungoja kibali cha mahakama (*Non –judicial mortgage enforcement*

*procedures).* Benki zinataka pia sheria itungwe kuhusu *condominium* ili kuwezesha mtu kumilikishwa *apartment* au *flat*. Vyombo vyta fedha vinataka pia taratibu za usajili wa dhamana (*legal – interest in properties*) ziimarishwe. Aidha, ukosefu wa vitambulisho vyta raia, ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, limetolewa wazo hapa kuwa ianzishwe Ofisi huru ya bajeti ili kuboresha bajeti zetu. Kwa kweli mimi sioni mantiki ya hoja hii, kwa kuwa hakuna maelezo ya kasoro za kimuundo yaliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa maandalizi ya bajeti yanasmamiwa kwa pamoja na Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Kazi hii inafanywa kwa uwazi mkubwa kushirikisha wakuu mbalimbali. Kama tulivyoshuhudia, mwaka huu Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kujadili Mwongozo wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa muda wa kati. Nafikiri mwezi huu ni muhimu katika mipango ili kuweka vipaumbele sahihi vyta matumizi ya rasilimali yetu. Siyo siri, Mheshimiwa Spika, kuwa amani, utulivu na mshikamano wa Kitaifa tunaojivunia misingi yeke ni hulka yetu ya kufanya mambo kwa uwazi na kushauriana.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu pia kukumbuka kuwa bajeti ni chombo muhimu cha kutekeleza sera na malengo ya Chama Tawala. Sera za Chama Tawala zinawekwa wazi katika Ilani ya Uchaguzi, na wananchi wanaamua ni Sera za Chama kipi wanataka zitekelezwe katika kipindi cha miaka mitano inayofuata. Kwa sasa, na naamini kwa miaka mingi ijayo, chagua lao ni Sera za CCM. Kupitia Serikali zake, mikakati ya kutekeleza sera hizo kupitia bajeti inawekwa wazi kwa utaratibu niliouelezea awali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamehoji juu ya ongezeko la kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwenye mafuta ya taa na ongezeko la viwango vyta ada ya mwaka ya leseni za magari. Kwa upande wa mafuta ya taa, Waheshimiwa Wabunge wameshauri, labda niseme ongezeko la mafuta ya taa ni shilingi 4 kwa lita. Kama mtu anatumia kwa mwezi mmoja lita moja kwa siku, siku 30 ni lita 120, yaani ni shilingi 120/= zaidi kwa mwezi mmoja. Lakini hata hivyo, Serikali imesikia maombi haya ya Waheshimiwa Wabunge pamoja wananchi na kwa hiyo itaondoa ongezeko hilo la shilingi 4 kwa lita na badala yake igawanywe kwenye bidhaa nyininge za mafuta ili kufidia pengo la mapato. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wameshauri kuwa Serikali iangalie tena mfumo unaopendekezwa wa kutoza ada ya mwaka ya leseni za magari ili kiwango cha shilingi 80,000 pia kitumike kwa magari ya ujazo wa injini zaidi ya 1500cc ambayo inajumuisha teksi nyingi, daladala na *pick-ups*. Waheshimiwa Wabunge pia wameshauri kiwango cha ada kwa piki piki na bajaji kipunguzwe ambapo mwanzo kilikuwa shilingi 80,000.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia wingi wa Waheshimiwa Wabunge wa CCM waliota ushauri huu, Serikali imekubali kufanya marekebisho yafuatayo katika hatua:-

- § Kusitisha ongezeko la kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwenye mafuta ya taa, na kuhamishia shilingi 4 kwa lita kutoka kwenye mafuta ya taa kwenda

kwenye kodi ya petroli na dizeli kwa shilingi 2 kwa lita kwa kila moja ya bidhaa hizo ili kufidia pengo la mapato. Viwango vinavyopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwenye mafuta ya taa kinapungua kwa shilingi 4 kutoka shilingi 56 hadi shilingi 52 kwa lita;
- (ii) Kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwenye petroli kinaongezeka kwa shilingi 2 kutoka shilingi 337 hadi shilingi 339 kwa lita;
- (iii) Kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwenye dizeli kinaongezeka kwa shilingi 2 kutoka shilingi 312 hadi shilingi 314 kwa lita;

Mheshimiwa Spika, Ada ya mwaka ya leseni za magari: Serikali imekubali kurekebisha mfumo wa kutoza ada ya mwaka ya leseni za magari ili kuwa na viwango vinne kulingana na ujazo wa injini kama ifuatavyo:-

- §  $0 - 500cc$ , hizi ni pikipiki pamoja na bajaji ambapo kwanza kabisa ilikuwa walipe shilingi 80,000/= lakini imerekebishwa na wanatakiwa kulipa shilingi 50,000/=
- §  $501cc - 1500cc$ , sasa watalipa shilingi shilingi 80,000/=, ni magari madogo madogo.
- §  $1501cc - 2500cc$ , magari ambayo ni madogo lakini kidogo makubwa ni shilingi 150,000/=
- §  $2501cc - 5000cc$ , mengi ya haya ni “mashangingi” ni shilingi 330,000/=.
- §  $5000cc$  na zaidi ni shilingi 175,000/=

Mheshimiwa Spika, narudia tena kukushukuru wewe kwa dhati kabisa pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kutoa hoja. Ahsante sana! (*Makofî/Vigelegele*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, hoja iliyio mbele yetu ni ya kuipitisha bajeti ya Serikali. Lakini, kabla sijawahoji, naomba nitoe maelezo kwamba kura hii kwa mujibu wa Kanuni ya 79(i) ni ya jina kwa jina (*Roll Call Vote*). Kwa hiyo, Waheshimiwa wote mtaitwa jina mmoja baada ya mwingine kwa utaratibu ambao Katibu ameuandaa na mtajibu NDIYO au HAPANA. Baada ya hapo, uamuzi utatokana na hicho mtakachokuwa mmeamua. Ikitokea kwamba kura zimefungana, Spika atakuwa na kura ya turufu. Baada ya maelezo hayo, kwanza kengele ipigwe maana kuna wenzetu labda wanakunywa chai, tutoe nafasi ili waweze kuingia humu Ukumbini.

*(Hapa Kengele Ilipigwa)*

Inaelekea Wabunge wote wamo ndani ya Ukumbi kwa sababu wanafahamu uzito wa jambo hili. Kwa hiyo, sasa namwita Katibu ili atuendeshee suala kura. (*Makofi*)

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa niite majina ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa utaratibu uliopo, wanapaswa kutamka NDIYO au HAPANA,. Na yule ambaye hayupo, tutaelezwa, na yule ambaye ana-*abstain*. Sasa, naomba kuita majina:

Mhe. Edward N. Lowassa .....	Ndiyo
Mhe. Batilda S. Burian .....	Ndiyo
Mhe. Muhammed Seif Khatib .....	Ndiyo
Mhe. Zakia Hamdani Meghji .....	Ndiyo
Mhe. Harith Bakari Mwapachu .....	Ndiyo
Mhe. Prof. Juma Athuman Kapuya.....	Ndiyo
Mhe. Dr. Mary Michael Nagu .....	Ndiyo
Mhe. John Pombe Joseph Magufuli .....	Hakuwepo
Mhe. Basil Pesambili Mramba .....	Ndiyo
Mhe. Prof. Mark James Mwandosya .....	Ndiyo
Mhe. Joseph James Mungai .....	Hakuwepo
Mhe. Dr. Juma Alifa Ngasongwa .....	Ndiyo
Mhe. Andrew John Chenge .....	Ndiyo
Mhe. Kingunge Ngombale-Mwiru .....	Ndiyo
Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda .....	Ndiyo
Mhe. Capt. John Zefania Chiligati .....	Ndiyo
Mhe. Dr. Ibrahim Said Msabaha .....	Ndiyo
Me. Dr. Hussein Ali Mwinyi.....	Ndiyo
Mhe. Anthony Mwandu Diallo .....	Ndiyo
Mhe. Philip Sang'ka Marmo .....	Ndiyo
Mhe. Margaret Simwanza Sitta .....	Ndiyo
Mhe. Prof. Peter Mahamudu Msolla .....	Ndiyo
Mhe. Nazir Mustafa Karamagi .....	Ndiyo
Mhe. Stephen Masatu Wasira .....	Ndiyo
Mhe. Prof. David Homeli Mwakyusa .....	Hakuwepo
Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe .....	Ndiyo
Mhe. Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa .....	Ndiyo
Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia .....	Ndiyo
Mhe. Sophia M. Simba .....	Ndiyo
Mhe. Bernard K. Membe .....	Ndiyo
Mhe. Johnson Paulo Mathias Mwanyika .....	Ndiyo
Anne S. Makinda .....	Ndiyo
Mhe. Dr. Maua Abeid Daftari .....	Ndiyo
Mhe. Abdisalaam Issa Khatib .....	Ndiyo
Mhe. Zabein Muhaji Mhita .....	Ndiyo
Mhe. Hezekiah Ndahani Chibulunje .....	Ndiyo
Mhe. Rita Louise Mlak.....	Hakuwepo

Mhe. Dr. Emmanuel John Nchimbi .....Ndiyo  
Mhe. Balozi Seif Ali Iddi .....Ndiyo  
Mhe. Mathias Meinrad Chikawe .....Ndiyo  
Mhe. Mwantumu Bakari Mahiza .....Ndiyo  
Mhe. Dr. Cyril August Chami .....Hakuwepo  
Mhe. Dr. Luka Jelas Siyame .....Ndiyo  
Mhe. Salome Joseph Mbatia .....Ndiyo  
Mhe. Dr. Diodorus Buberwa Kamala .....Ndiyo  
Mhe. Dr. Milton Makongoro Mahanga.....Ndiyo  
Mhe. Shamsa Selengia Mwangunga .....Ndiyo  
Mhe. Dr. Aisha Omar Kigoda .....Ndiyo  
Mhe. Ludovick John Mwananzila .....Ndiyo  
Mhe. Joel Nkaya Bendera .....Ndiyo  
Mhe. Daniel Nicodem Nsanzugwanko .....Ndiyo  
Mhe. Dr. David Mathayo David .....Ndiyo  
Mhe. Celina Ompeshi Kombani .....Ndiyo  
Mhe. Mustafa Haidi Mkulo .....Ndiyo  
Mhe. Christopher Kajoro Chiza .....Ndiyo  
Mhe. Lawrence Kego Masha .....Hakuwepo  
Mhe. Gaudentia Mugosi Kabaka .....Ndiyo  
Mhe. Jeremiah Solomon Sumari .....Ndiyo  
Mhe. Mohamed Aboud Mohamed .....Ndiyo  
Mhe. Dr. Charles Ogesa Mlingwa .....Ndiyo  
Mhe. Omar Yussuf Mzee .....Ndiyo  
Mhe. Gaudence C. Kayombo .....Hakuwepo  
Mhe. William M. Ngeleja .....Ndiyo  
Mhe. Dr. Abdallah Omar Kigoda .....Ndiyo  
Mhe. John Momose Cheyo .....Hapana  
Mhe. Mgana Izumbe Msindai .....Ndiyo  
Mhe. George Malima Lubeleje .....Ndiyo  
Mhe. William Hezekia Shellukindo .....Ndiyo  
Mhe. Anna Margareth Abdallah .....Ndiyo  
Mhe. William Jonathan Kusila .....Ndiyo  
Mhe. Gideon Asimulike Cheyo .....Ndiyo  
Mhe. Omar Shabani Kwaangw' .....Ndiyo  
Mhe. Juma Suleiman Nh'unga .....Hakuwepo  
Mhe. Jenista J. Mhagama .....Ndiyo  
Mhe. Job Y. Ndugai .....Ndiyo  
Mhe. Mohamed Hamisi Missanga .....Ndiyo  
Mhe. Hamad Rashid Mohamed .....Hapana  
Mhe. Dr. Wilbrod P. Slaa .....Hapana  
Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa .....Hakuwepo  
Mhe. Fatma Mussa Maghimbi .....Hapana  
Mhe. Magdalena Hamis Sakaya .....Hakuwepo  
Mhe. Kabwe Z. Zitto .....Hapana  
Mhe. Masoud Abdallah Salim .....Hapana

Mhe. Ibrahim Mohamed Sanya .....	Hapana
Mhe. Lucy F. Owenya .....	Hapana
Mhe. Muhonga S. Ruhwanya .....	Hapana
Mhe. Susan A. J. Lyimo .....	Hakuwepo
Mhe. Abubakar Khamis Bakary .....	Hakuwepo
Mhe. Anna M. Komu .....	Hakuwepo
Mhe. Grace Sindato Kiwelu .....	Hapana
Mhe. Philemon Ndesamburo .....	Hapana
Mhe. Chacha Z. Wangwe .....	Hakuwepo
Mhe. Said Amour Arfi .....	Hakuwepo
Mhe. Phares K. Kabuye .....	Hapana
Mhe. Mohamed Habib Juma Mnyaa .....	Hapana
Mhe. Dr. Ali Tarab Ali .....	Hakuwepo
Mhe. Mwanawetu Said Zarafi .....	Hapana
Mhe. Shoka Khamis Juma .....	Hapana
Mhe. Salim Abdallah Khalfan .....	Hapana
Mhe. Bakari Shamis Faki .....	Hapana
Mhe. Mwadini Abbas Jecha .....	Hapana
Mhe. Salim Hemed Khamis .....	Hapana
Mhe. Riziki Omar Juma .....	Hapana
Mhe. Halima J. Mdee .....	Hapana
Mhe. Ania S. Chaurembo .....	Hapana
Mhe. Fatma Abdallah Fereji .....	Hakuwepo
Mhe. Mkiwa Adam Kimwanga .....	Hapana
Mhe. Nuru Awadhi Bafadhili .....	Hapana
Mhe. Salim Yusufu Mohamed .....	Hapana
Mhe. Ali Said Salim .....	Hapana
Mhe. Savelina Silvanus Mwijage .....	Hapana
Mhe. Ali Khamis Seif .....	Hapana
Mhe. Maida Hamad Abdallah .....	Ndiyo
Mhe. Mohamed Rished Abdallah .....	Ndiyo
Mhe. Mohammed Abdi Abdulaziz .....	Ndiyo
Mhe. Bahati Ali Abeid .....	Ndiyo
Mhe. Ali Haji Ali .....	Hakuwepo
Mhe. Fatma Othman Ali .....	Ndiyo
Mhe. Aziza Sleyum Ally .....	Ndiyo
Mhe. Ame Pandu Ame .....	Ndiyo
Mhe. Kheri Khatib Ameir .....	Ndiyo
Mhe. Ameir Ali Ameir .....	Ndiyo
Mhe. Khadija Salum Ally Al-Qassmy .....	Hapana
Mhe. Idd Mohamed Azzan .....	Ndiyo
Mhe. Rostam Abdulrasul Azizi .....	Ndiyo
Mhe. Faida Mohamed Bakar .....	Hakuwepo
Mhe. Prof. Feethan Filipo Banyikwa .....	Hakuwepo
Mhe. Elizabeth Nkunda Batenga .....	Ndiyo

Mhe. Gosbert Begumisa Blandes .....	Ndiyo	Mhe.
Felister Aloyce Bura .....	Ndiyo	
Mhe. Pindi Hazara Chana .....	Ndiyo	
Mhe. Dr. Raphael Masunga Chegeni .....	Ndiyo	
Mhe. Diana Mkumbo Chilolo .....	Ndiyo	
Mhe. Samuel Mchele Chitalilo .....	Ndiyo	
Mhe. Mohammed Amour Chomboh .....	Ndiyo	
Mhe. Paschal Constantine Degera .....	Ndiyo	
Mhe. Hasnain Gulamabbas Dewji .....	Hakuwepo	
Mhe. Mohammed Gulam Dewji .....	Hakuwepo	
Mhe. Meryce Mussa Emmanuel .....	Hapana	
Mhe. Col. Saleh Ali Farrah .....	Ndiyo	
Mhe. Stephen Jones Galinoma .....	Ndiyo	
Mhe. Dr. Zainab Amir Gama .....	Ndiyo	
Mhe. Josephine Johnson Genzabuke .....	Ndiyo	
Mhe. Ali Juma Haji .....	Ndiyo	
Mhe. Dr. Haji Mwita Haji .....	Ndiyo	
Mhe. Zuleikha Yunus Haji .....	Ndiyo	
Mhe. Hemed Mohammed Hemed .....	Hakuwepo	
Mhe. Maria Ibeshi Hewa .....	Ndiyo	
Mhe. Parmukh Singh Hoogan .....	Ndiyo	
Mhe. Issa Kassim Issa .....	Ndiyo	
Mhe. Yahya Kassim Issa .....	Ndiyo	
Mhe. Athumani Said Janguo .....	Hakuwepo	
Mhe. Asha Mshimba Jecha .....	Ndiyo	
Mhe. Rajab Ahmad Juma .....	Ndiyo	
Mhe. Siraju Juma Kaboyonga .....	Ndiyo	
Mhe. Mgeni Jadi Kadika .....	Hapana	
Mhe. Balozi Hamis Suedi Kagasheki .....	Hakuwepo	
Mhe. Janet Bina Kahama .....	Ndiyo	
Mhe. Charles Muguta Kajege .....	Ndiyo	
Mhe. Teddy Louise Kasella-Bantu .....	Ndiyo	
Mhe. Mariam Reuben Kasembe .....	Ndiyo	
Mhe. Eustace Osler Katagira .....	Ndiyo	
Mhe. Vita Rashid Kawawa .....	Ndiyo	
Mhe. Charles N. Keenja .....	Ndiyo	
Mhe. Yono Stanley Kevela .....	Ndiyo	
Mhe. Vuai Abdallah Khamis .....	Ndiyo	
Mhe. Mwajuma Hassan Khamis .....	Hapana	
Mhe. Hassan Rajab Khatib .....	Ndiyo	
Mhe. Hassan Chande Kigwalilo .....	Hakuwepo	
Mhe. Felix Ntibenda Kijiko .....	Ndiyo	
Mhe. Estherina Julio Kilasi .....	Ndiyo	
Mhe. Juma Hassan Killimbah .....	Hakuwepo	
Mhe. Aloyce Bent Kimaro .....	Ndiyo	

Mhe. Halima Omar Kimbau .....	Ndiyo
Mhe. Fuya Godwin Kimbita .....	Ndiyo
Mhe. Paul Peter Kimiti .....	Ndiyo
Mhe. Rosemary Kasimbi Kirigini.....	Hakuwepo
Mhe. Capt. John Damiano Komba .....	Ndiyo
Mhe. Suleiman Omar Kumchaya .....	Ndiyo
Mhe. Florence Essa Kyendesya .....	Ndiyo
Mhe. Michael Lekule Laizer .....	Ndiyo
Mhe.James Daudi Lembeli .....	Ndiyo
Mhe. Castor Raphael Ligallama .....	Ndiyo
Mhe. Devota Mkuwa Likokola .....	Ndiyo
Mhe. Dr. Festus Bulugu Limbu .....	Hakuwepo
Mhe. Benedict Kiroya Losurutia .....	Ndiyo
Mhe. Sameer Ismail Lotto .....	Ndiyo
Mhe. Emmanuel Jumanne Luhahula .....	Ndiyo
Mhe. William Vangimembe Lukuvi .....	Ndiyo
Mhe. Riziki Said Lulida .....	Ndiyo
Mhe. Anna Richard Lupembe .....	Ndiyo
Mhe. John Paul Lwanji .....	Ndiyo
Mhe. Clemence Beatus Lyamba .....	Hakuwepo
Mhe. Ernest Gakeya Mabina .....	Ndiyo
Mhe. Joyce Nhamanilo Machimu .....	Ndiyo
Mhe. Ephraim Nehemia Madeje .....	Ndiyo
Dr. Binilith Satano Mahenge .....	Ndiyo
Mhe. Ezekiel Magolyo Maige .....	Ndiyo
Mhe. Yusuf Rajab Makamba .....	Ndiyo
Jackson Muvangila Makwetta .....	Hakuwepo
Benito William Malangalila .....	Ndiyo
Mhe. Anne Kilango Malecela .....	Ndiyo
Dr. John Samwel Malecela .....	Hakuwepo
Adam Kighoma Ali Malima .....	Ndiyo
Mhe. Halima Mohammed Mamuya .....	Hakuwepo
Ramadhani Athumani Maneno .....	Hakuwepo
Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya .....	Ndiyo
Mhe. Vedastusi Mathayo Manyinyi .....	Hakuwepo
Mhe. Abdul Jabiri Marombwa .....	Ndiyo
Mhe. Wilson Mutagaywa Masilingi .....	Ndiyo
Mhe. Masolwa Cosmas Masolwa .....	Ndiyo
Haroub Said Masoud .....	Ndiyo
Mhe. Janeth Mourice Massaburi .....	Ndiyo
Mhe. Joyce Martin Masunga .....	Ndiyo
Mhe. Zubeir Ali Maulid .....	Ndiyo
Mhe. Lucy Thomas Mayenga .....	Ndiyo
Mhe. Kiumbwa Makame Mbaraka .....	Ndiyo
Monica Ngezi Mbega .....	Ndiyo
Mhe. Mwanne Ismaily Mchemba .....	Ndiyo

Mhe. Mariam Salum Mfaki .....	Ndiyo	
Mhe. Col. Feteh Saad Mgeni .....	Ndiyo	
Mhe. Laus Omar Mhina .....	Ndiyo	
Mhe. Fatma Abdallah Mikidadi .....	Hakuwepo	Mhe.
Margreth Agness Mkanga .....	Ndiyo	
Mhe. Dunstan Daniel Mkapa .....	Ndiyo	Mhe.
Nimrod Elirehema Mkono .....	Ndiyo	
Mhe. Capt. George Huruma Mkuchika .....	Ndiyo	Mhe.
Martha Mosses Mlata .....	Ndiyo	Mhe. Lediana
Mafuru Mng'ong'o .....	Ndiyo	Mhe. Herbert
James Mntangi .....	Ndiyo	Mhe. Ali Ameir
Mohamed .....	Ndiyo	Mhe. Elisa David Mollel
.....Ndiyo	Mhe. Dr. Balozi Getrude	
Ibengwe Mongella .....	Ndiyo	Mhe. Dr. Samson Ferdinand
Mpanda .....	Hakuwepo	Mhe. Amina Chifupa
Mpakanjia .....	Hakuwepo	Mhe. Benson
Mwailugula Mpesa .....	Ndiyo	Mhe. Luhaga
Joelson Mpina .....	Ndiyo	
Mhe. Kilontsi Muhamma Mporogomyi .....	Hakuwepo	Mhe.
Felix Christopher Mrema .....	Ndiyo	Mhe.
Raynald Alfons Mrope .....	Ndiyo	Mhe. Ruth
Blasio Msafiri .....	Ndiyo	Mhe. Manju
Salum Omar Msambya .....	Hakuwepo	
Mhe. Dr. James Alex Msekela .....	Ndiyo	Mhe.
Balozi Abdi Hassan Mshangama .....	Ndiyo	Mhe.
Mwinchoum Abdulrahman Msomi .....	Ndiyo	Mhe.
Abbas Zuberi Mtemvu .....	Ndiyo	Mhe. Prof.
Idris Ali Mtulia .....	Ndiyo	
Mhe. Mtutura A. Mtutura .....	Ndiyo	
Mhe. Mudhihir Mohamed Mudhihir .....	Ndiyo	
Mhe. James Philipo Musalika .....	Ndiyo	
Mhe. Omar Sheha Mussa .....	Ndiyo	
Mhe. Mossy Suleiman Mussa .....	Ndiyo	
Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu .....	Ndiyo	
Mhe. Dorah Herial Mushi .....	Hakuwepo	
Mhe. Dr. Harrison George Mwakyembe .....	Ndiyo	
Mhe. Prof. Raphael Benedict Mwalyosi.....	Hakuwepo	
Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa.....	Ndiyo	
Mhe. Mbaruk Kassim Mwandoro.....	Ndiyo	
Mhe. Thomas Abson Mwang'onda .....	Ndiyo	
Mhe. Aggrey Deaisile Joshua Mwanri .....	Ndiyo	Mhe.
Hamza Abdallah Mwenegoha.....	Ndiyo	Mhe. Omar
Ali.....	Hapani	Mhe. Dr. Chrisant
Majiyatanga Mzindakaya.....	Ndiyo	
Mhe. Damas Pascal Nakei.....	Ndiyo	
Mhe. Richard Mganga Ndassa.....	Ndiyo	

Mhe. Sigifrid Seleman Ng'itu.....	Ndiyo
Mhe. Cynthia Hilda Ngoye.....	Ndiyo
Mhe. Hadija Saleh Ngozi.....	Hakuwepo
Mhe. Brg. Gen. Hassan Athuman Ngwilizi.....	Ndiyo
Mhe. Juma Abdallah Njwayo.....	Ndiyo
Mhe. Dr. Omari Mzeru Nibuka.....	Ndiyo
Mhe. Sijapata Fadhili Nkayamba.....	Ndiyo
Mhe. Said Juma Nkumba .....	Ndiyo
Mhe. Dr. Lucy Sawere Nkya.....	Ndiyo
Mhe. Tomus Musa Ntimizi.....	Ndiyo
Mhe. Lazaro Samuel Nyalandu .....	Ndiyo
Mhe. Ponsiano Damiano Nyami.....	Masomoni
Mhe. Richard Said Nyaulawa.....	Ndiyo
Mhe. Esther Kabadi Nyawazwa.....	Ndiyo
Mhe. Juma Said Omar.....	Hapania
Mhe. Ussi Ame Pandu.....	Ndiyo
Mhe. Mwaka Abdulrahaman Ramadhan.....	Ndiyo
Mhe. Shally Josepha Raymond.....	Ndiyo
Mhe. Kabuzi Faustine Rwilomba.....	Ndiyo
Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq.....	Ndiyo
Ali Said.....	Hapania
Kassim Said.....	Ndiyo
Sakila.....	Ndiyo
Mhe. Kidawa Hamid Salehe .....	Ndiyo
Mhe. Ahmed Ally Salum.....	Ndiyo
Mhe. Salum Khamis Salum .....	Hakuwepo
Mhe. Prof. Philemon Mikol Sarungi.....	Ndiyo
Mhe. Lucas Lumambo Selelili.....	Ndiyo
Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka.....	Ndiyo
Mhe. Haji Juma Sereweji .....	Ndiyo
Mhe. Peter Joseph Serukamba .....	Hakuwepo
Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby .....	Ndiyo
Mhe. Abdulkarim Esmail Hassan Shah .....	Ndiyo
Mhe. Beatrice Matumbo Shellukindo.....	Ndiyo
Mhe. Jacob Dalali Shibili .....	Ndiyo
Mhe. John Magale Shibuda.....	Ndiyo
Mhe. Dr. Guido Gorogolio Sigonda.....	Ndiyo
Mhe. George Boniface Simbachawene.....	Ndiyo
Mhe. Mohamed Said Sinani.....	Hakuwepo
Mhe. Mohammed Rajab Soud .....	Ndiyo
Mhe. Ali Haroub Suleiman .....	Hakuwepo
Mhe. Abdallah Salum Sumry .....	Ndiyo
Mhe. Eliatta Namdumpe Switi .....	Ndiyo
Mhe. Hafidh Ali Tahir.....	Ndiyo
Mhe. Fatma Abdalla Tamim.....	Hakuwepo
Mhe. Kaika Saning'o Telele.....	Ndiyo

Mhe. Fred Mpendazoe Tungu.....	Hakuwepo
Mhe. Martha Jachi Umbulla .....	Hakuwepo
Zaynab Matitu Vulu.....	Hakuwepo
Mhe. Anastazia James Wambura.....	Ndiyo
Mhe. Dr. James Mnanka Wanyancha.....	Ndiyo
Mhe. Godfrey Weston Zambi.....	Hakuwepo
Mhe. Mzee Ngwali Zubeir.....	Hakuwepo
Mhe. Mussa Azan Zungu.....	Ndiyo

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, huu ndiyo mwisho wa orodha ya Waheshimiwa Wabunge 319 waliopiga kura nikiacha kutaja jina lako Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Ahsante sana Katibu. Sasa mfanye hesabu ili mniipe matokeo.

*(Hapa kura zilihesabiwa)*

### **MATOKEO YA KURA**

Waheshimiwa Wabunge haya ndiyo matokeo ya kura zenu. Kwanza, nifafanue kwa mujibu wa Kanuni, uamuzi unaochukuliwa na Bunge ni lazima akidi iwe ni zaidi ya asilimia 50, kuanzia asilimia 50. Kwa kuwa ndani ya Ukumbi mko Waheshimiwa Wabunge 270 kati ya Wabunge 319 basi akidi ilikuwa imefikiwa. Kwa hiyo, uamuzi wowote ambao sasa unafikiwa ni halali. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge kwa sasa ni 319, kuna Wabunge ambao wa kuteuliwa, hawajateuliwa, kwa hiyo, tuna nafasi tatu.

Sasa ambao hawapo kwa asubuhi wakati tunapiga kura ni 49. Waliopo, yaani tuliopo humu ni 271, kwa jumla ilitakiwa 320, wamesahau kunihesabu mimi. Ni 320. Kwa hiyo, tuliomo ni 271. Kwa bahati njema sikulazimika kutumia kura ya turufu.

Matokeo ni kama ifuatavyo:- Kura za hapana ni 36, na kura za ndiyo ni 234. Kwa matokeo hayo hoja iliyokuwa mbele yetu na ambayo ni ya kupitisha bajeti ya mwaka 2007/2008 ya Serikali kama ilivyowasilishwa na Waziri wa Fedha, alitoa hoja hiyo na ikaungwa mkono kwa kura 234 dhidi ya 36. Sasa mmeipitisha hoja hiyo.

Kwa hiyo, sasa natangaza rasmi kwamba bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2007/2008 imepitishwa rasmi na Bunge hili. (*Makofî*)

*Order please!* Waheshimiwa Wabunge kwa nafasi yangu kama kiongozi hapa wa shughuli napenda niwapongeze nyote, kwa sababu kiwango cha hoja na mjadala kilikuwa cha juu sana Mimi sidhani kuna mwaka wowote pengine tangu uhuru ambapo mjadala umekuwa mzuri kiasi hiki.

Upande wa Upinzani ulikuwa na hoja ambazo zimewasilishwa vizuri, lakini kilele cha yote ni Waziri wa Fedha. Hata baadhi yetu ambao tunamfahamu miaka mingi leo

tumefurahi sana kwa sababu kidogo aliweka weka kajeuri jeuri hivi lakini basi mwana Mama aliye Waziri wa Fedha lazima aonyeshe jeuri kiasi fulani. (*Makofi/Kicheko*)

Baada ya hayo ninalo tangazo moja tu kwamba Kamati Mambo ya Nje kutakuwa na Kikao leo saa 8 mchana Chumba Na.227. La pili, msisahau Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho saa tatu na nusu ni Semina ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambayo inahusu *NBC*, ambayo ni benki yetu kubwa, wataeleza mafanikio waliyoyapata. Ni saa tatu na nusu katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Baada ya kusema hayo, sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi Jumatatu, tarehe 25 saa tatu asubuhi. (*Makofi*)

(*Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2007/2008 Ilipitishwa Rasmi na Bunge*)

(*Saa 06.47 Mchana Bunge lilahirishwa Mpaka siku ya Jumatatu,  
Tarehe 25 Juni, 2007 Saa Tatu Asubuhi*)